Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Tisa – Tarehe 18 April, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 104

**Usimamizi wa Hospitali za Wilaya**

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI** aliuliza:-

Kwa kuwa hospitali zote za Wilaya zinatakiwa kusimamiwa na Bodi za Afya na kuongozwa na *Medical Officers:-*

Je, ni hospitali ngapi za Wilaya nchini zimetimiza masharti hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi za Afya za Halmashauri zilianzishwa kwa Sheria Na. 7 ya mwaka 1982, Kifungu cha 86A. Jukumu kubwa la bodi hizi ni kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa Sekta ya Afya katika kuhakikisha kuwa huduma bora za afya zinapatikana na zinapaswa kuwajibika moja kwa moja kwa Halmashauri husika. Bodi hii ina wawakilishi wa jamii kutoka kwa watumiaji huduma za Afya, Kamati za hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na watoa huduma binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa Bodi ya Afya utakuwa na wajumbe saba na wataalam wanne kama ifuatavyo:-

Wajumbe wanne wanaotoka katika jamii, asilimia hamsini kati yao wawe wanawake, Mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya bila faida *(voluntary agencies*); mjumbe mmoja kutoka kwa watoa huduma za afya kwa faida (*private*); mjumbe mmoja ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii katika Halmashauri.

Kwa upande wa wataalam ni Mganga Mkuu wa Halmsahauri ambaye ni Katibu wa Bodi; Mchumi wa Halmsahauri; Mwakilishi wa Timu ya Uendeshaji ya Afya ya Mkoa *(Regional Health Management Team*) na mwakilishi wa Hospitali ya Wilaya au Mkoa pale ambapo hakuna hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi inalo jukumu la kuhakikisha jamii inapata huduma bora za afya inazozimudu na zinazoimarisha afya zao na upatikanaji wa rasilimali na mgawanyo wake unazingatia mahitaji ya ngazi zote za utoaji huduma za afya. Hospitali zote za Wilaya nchini zinatakiwa kuwa na Bodi za Afya za Halmashauri. Natoa agizo kwa Halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba wanaanzisha Bodi kwa zile Halmashauri ambazo hazina Bodi hizo na kwa zile Halmashauri ambazo zina Bodi hizo kuziimarisha.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna hospitali zipo hapa nchini pamoja na Wilaya ya Ludewa ambazo kwa miaka mingi hazijakuwa na Bodi hizi za Afya na hivyo kuzorotesha usimamizi na utendaji wa hospitali hizo kwa sababu ya kukosa mchango wa mawazo kutoka kwa wajumbe wa Bodi hizo.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kwamba zinakuwa na utaratibu unaoeleweka wa kufuatilia na kuhakikisha kwamba kila hospitali ya Wilaya inakuwa kweli na Bodi kwa mujibu wa sheria? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizi Bodi kama nilivyosema kwamba zimeanzishwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, Halmashauri yoyote ambayo haitakuwa na Bodi kama hii ina maana kwamba imekwenda kinyume cha sheria ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimetoa agizo kwa Halmashauri zile ambazo hazijaanzisha Bodi hizi waanzishe mara moja.

Na. 105

**Uhifadhi wa Pori la Akiba la Moyowosi -Kigosi**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:-

Kwa kuwa Kata za Ulowa, Bulungwa na Idahina zilizoko kwenye Jimbo la Kahama zinapakana na Pori la akiba la Kigosi-Muyowosi, hivyo kuwa mdau mkubwa wa kazi za uhifadhi wa pori hilo lenye maliasili nyingi:-

(a) Je, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Idara inayohusika imewashirikisha vipi wananchi wa Kata hizo kwa kuhakikisha maliasili iliyomo kwenye pori hilo inalindwa na kuhifadhiwa kwa mujibu wa sheria?

(b)Je, chini ya programu ya ujirani mwema inayoendeshwa na Idara ya Wanyamapori ni miradi mingapi imekamilishwa kwenye Kata hizo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na iligharimu fedha kiasi gani na kuhusisha sekta zipi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii napenda kujibu swali la kaka yangu Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Jimbo la Kahama, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekuwa inawashirikisha wananchi katika uhifadhi wa pori hilo kwa njia kuu mbili ambazo ni:-

Kwa kutoa elimu pamoja na kuwashirikisha katika kugawana manufaa yatokanayo na rasilimali ya wanyamapori kama vile kuwaruhusu kuendesha urinaji asali ndani ya pori, uvuvi wa samaki kwa ajili ya kitoweo na ajira kwa kuajiriwa kama vibarua kwa kazi za kufyeka mipaka, utengenezaji barabara, kujenga kambi za uwindaji wa kitalii na kutoa huduma kwa watalii.

Kuwatumia kama wasiri (*informers*) kuhusiana na mienendo ya majangili kwa uongozi wa pori. Kutokana na ushirikiano huo, jumla ya majangili 3,607 walikamatwa katika pori la akiba la Kigosi na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

(b) Wizara yangu inaendesha mpango wa ujirani mwema katika vijiji ambavyo vinapakana na Hifadhi za Taifa. Mpango huu haupo katika vijiji vinavyopakana na mapori ya akiba kama vile Moyowosi/Kigosi. Hata hivyo, kwa kutambua umuhimu wa wananchi, wananchi wa maeneo hayo hunufaika na mgawo wa asilimia 25 kutokana na uwindaji wa kitalii kupitia Halmashauri za Wilaya.

Aidha, katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2002 hadi 2007), Wizara yangu imechangia jumla ya Sh. 46,000,000/= kwa ajili ya kusaidia miradi ya maendeleo katika Kata za Ulowa, Bulungwa na Idahina. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa madarasa, nyumba ya mwalimu, zahanati, nyumba ya mganga na madawati.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu maswali ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Moja, kwa kuwa takriban miaka minne iliyopita Idara ya Wanyamapori kupitia Mfuko wake wa Uhifadhi wa Wanyamapori kwa ushirikiano na wananchi wa Kijiji cha Nyalwelwe, Kata ya Bulungwa walianzisha mradi wa ujenzi wa zahanati ili kuwasaidia wananchi hawa wasitembee muda mrefu kufika hospitali ya Kata iliyopo kilomita zipatazo thelathini. Hadi leo zahanati hiyo haijakamilika na wananchi wanaendelea kupata matatizo. Je, Wizara itawasaidia vipi wananchi hao kuhakikisha kwamba zahanati hiyo inakamilika haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa pori hili la akiba la Kigosi-Moyowosi linapakana na Kata nne za Jimbo la Kahama kwa maana ya Ushetu, Bulungwa, Idahina na Igwamanoni na katika siku za karibuni, pori hili limekuwa kichaka cha majambazi ambayo yanawavamia wananchi kila siku. Je, Wizara ya Maliasili na Utalii itawasaidia vipi wananchi hawa ambao kila siku wanaishi kwa hofu ya kuvamiwa na majambazi haya ambayo hatimaye yanakimbilia katika pori hilo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mradi wa zahanati Kijiji cha Nyalwelwe, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kweli kwa jitihada kubwa ambazo amezifanya kwa kushirikiana na Wizara yangu na wananchi wa Jimbo lake. Mradi huu kama mwenyewe alivyosema ulianza kujengwa kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana au kwa kupata usaidizi kutoka kwenye Wizara yangu.

Sasa kwa kuwa lengo lilikuwa ni kukamilisha nilikuwa naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu ikiwa ni pande ya pili ya mradi huu iko tayari kushirikiana na wananchi wa kijiji hiki cha Nyalwelwe ambao ni upande wa pili wa ushirikiano katika kukamilisha mradi huu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya shughuli hizi za Bunge tunamkaribisha ili aweze kuwasiliana na sisi aweze kuona ni namna gani wao wamejipanga kama wanufaika wa mradi kuweza kukamilisha shughuli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la tatizo la ujambazi kwenye eneo hili. Ni kweli kumekuwa na tatizo la ujambazi katika maeneo ya Kata alizozitaja na ni kweli kwamba tatizo hili haliishi pale linakwenda hata kwenye Kata za Ngogwa na hata Wilaya ya Bukombe. Wizara yangu kama tulivyojibu swali hapa jana imekuwa ikiimarisha kwa kutoa vitendea kazi kwenye vikosi vyake vya Kanda na kwa Kanda hii ya Kigosi ambayo tuna Ofisi ya Wanyamapori pale Kahama tayari kuna vitendea kazi ingawa si vingi sana, kuna magari na hata vifaa mbalimbali zikiwemo silaha kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hili. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kushirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Mambo ya Ndani kuomba kwamba pale ambapo inabidi doria ziwe zikifanyika lakini kasi ya doria hizi ziongezwe na mara nyingine ikibidi tufanye *operation* kwa ajili ya kukabiliana na majambazi hayo.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa asilimia ishirini na tano inayotolewa kwa ajili ya maeneo ya *blocks* za uwindaji ni ujirani mwema tosha kabisa kwamba wananchi watajua kwamba, wanyamapori ni mali na kwa kuwa miaka miwili iliyopita Serikali haikutoa hiyo asilimia ishirini na tano na kila mwaka tunatangaziwa katika kipindi cha bajeti kwamba kila Halmashauri itapata kiasi gani, je, ni kwa nini hatujapata asilimia ishirini na tano katika bajeti za miaka miwili iliyopita? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama alivyosema kwamba, miaka miwili iliyopita asilimia ishirini na tano haikutoka, jibu ni kwamba inawezekana haikutoka katika Wilaya yake ya Longido si kwamba haikutoka kwa nchi nzima kwa sababu kwa ujumla kuna Wilaya karibu arobaini ambazo zinapata hiyo. Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo yamepata. Kupatikana au kutokupatikana kwa asilimia hii ishirini na tano kunategemea na shughuli zilizofanyika katika kipindi hicho. Kwa hiyo, inawezekana katika mwaka anaozungumzia uwindaji haukufanyika kwenye eneo hilo ndiyo maana mapato hayakuwepo.

Na. 106

**Maporomoko ya Kalambo**

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA** aliuliza:-

Kwa kuwa maporomoko ya Kalambo ni ya pili kwa ukubwa Afrika:-

Je, Serikali itasaidia vipi kulinda hifadhi yake ya mazingira na kuyatangaza kuwa kivutio cha utalii?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Msitu wa Hifadhi ya Maporomoko ya Kalambo unakabiliwa na matatizo mbalimbali yakiwemo uvamizi kwa ajili ya makazi, uchomaji wa mkaa, upasuaji wa mbao na kilimo. Ili kudhibiti hali hii, Wizara yangu imepanga kupeleka watumishi wa misitu ili kuimarisha doria katika eneo hilo, kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Msitu *(Management Plan),* kuweka vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu, kutenga fedha kwa ajili ya kusafisha na kuhakiki mipaka ya msitu na kuanzisha mpango shirikishi wa ulinzi wa msitu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maporomoko ya Kalambo yapo mpakani kabisa na Zambia na ni kati ya vivutio vilivyobainishwa na uongozi wa Mkoa wa Rukwa kwa kushirikiana na Wizara yangu kama maeneo yanayoweza kuvutia watalii. Vivutio hivyo yakiwemo maporomoko ya Kalambo vimeanza kutangazwa katika majarida mbalimbali yatolewayo na Bodi ya Utalii Tanzania kama vile Jarida la *Tantravel* na Jarida la *Selling*

Tanzania. Aidha, Bodi ya utalii Tanzania imekuwa ikiwahamasisha Wakala wa biashara ya utalii kuhusu maporomoko hayo ili wajumuishe eneo hilo katika ratiba za watalii wanaotembelea Hifadhi za Taifa za Katavi, Ruaha na Mahale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kukamilika kwa ujenzi wa uwanja mpya wa ndege wa Kimataifa wa Songwe, Mbeya pamoja na barabara ya Tunduma-Sumbawanga kutaimarisha mawasiliano katika maeneo hayo na kuvutia wawekezaji kwa kuzingatia kuwa Mkoa wa Rukwa umepakana na nchi ya Zambia na hivyo kuwepo uwezekano wa kuvutia watalii na wawekezaji kutoka nchi zilizoko Kusini mwa Afrika.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, Waziri anaweza akatuthibitishia ni lini mpango huo anaousema utatengenezwa na kukamilika na kuanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Waziri anafahamu kwamba hata kama Bodi inatangaza Kalambo watalii hawawezi kufika pale kwa sababu barabara ya kufika Kalambo ni ya Zambia na siyo ya Tanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi si kwamba tumekaa tu kuna shughuli ambazo zinaendelea lakini *scale* yake ni ndogo sana. *Operation* zipo zinafanyika za kuhifadhi na kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwenye eneo hilo kwa mfano, katika mwaka uliopita tumekamata wavamizi ishirini na moja na pia tumekamata magunia 1,260 ya mkaa na tumekamata watu 37 ambao ni *intruders* ambao wamekwenda kuishi na kujenga katika eneo hilo. Mpango huu tunaouzungumzia ni mpango ambao tunategemea kuanza nao kwenye mwaka wa fedha ujao kwa sababu utakuwa ni mpango mkubwa utakuwa unachukua miaka kadhaa ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la barabara ni kweli kwamba barabara inatoka upande wa Zambia, malengo ni kuwa na miundombinu yetu ya ndani kwa maana hiyo barabara hii niliyoizungumzia ni barabara itakayofungua mawasiliano ya upande huo wa Kusini Magharibi mwa nchi yetu. Baada ya kuwa barabara hiyo imefika Sumbawanga, tunategemea mawasiliano kutoka Sumbawanga kwenda Kalambo yatakuwa ni rahisi zaidi wakati huo tukiwa tunaendelea kutumia mawasiliano yanayotoka Zambia, lakini tunajua njia ya uhakika zaidi ni kutumia njia zetu ili tuweze kufikia maeneo yetu ya utalii kwa kutumia barabara zetu za ndani. *(Makofi)*

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipendelea. Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameyatoa na nina swali moja la nyongeza. Kutokana na ile ni rasilimali kubwa sana nchini na maeneo yale wenzetu upande wa Zambia wanaingiza kipato kikubwa sana kwa ajili ya utalii ule wa maporomoko wakati sisi huku kwetu tumezubaa. Je, Waziri yuko tayari tukimaliza Bunge hili twende naye akaone hali halisi ya maporomoko hayo? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Unataka kuwa mtalii namba *one*. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nia yangu na nia ya Wizara yetu ni kutembelea maeneo yote. kwa hiyo, namhakikishia kwamba niko tayari kufuatana naye pamoja na uongozi wa Mkoa wa Rukwa kwenda kuona maporomoko hayo. (*Kicheko*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri lilijumuisha pia hifadhi ya Katavi na kwa kuwa maporomoko haya ni kivutio pia tunayo chemchem ya maji ya moto *(Hot spring)* kule Kijiji cha Maji ya Moto, Mpimbwe, Jimbo la Mpanda Mashariki. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhifadhi chemchem hii ya maji ya moto ambayo sasa hivi imevamiwa na makazi ya watu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza jitihada ambazo zimekuwa zikifanywa kwa ajili ya kudhibiti uharibifu kwenye maeneo yetu ya vivutio vya utalii zipo lakini kwa kiasi tumekuwa tukikwazwa na tatizo la uwezo kifedha. Hata hivyo kwa kuzingatia kwamba tuna mpango kabambe wa kukuza utalii tumekusudia kama tunavyojua kuleta watalii milioni moja ifikapo mwaka 2012.

Katika mikakati yetu ya kutekeleza ahadi yetu hiyo ya Chama cha Mapinduzi tunategemea kuvipitia vivutio vya utalii ili kuangalia matatizo yaliyopo na kuweka kwenye bajeti zetu mwaka hata mwaka ili tuweze kupunguza matatizo hayo.

Na. 107

**Mishahara ya Walimu Kucheleweshwa**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa walimu wamekuwa wakiteseka sana mara waanzapo kazi kwa kucheleweshewa mishahara yao au mishahara yao kupelekwa sehemu nyingine kama ilivyotokea kwa Mwalimu Charles Rwechungura *ED/PF 50373* wa Sekondari ya Chigunga, Geita ambaye mishahara yake ya miezi nane ilipelekwa Makambako Iringa:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondoa usumbufu na mateso wanayopata walimu wakati wa kuanza kazi?

(b) Je, ni lini mishahara ya mwalimu aliyetajwa itarejeshwa kwake?

(c) Je, Serikali inasemaje juu ya kudhibiti uzembe wa aina hiyo na isingekuwa vema walimu wanapocheleweshewa madai yao halali wawe wanalipwa na *interest* ya 10% kila mwezi kwa ajili ya ucheleweshaji?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa kero zinazowakabili walimu nchini ikiwa ni pamoja na kupata mishahara kwa wakati wanapoanza kazi. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kutoa maelekezo ya jinsi ya kujaza fomu za kudhibiti ajira Serikalini (*EB1*) na *personel Data form* kabla walimu hawajatoka vyuoni kwenda kuripoti katika vituo walivyopangiwa kufanya kazi. (Makofi)

Lengo ni kuhakikisha kuwa fomu hizo zinajazwa kwa usahihi ili kuepuka makosa ambayo yanachangia sana walimu wapya kuchelewa kuingia kwenye *payroll* au mishahara kupelekwa kituo kingine.*(Makofi)*

(ii) Kutuma fedha za kujikimu kupitia Hazina ndogo za Mikoa kabla walimu hawajaripoti vituoni.

(iii) Kuingia Mkataba na Benki ya *NMB*, utakaowezesha kulipa mishahara ya watumishi bila kusubiri mishahara itoke Hazina.

(iv) Kuanzisha vituo vya malipo *(pay station)* katika benki zilizo karibu na shule kwa walimu wa shule za sekondari ili kuepusha usumbufu na kurahisisha malipo ya mishahara.

(b) Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zilizopo zinaonyesha kuwa Mwalimu Joseph Rwechungura Charles mwenye Jalada *ED/PF 50373* aliajiriwa tarehe 26/7/2006 na kuingia kwenye orodha ya mishahara ya watumishi wa Serikali (*Payroll)* Oktoba, 2006.

Mishahara ya miezi sita kuanzia Oktoba, 2006 hadi Februari, 2007 ilielekezwa katika kituo cha kulipia mishahara Na. 638 cha shule ya sekondari Makambako kwa makosa. Mishahara hiyo imerejeshwa Wizarani na Mwalimu amelipwa kwa hundi.

Kuanzia mwezi Aprili, 2008 mshahara wake umeelekezwa katika kituo chake sahihi cha malipo ya mishahara Na 565 cha Moringe kinacholipiwa katika Benki ya *NMB*, Geita. Mishahara ya miezi miwili ya Agosti na Septemba, 2006 ni malimbikizo

kabla ya kuingia kwenye *payroll* ambayo atalipwa kupitia kwenye hundi ambazo zinapelekwa kuanzia leo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, mshahara wa mtumishi kuelekezwa katika kituo kingine inatokea kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kukosewa kwa namba ya Kituo cha Malipo wakati wa kuingiza kwenye kompyuta na makosa katika kujaza fomu za ajira.

Hata hivyo uchunguzi uliofanyika umebaini chanzo cha kosa hilo ni kukosewa kwa namba huko Hazina. Aidha, Wizara inamwomba radhi Mwalimu Joseph Rwechungura Charles kwa usumbufu alioupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni za fedha haziruhusu Serikali kulipa asilimia yoyote kila mwezi kama fidia kwa watumishi wanaocheleweshewa mishahara.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa mshahara wa mtu ndiyo uhai wake anapokwenda kufanya kazi, Mheshimiwa Waziri afikirie ni yeye amepelekwa kwenye shule hiyo kwa muda wa miezi minane bila mshahara.

Naomba anieleze ni mbinu gani ataitumia kuishi kwa Katibu Kata au Mwenyekiti wa Kijiji au *Headmaster* ili aweze kukubalika kuishi huku anakula bure?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, hivi sasa tunavyozungumza Mwalimu mhusika amekaa kwenye benchi la Mkaguzi wa Kanda ya Ziwa anasubiri kupewa *cheque* yake leo.

Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kwamba, huo ni uzembe na kuna tatizo ndani ya Wizara? Nasema hivi kwa sababu nimefuatilia muda mrefu mpaka swali likatoka na ndiyo analipwa leo na bado hajapewa hiyo hundi, kwa sababu kabla ya swali hili nilimwuliza umepata akasema bado sijapata. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niseme kwamba Wizara inamwomba radhi mwalimu kwa sababu tatizo lilikuwa ni la kiutaalam zaidi.

Katika kujaza fomu ambao ushahidi tunao na Mheshimiwa Mbunge anaweza kuja nikampatia, namba ya Kituo cha Malipo ni 565, kwa makosa ikagongwa Na. 638, kiutaalam hilo ni tatizo kubwa. Hatua za kisheria na kinidhamu zitachukuliwa kwa aliyesababisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kazi zinazofanywa na binadamu hupata makosa, si jambo la kushangaza na mwalimu huyu alikuwa anaishi kwa kupatiwa nusu ya mshahara wakati akisubiri mshahara huo, na ndiyo maana tulichelewa tena kumlipa *cash* money kwa sababu madai yale yaliingizwa katika madai pamoja na walimu wengine.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali ina mipango mizuri sana kuhusu walimu, na kwa kweli ililetwa Bungeni mwaka jana tukaithibitisha na ikaelekea ingekuwa kweli ni ukombozi wa walimu. Lakini Watendaji wa Serikali wanaofanya kazi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais. Hao watendaji wanashindwa kutimiza wajibu wao, wanashindwa kutekeleza maagizo ya Wizara, wanaoshindwa kufikisha mishahara hiyo kwa walimu ambao kwa kweli ndiyo chombo tunachokihitaji nacho tunachokitegemea. Je, Serikali sasa itaonyesha meno yapi kwa hao watendaji wabovu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi sana kwa sababu umekwishajibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakiri kabisa kwamba mishahara ndiyo chanzo kikubwa cha kumwezesha mwalimu kuishi na kumwezesha kufanya kazi zake kwa utulivu. Makosa yaliyotendeka tumeomba radhi, na ninasema tunajipanga vizuri sana katika kuhakikisha kwamba kero za walimu zinaondoka.

Pamoja na hayo Wizara inabidi kuwa angalifu sana baada ya kuonekana kwamba baadhi ya walimu uripoti na kuondoka ama kubadili vituo vyao vya kazi. Kwa hiyo, unapopata hali kama hiyo inabidi tutulie kidogo tufanye utafiti tujiridhishe ndipo tupeleke fedha, vinginevyo tunaogopa kulipa walimu hewa.

Na. 108

**Ufanyikaji wa Mitihani ya Kidato cha IV na VI**

**MHE. SALIM A. KHALFANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwanafunzi anayetakiwa kufanya mtihani wa mwisho wa Kidato cha IV na VI ikithibitika toka kwa Daktari kuwa anaumwa kiasi cha kutofanya mtihani kwa wakati huo huwa anaruhusiwa kutofanya mpaka hapo baadaye:-

Je, ni kwa nini mwanafunzi huyo baada ya kupona asiruhusiwe kufanya mitihani hiyo kama “*School Candidate*” na badala yake analazimika kufanya kwa kujitegemea *(Private Candidate)?*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mbunge wa Tumbe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) lina utaratibu wa kuwataka wasimamizi wa mitihani kutoa taarifa kuhusu matatizo mbalimbali (yakiwemo ya ugonjwa) yanayowapata watahiniwa wakati mitihani ikifanyika. Katika taarifa hizo wasimamizi hueleza aina ya matatizo waliyoyapata watahiniwa hao na hatua iliyochukuliwa kuyatatua katika vituo vya mitihani. Aidha, walimu wa masomo husika hushirikishwa katika kutoa maoni kwa Baraza la Mitihani la Tanzania kuhusu kiwango cha watahiniwa husika na hivyo kushindwa kufanya mtihani.

Baraza la Mitihani la Tanzania hupima uzito wa taarifa hizo na kufanya uamuzi wa ama kutoa matokeo ya mtahiniwa kama yalivyo iwapo hakuathirika sana au kutoa nafasi ya kufanya upya mtihani kama mtahiniwa wa shule iwapo mhusika aliathirika sana. Mtahiniwa anawajibika kuomba kufikiriwa kufanya mtihani kama mtahiniwa wa shule. Mtahiniwa ambaye hakuathirika sana kama atataka kufanya mtihani upya atafanya hivyo kama mtahiniwa wa kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtahiniwa aliyethibitishwa na daktari kuwa aliumwa kiasi cha kutofanya mtihani yupo katika kundi la watahiniwa wanaopewa nafasi ya kurudia mtihani kama watahiniwa wa shule iwapo ataomba kufanya hivyo.

**MHE. SALIM A. KHALFANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza kama ifuatavyo: -

Pamoja na tatizo hilo la wanafunzi kuhusu masuala ya ugonjwa na mambo mengine. Lakini kuna tatizo kubwa sasa hivi la wanafunzi ambao wanaamini kuwa wanapelekewa matokeo yasiyokuwa yao katika suala la mitihani, na wanapotaka kuthibitsha habari hizo inabidi waingie gharama ambazo wengine hawaziwezi. Hivi kuna njia gani rahisi ambayo Baraza la Mitihani na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itawasaidia wanafunzi pamoja na wazazi wao endapo itatokea hali ya kutoridhika kwa matokeo na mwanafunzi ili waweze kupata usahihi wa mambo bila ya kusumbuka sana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yasiyokuwa yao yanaweza kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na wanafunzi wenyewe kukosea namba. Lakini mwanafunzi mhusika anayo haki ya kudai, na kwa kufanya hivyo itamlazimu aandike barua na alipe fedha na Kamati Maalum itapitia tena matokeo yake na itampatia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante, lakini swali hili lilikuwa halihusiani.

Na. 109

**Wilaya ya Tunduru Kupewa Mbolea ya Ruzuku ya Chakula**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Tunduru inazalisha chakula cha nafaka kama Mahindi na Mpunga kwa wingi sana; na kwa kuwa, Mikoa jirani ya Mtwara na Lindi huitegemea Wilaya ya Tunduru pale panapotokea upungufu wa chakula:-

(a) Je, Serikali itakubali mapendekezo ya kuiweka Wilaya ya Tunduru kwenye orodha ya kupata ruzuku ya mbolea kwa mazao ya chakula badala ya mbolea ya ruzuku ya zao la Tumbaku kama ilivyo sasa?

(b) Je, Serikali itakubali kuipatia Wilaya hiyo mbolea ya ruzuku isiyopungua tani 600 kwa mwaka ikiwa ni moja ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ili kuongeza tija kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Tunakubaliana na mapendekezo ya Mheshimiwa Mtutura kwamba Wilaya ya Tunduru ipewe mbolea kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Ruvuma itaendelea kupewa mbolea yenye ruzuku kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya chakula hususan mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Ruvuma kupitia Kamati yake ya Ruzuku ya Mkoa ya Pembejeo inashauriwa kutoa mgao wa mbolea ya ruzuku kwa Wilaya ya Tunduru kulingana na umuhimu wa Wilaya hiyo katika kuzalisha mazao ya chakula.

Hata hivyo, napenda kusisitiza kwamba Serikali haina uwezo wa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wote na kukidhi mahitaji yote.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kama swali langu la msingi lilivyoeleza kwamba sasa hivi mapinduzi ya kilimo katika Wilaya ya Tunduru ni makubwa. Je, Wizara haioni haja ya kutazama sana Wilaya hii kwa sababu iko nyuma sana kimaendeleo ikapatiwa mbolea ya ruzuku kiasi ambacho tulikiomba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mtutura kwamba mbolea ambayo imepelekwa Tunduru kwa mwaka huu wa fedha ni nyingi kuliko kiasi alichokiomba. Kwa mfano, tumbaku ilipelekwa *NPK* tani 640, mbolea ya mahindi *urea* tani 500, na *DPA* tani 20 jumla tani 1160 na tani alizoomba ni tani 600 tu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwanza kabisa kwa kunipa nafasi hii na pili kwa kuniombea mbolea ya tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Wilaya ya Namtumbo kuna Tarafa ambazo zipo zaidi ya kilomita 260 katika Kata za Magazini na Lusewa, na Wilaya ya Namtumbo haina kituo cha mbolea ya ruzuku. Je, Serikali inaweza mwaka huu kutuwekea kituo cha mbolea ya ruzuku; kwa kuwa kuna umbali wa kituo kilichopo sasa hivi Songea Mjini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu tutakuwa na *stockist* ambao wanafundishwa na wanapewa mafunzo maalum na kupewa mikopo ili waweze kufikisha mbolea kwa wakulima kule walipo vijijini na *stockist* hawa watatoka kwenye vijiji. Kwa hiyo, kama kutakuwa na haja ya kuongeza vituo katika Jimbo lake tutafanya hivyo. Lakini *stockist* hao watafika huko pamoja na Vyama vya Ushirika ambavyo viko hai vitashughulika na suala hilo la kusambaza mbolea.

Na. 110

**Kilimo cha Mananasi – Kigoma Kaskazini**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO)** aliuliza:-

Kwa kuwa, zao la Nanasi linalimwa kwa wingi katika Kata ya Bitale hasa vijiji vya Bubango, Mkongoro na Chankele kwenye Jimbo la Kigoma Kaskazini; na kwa kuwa, wakulima wamekuwa wakitumia nguvu kubwa bila kupata msaada maalum kutoka kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na hata Serikali Kuu; na kwa kuwa, pia kuna tatizo kubwa la soko kwa zao hilo na pia bei ni ndogo kiasi kwamba, haiwezi kuwakwamua wakulima hao kwenye umaskini:-

(a)Je, Serikali kupitia mipango ya kilimo kama *DASIP, ASDP,* na mipango ya mikopo ya wajasiriamali itakuwa tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma kuweka mpango wa uzalishaji (Kigoma *Rural Pineapple Scheme*), usafirishaji na usindikaji wa nanasi ili kusaidia kuboresha maisha ya wananchi wa vijiji vilivyotajwa?

(b)Kwa kuwa, nanasi huharibika haraka, na vijiji vya Kigoma havina umeme ambao ungesaidia kusindika nanasi na kupata 'j*uice*;' Je, Serikali kwa kushirikisha

Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Nishati na Madini haiwezi kuangalia uwezekano wa kuunganisha mpango huo wa kilimo cha nanasi na mradi mdogo wa umeme vijijini ili manufaa yawe makubwa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha chini ya mradi wa *DASIP* na mpango wa *ASDP* ni wa mbinu shirikishi ambapo miradi hiyo hujumuishwa katika Mipango ya Kuendeleza Kilimo ya Wilaya *(DADPs).*

Nashauri Halmashauri za Wilaya Mkoani Kigoma zihamasishe zaidi wananchi na kutoa kipaumbele kwenye mradi wa kuzalisha, kusindika na kusafirisha nanasi kupitia *(DADPs).* Serikali tayari imeandaa na kupeleka Mwongozo wa kuandaa *DADPs* kwa kila Wilaya.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto kwamba, suala la usindikaji wa zao la nanasi ni muhimu; kwa kuwa ni zao linaloharibika kwa muda mfupi. Wakulima wanapaswa kupata taaluma ya hifadhi ya zao hilo ikiwemo usindikaji na ukaushaji kwenye ngazi za kaya. Kwa hiyo, tunazishauri Halmalshauri za Mkoa wa Kigoma kuwasiliana na Shirika la Viwanda Viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* kuhusu usindikaji wa nanasi katika Mkoa wa Kigoma.

Aidha, ili kusambaza huduma ya umeme vijijini Mkoani Kigoma tuna ushauri kuandaa na kuwasilisha mapendekezo maalum kwa Wizara ya Nishati na Madini.

**MHE. HAMAD R. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa asilimia isiyopungua 30 ya mazao yanayozalishwa nchini ama hupotea kutokana na kuharibika au kukosa soko. Je, Serikali baada ya kujua kwamba kuna teknolojia ambayo ingeweza kuhifadhi mazao hayo kwa muda mrefu bila kuharibika, sasa ikaitumia teknolojia hiyo ya *hybreeds* ili kusaidia kupunguza tatizo hili la uharibifu wa mazao na pia kuweza kusindika mazao hayo kwa urahisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba Mheshimiwa Hamad alikwishakuja ofisini akaniletea *document* ya kuhusu kukausha mazao mbalimbali n bado tunaifanyia kazi. Lakini kwa sasa hivi kama nilivyosema kwamba tuna DADPs hizi zinaweza zikatumika katika kuibua miradi mbalimbali ya kukausha mazao kwa ngazi ya kaya. Wananchi wanaweza kuibua miradi kwa kusaidiana na viongozi wa Wilaya katika kilimo na kujumuisha katika mipango ya maendeleo ya Wilaya yaani *DADPS.*

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake anasisitiza kuzishauri Halmashauri za Mkoa wa Kigoma kuhusu kushughulikia zao la nanasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri mwaka 1992 nilipata bahati ya kwenda Burundi nikiwa katika msafara wa aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa John Malecela, tulipofika kule tulikuta nanasi nyingi zipo uwanja wa ndege, nilipodadisi, nikaambiwa nanasi hizo zimetoka Kigoma, na mananasi yale yanapelekwa Brussels na yakiwa na *label* inayosema *the produce of* Burundi. Lakini yakiwa yametoka Kigoma, na niliporudi niliuliza swali Bungeni bado nilipewa ushauri ule ule kwamba Halmashauri za Mkoa wa Kigoma zishughulikie zao hilo. Je, Serikali haioni kwamba uwezo wa Halmashauri za Mkoa wa Kigoma kushughulikia suala la umeme ili waweze kuendeleza zao la nanasi haupo na kwamba ni jukumu la Serikali kusimamia suala hili?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwa ufasaha kabisa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba kwa kweli jukumu la kutazama namna gani mazao hayo yanahifadhiwa ni jukumu la Halmashauri zenyewe. Kwa bahati mbaya inaelekea kwamba huu mpango wa *DADPs* watu wengi hawajajua kuutumia sawasawa.

Kinachokosekana nafikiri ni watu kusaidia wananchi waweze kuibua miradi, na suala la umeme vilevile lazima lianzie chini kwenye Halmashauri ili lipelekwe kwenye Wizara husika ili kusudi wananchi waweze kufikishiwa nishati hiyo, na wote tunafahamu kwamba Wizara inayohusika ina mpango wa *Rural Electrification* kuweza kuwafikia wananchi katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana kabisa na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati umefika kwamba wananchi wa Kigoma wasaidiwe ili kusudi waweze kupata nishati na waweze kukausha au kuhifadhi zao la nanasi. Ahsante.

Na. 111

**Kukarabati Barabara za Nyashimo – Ngasamo na Lamadi –Mkula –Sapiwi**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Barabara za Nyashimo – Ngasamo na Lamadi –Mkula -Sapiwi ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao na wananchi wa Mikoa ya Shinyanga, Mara na Mwanza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati ili ziweze kupitika kwa muda wote pasipo kuwa na matatizo?

(b) Je, tatizo la madaraja yaliyopo Malili, Ngunga, Ngasamo na Shigala ambayo ni kikwazo kikubwa litapatiwa ufumbuzi lini?

(c) Je, ni lini barabara hizo zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRU MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Jimbo la Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nyashimo hadi Ngasamo lenye urefu wa kilometa 40 na ile ya Lamadi –Mkula – Sapiwi yenye urefu wa kilometa 15.5 ni barabara za Mkoa zinazohudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mwanza. Barabara hizi ziko chini ya usawa wa ardhi katika maeneo mengi zinakopita hususan maeneo yenye mashamba ya mpunga yanayochangia kwa kiasi kikubwa kuzidhoofisha barabara hizo hasa wakati wa maji yanapofurika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara hizo. Katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 jumla ya shilingi milioni 157.306 zimetengwa kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya kawaida, sehemu korofi na sehemu maalum kwa barabara ya Nyashimo hadi Ngasamo. Aidha, shilingi milioni 75.792 zimetengwa kwa ajili ya ya matengenezo ya kawaida na sehemu korofi na maalum barabara ya Lamadi -Mkula – Sapiwi. Kwa sasa barabara imefanyiwa matengenezo yaliyohusisha kazi za kuchonga barabara, kujenga makalvati, kuweka tabaka la changarawe na kuzibua mifereji. Wakandarasi wamemaliza matengenezo na barabara hizo na zinapitika bila tatizo.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nyashimo hadi Ngasamo ina madaraja mengi kutokana na mikondo mingi ya maji inayoingia katika Ziwa Victoria. Miongoni mwa madaraja hayo ni Malili, Shigala, Ngasamo na kalvati la Ngunga. Katika mwaka huu wa fedha Wizara kupitia Ofisi ya Meneja wa Wakala wa Barabara, Mwanza imefanya matengenezo yafuatavyo:-

(i) Daraja la Malili: Kazi ya ujenzi wa daraja hili iliyoanza mwezi Janauri, 2008 na imekamilika na daraja hili limeanza kutumika.

(ii) Daraja la Shigala : Ujenzi wa daraja hili la aina ya '*box*' Kalvati umekamilika mwishoni mwa Desemba, 2007 na hivyo kuondoa kero ya wananchi wa sehemu hiyo.

(iii) Daraja la Ngasamo: Matengenezo madogo (*preventive maintenance*) yamekamilika, hivyo kuliimarisha daraja hilo.

(iv) Daraja la Ngunga: Katika barabara ya Nyashimo - Ngasamo kuna kalvati katika kijijini Ngunga ambalo lipo katika hali nzuri na linapitika bila matatizo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo imeainishwa katika bajeti ya Wizara ya Miundombinu, Serikali ina mpango wa kujenga barabara ya Mwigumbi - Maswa - Lamdi yenye urefu kilometa 171 kwa kiwango cha lami, ambapo jumla ya shilingi milioni 400 zimetengwa kwa ajili ya usanifu wa kina baada ya upembuzi yakinifu na usanifu wa wali kukamilika. Zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri ilishatangazwa mwezi Januari, 2008. *(Makofi)*

Aidha, kwa upande wa barabara ya Nyashimo hadi Ngasamo, Serikali haina mpango wa kuijenga katika kiwango cha lami bali itaendelea na matengenezo ya kawaida kwa kiwango cha changarawe.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri nay a kuridhisha ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kweli napenda niwapongeze TANROADS kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuhudumia barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na pongezi hizi ni kwamba tatizo la barabara hizi ni unapotoka Bariadi kuja Duntwa au kwenda Sapiwi hiyo ni barabara ya *Trunk Road* ambayo ina uwezo wa kupitisha magari makubwa zaidi na yenye mizigo mikubwa zaidi. Lakini barabara kuanzia Ngasamo kuja Nyashimo ni *Regional Road* ambayo inapaswa yapite magari yasiyozidi tani 10. Sasa hii ya kutokuwa na uwiano wa barabara ni lini sasa Serikali itafumbua kitendawili hiki?

La pili, Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu nimuulize kwamba kwa kuwa, matengenezo ya barabara hizi yanafanyika kwa kiwango kidogo cha fedha. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kutumia fedha za kutosha ili barabara inapotengeneza basi iweze kudumu kwa muda mrefu badala ya kutumia tope kuweka barabarani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRU MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mipango ya Serikali tunatengeneza hizo barabara kwa awamu; na kwa awamu ya kwanza tumesema kwamba tuimarishe kwanza zile barabara ambazo tunaona kwamba wananchi wengi wana matatizo. Ndiyo maana katika swali la msingi nimesema kwamba barabara moja itajengwa kwa lami na ipo katika mpango huu. Sasa barabara hiyo ya Nyashimo hadi Ngasamo hiyo kwa kweli tutaendelea kuimarisha katika kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kutenga fedha nyingi ndugu zangu bajeti tunapitisha sisi hapa Bungeni, na hali yetu ya bajeti tunaifahamu. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba ni nia ya Serikali kutenga fedha nyingi, lakini

tunatengeneza barabara kulingana na uwezo wa upatikanaji wa fedha hizo kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaendelea kuziimarisha barabara hizo na tutaendelea kuzitengea fedha kadri Serikali itakavyokuwa na uwezo.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba Serikali haina mpango na ukizingatia kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Busega ametoa ufafanuzi kwamba magari makubwa yanayokusanya pamba yanatoka katika maeneo hayo.

Je, Serikali sasa haioni umuhimu angalau badala ya kuweka changarawe ikaandaa hata utaratibu wa kuweka lami nyepesi kama iliyopo katika barabara ya Dodoma Mjini kwenda Mnadani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRU MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema mwenyewe kwamba barabara hiyo inapitishia magari makubwa, sasa ukiiwekea lami nyepesi itaharibika kwa muda mfupi sana.

Lakini lami nyepesi mara nyingi inafaa kwa barabara zile ambazo yanapita magari machache na magari madogo. Kwa hiyo, mimi nimwombe tu awe na subira tuitengenezea kwa kiwango cha changarawe; na hapo tutakapokuwa na hali nzuri tutaitengeneza kwa kiwango cha lami halisi na siyo lami nyepesi.

Na. 112

**Fedha iliyotengwa kwa ajili ya Wafugaji**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi karibuni Serikali ilitangaza kuwa, imetenga shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya maendeleo ya wafugaji wanaoishi kandokando ya Hifadhi ya Ngorongoro:-

Je, Serikali imetenga au imepanga nini kuhusu jamii hiyo ya wafugaji wanaoishi kandokando ya hifadhi za akiba za Rungwa, Mhesi na Kizigo, Wilayani Manyoni?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Manyoni imetengewa jumla ya shilingi bilioni 1,207,216,608 na Wilaya ya Ngorongoro shilingi milioni 616,032,913 kati ya shilingi bilioni 59,330,165,000 zilizotengwa kwa nchi nzima mwaka 2007/2008 kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)*.

Hadi mwezi Machi, 2008 fedha zilizotumwa ni shilingi bilioni 1,031,679,522 kwa Wilaya ya Manyoni na shilingi milioni 496,208,000 kwa Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa tulizopata toka Wilaya ya Manyoni, iliibua miradi ya kuwaendeleza wafugaji waishio kando kando ya Hifadhi za Rungwa, Mhesi na Kizigo ya ujenzi wa majosho matatu na ukarabati wa majosho mengine matano kwa gharama ya shilingi milioni 82,500,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa malambo mawili na bwawa moja katika vijiji vya Winamila na Itagata kwa shilingi milioni 203, 000,000. Ukarabati wa Vituo vya Afya ya Mifugo katika vijiji vya Chikola na Itigi kwa shilingi milioni 20,000,000. Ununuzi na usambazaji wa madume bora ya ng'ombe na mbuzi wa maziwa na ununuzi wa vyombo vya usafiri kwa shilingi milioni 156,750,000. *(Makofi)*

Hadi sasa kazi zilizokamilika ni kutoa mafunzo kwa wafugaji 1,154 kuhusu mbinu bora za ufugaji, kununua madume bora 44 ya Boran na sita ya Mpwapwa, kukarabati majosho matano ya Kintinku, Magiri, Gurungu, Aghondi na Mbugani na kuanzisha Mifuko ya vikundi vya kuendesha majosho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wafugaji wanaozunguka Hifadhi ya Ngorongoro, jumla ya shilingi milioni 37,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuchimba malambo matatu katika vijiji vya Arash, Mashili na Malambo, kukarabati majosho sita katika vijiji vya Arash, Oloirobi, Enguserosambu, Aliilai, Ngoite na Soitsambu kwa shilingi milioni 56,000,000; kukarabati malambo mawili katika vijiji vya Kakesyo na Soitsambu kwa shilingi milioni 28,000,000 na kufuatilia magonjwa ya mifugo kwa shilingi milioni 8,000,000.

Kazi nyingine zilizopangwa ni kutoa mafunzo kwa wafugaji, kuboresha uwambaji wa ngozi na kuweka mitambo baridi ya kuhifadhia dawa za mifugo kwa gharama ya shilingi milioni 54,250,000.

Aidha, Halmalshauri imepanga kuendesha kampeni dhidi ya ugonjwa wa Homa wa Mapafu, ugonjwa wa Ndigana Kali na Kichaa cha Mbwa kwa gharama ya shilingi milioni 101,324,491. Vile vile, vikundi 10 vya wafugaji vitawezeshwa kuboresha koosafu za mifugo yao ambapo shilingi milioni 63,000,000 zitatumika.

Kulingana na taarifa za Halmasahuri, kazi zilizotekelezwa hadi sasa ni uchimbaji wa malambo matatu katika vijiji vya Arash, Mashili na Malambo, usanifu na uchoraji wa bwawa katika kijiji cha Arash, ukarabati wa lambo na josho katika kijiji cha Soitsambu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa wito kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na Ngorongoro waongeze bidii katika kukamilisha miradi waliojipangia kuitekeleza katika kipindi cha 2007/2008.

**MHE. PAUL J. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani ili kuweza kuwasaidia wananchi hao kuweza kujiletea maendeleo kwa haraka zaidi.

(b) Ni muda mrefu sasa Waziri au Naibu Waziri wa Wizara ya Mifugo hawajawahi kutembelea Wilaya ya Manyoni kujionea mapungufua makubwa ya miundombinu ya mifugo. Je, ni lini watapanga ziara kuja Manyoni? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi lilikuwa ni fedha zilizopelekwa katika Wilaya ya Manyoni zinazohusu Mradi wa *(DADPs)* ambazo zimeelezwa katika jibu la msingi. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusu Maofisa Ugani Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imeliona hili suala na kwamba katika nchi nzima palitakiwa kuwa na Maofisa Ugani wa Mifugo zaidi ya 16,000 na waliopo ni 2,550.

Hatua zinazochukuliwa katika bajeti ya mwaka huu tulionao Maofisa Ugani zaidi ya 950 wamepelekwa chuoni na katika mwaka ujao wengine 1,000 watapelekwa katika vyuo sita ambavyo vinahusika. Lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba hili pengo linaweza kuzuilika na hivyo baadhi ya Maofisa Ugani wengine watakaomaliza mwaka huu tutawapeleka katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Kuhusu suala la kutembelea Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni tutakaa na kujipanga vizuri mimi na Naibu Waziri na watendaji wangu ili kati yao mmoja aweze kutembelea kule na kuhakikisha hiyo miradi inatekelezwa kama alivyouliza.

Na. 113

**Uvuvi Kwenye Mabwawa yaliyopo Selous**

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO (K.n.y. MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwenye Mbuga ya Hifadhi ya Selous Wilayani Rufiji kuna Mabwawa ya asili yaliyojaa samaki wakubwa; na kwa kuwa, wakati wa utawala wa awamu zilizopita wananchi wa Rufiji walikuwa wamepewa vibali vya kuvua samaki kwenye mabwawa hayo kwa muda maalum lakini siku hizi Serikali haitoi vibali hivyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itawarudishia wananchi hao ule utaratibu uliokuwepo wa kuvuna maliasili yao kwa lengo la kuondoa umaskini?

(b) Je, Serikali itawalipa fidia kutokana na kunyimwa fursa ya kuvua samaki kwenye wakazi wa vijiji vya Ngorongo, Nyaminywili, Mtanza mpaka Mloka?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kumbukumbu tulizonazo zinaonyesha kwamba mwaka 1994 kibali cha kuvua samaki ndani ya Pori la Akiba la Selous kiliwahi kutolewa kwa wanavijiji wa Kata za Mwaseni na Ngorongo kutokana na maombi ya wanavijiji hao. Hata hivyo, kibali hicho kilisitishwa baada ya kuwepo ukiukwaji wa masharti yaliyotolewa.Vijiji vilitakiwa kuteua wavuvi wawakilishi na wavuvi hao kujiandikisha kabla ya kwenda kuvua.

Aidha, hao walitakiwa kusindikizwa na askari wakati wote wa kuvua. Hata hivyo, baadhi ya wawakilishi hao waliingia ndani ya hifadhi bila kujiandikisha na kuvua samaki kwa ajili ya kufanya biashara kinyume cha sheria na maelekezo waliyopewa na hivyo kukiuka utaratibu uliowekwa.

Kwa upande mwingine, wavuvi hao waliruhusiwa kuvua katika eneo hilo kwa sababu hapakuwa na mahitaji mengine kama vile Utalii wa picha uliojitokeza baadae. Utalii wa picha ulikomaa polepole kwa kuanzisha kambi mbili za utalii wa picha za Rufiji River na Mbuyu.

Hivyo uvuvi ulianza kuelekezwa kwenye mabwawa ambayo yalikuwa hayatumiki kwa utalii wa picha.

Kutokana na kukua kwa utalii, huo, sasa kuna kambi tisa (9) zinazoendesha utalii wa picha na kambi kumi (10) ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, kutokana

na kukua kwa utalii huo mpya, uwezekano wa kuruhusu wavuvi kuvua eneo lolote ndani ya Pori unakuwa mdogo sana ama kutokuwepo kabisa.

Kwa bahati nzuri yapo mabwawa mengi nje ya hifadhi katika maeneo ya vijiji hivyo kwa mfano, bwawa ya Zumbi lililopo kati ya vijiji vya Nyaminywili, Kipugia na Kipo, Bwawa la Ruwe karibu na Mkongo, Bwawa la Lugondo katika Kijiji cha Mtanza na Bwawa la Zimbwini lililopo Kibiti. Mabwawa haya yakisimamiwa vizuri na kuendelezwa, yanayo nafasi ya kuruhusu uvuvi endelevu na pia yanaweza kukidhi mahitaji ya samaki katika vijiji hivyo na ziada kwa ajili ya biashara.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la ulipaji wa fidia kwa wakazi wa vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, Serikali haiwezi kuwalipa fidia wananchi hao kwa kuwa hapakuwa na haki ya kisheria ya kufanya hivyo. Aidha, kutokana na uamuzi wake huo, Serikali haikukiuka utaratibu wowote katika kusitisha vibali vya wananchi kuvua ndani ya hifadhi. Napenda kurudia kuwaasa wananchi wa vijiji hivyo pamoja na vijiji vingine kandokando ya Pori la Selous kusimamia vizuri mabwawa yaliyopo nje ya Pori ambayo baadhi yake nimeyataja ili waweze kuvua samaki wa kutosha kutoka katika mabwawa hayo kwa ajili ya matumizi yao na matumizi ya kibiashara.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ambayo nimeridhika kidogo ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa hawa watalii watahitaji kupewa vyakula ambavyo ingesaidia kutokana na pale. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni vizuri waendelee kuvua ili kusudi pamoja na kupeleka katika masoko mengine waweze kutoa samaki kwa hawa wataliii?

(b) Kwa kuwa, wavuvi hawa katika maeneo haya mengine ambayo wamesema yataruhusiwa wamekuwa wakitumia nyenzo za kizamani.

Je, kwa utaratibu wa MKURABITA Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuweza kuwasaidia wavuvi nyenzo za kisasa ili waweze kuvua vizuri na pia vile vile kuwaunganisha na masoko makubwa kama vile ya Dar es Salaam kwa kutengeneza barabara ya kutoka Mkongo hadi Kibiti na barabara ya kutoka Mtanza mpaka kule Vikumburu Wilaya ya Kisarawe ili kusudi tuweze kufika Dar es Salaam kwa urahisi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Na. 12 ya Mwaka 1974 sehemu ya 10(1) inazuia uwindaji wa wanyama wakiwemo samaki katika maeneo ya Hifadhi ya Wanyamapori. Hivyo kufuatia sheria hii hatuwezi kuendelea tena kuvunja sheria na kuruhusu watu kuvua. Tunaamini kwamba kuna sehemu wakitumia mabwawa ambayo nimeyataja wananchi wataweza kuvua samaki wakatumia katika kambi za kitalii.

Kuhusu nyenzo za kisasa tunaomba wananchi wa Halmashauri ya Rufiji wanaoishi kandokando ya Bodi za Selous kwa kupitia Mradi wa *PADEP's* waweze kutumia Halmashauri zao na kuingiza katika miradi ya bajeti ambayo wataweza kuwapatia nyenzo za kisasa. Kwanza wapewe elimu pamoja na nyenzo za kisasa.

Kuhusu mambo ya barabara Wizara yangu kwa kweli haihusiki na mambo ya barabara nafikiri itabidi wapitie katika Wizara ya Mindombinu au katika Halmashauri zao kwa ajili ya kujengwa hizo barabara.

Na. 114

**Ajali za Magari Kati ya Ubungo na Kibamba**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wengi wamepoteza maisha kwa kugongwa na magari yaendayo kwa kasi, kwenye baadhi ya maeneo kati ya Ubungo na Kibamba ambapo ajali nyingi zinatokea kwenye kituo cha mabasi na kituo cha kukagua mizigo Mbezi Luis:-

(a) Je, ni wananchi wangapi wamegongwa na magari kati ya Ubungo na Kibamba katika miaka mitatu iliyopita?

(b) Kwa kuwa, ajali nyingi zinatokea kwenye maeneo machache tu ya barabara. Je, Serikali inakusudia kuchukua hatua gani kupunguza ajali hizo?

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kuwalipa kifuta machozi familia zinazopoteza watu hao kutokana na ajali za barabarani?

**NAIBU WAZIRI MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu suala la Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi waliogongwa na magari kati ya Ubungo na Kibamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita yaani Mwaka 2005, 2006 na 2007 ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2005 waliogongwa walikuwa 216 waliofariki 44, Mwaka 2006 waliogongwa ni 275, waliofariki 58 na mwaka 2007 waliogongwa ni 383 na waliofariki 79.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ambazo Serikali inachukua ili kupunguza ajali barabarani pamoja na kusimamia ipasavyo sheria na kanuni zinazohusu usalama barabarani.

Pili, kutoa elimu kwa watumiaji barabara kuhusu sheria na kanuni za usalama barabarani.

Tatu, kuwadhibiti madereva wanaokwenda mwendo wa kasi kwa kutumia vipima mwendo wa kasi. Nne, kufanya doria na ukaguzi kwenye barabara kuu na kuchukua hatua kwa madereva wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani.

Tano, kuainisha maeneo yanayotokea ajali mara kwa mara na kuwasiliana na *TANROADS* Halmashauri za Miji na Manispaa ili kuongeza na kurudisha alama za kuongoza magari barabarani. Sita na mwisho kudhibiti mwendo wa kasi wa mabasi ya abiria kwa kutumia ratiba za magari kutoka mkoa mmoja hadi mwingine inayotolewa na *SUMATRA* kwa kuweka *checkpoint* barabarani ili kuwabaini wakosaji na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kisheria kwa wanaopata ajali za barabarani au jamaa zao kwa wale wanaopoteza maisha kupitia Sheria na Bima ya Magari. Hivyo iwapo mtu atapoteza maisha kutokana na ajali za barabarani atalipwa kupitia Bima iliyowekwa katika gari iliyosababisha ajali.

Aidha, wahanga au ndugu zao wanaweza pia kudai na kulipwa fidia na wamiliki wa magari au madereva wa magari yaliyopata ajali kupitia Mahakamani iwapo Bima iliyowekwa haikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kuwakumbusha watumiaji wote wa barabara kuwa makini katika matumizi ya barabara ili kupunguza wimbi la ajali hapa nchini ambalo linachangia kupunguza nguvu kazi ya Taifa kuongeza idadi ya yatima, walemavu, uharibifu wa mali na hatimaye kudhoofisha uchumi wa nchi yetu.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hizi takwimu zinatisha, kwamba ni katika miaka mitatu waliokufa watu 181. Kwa kuwa *RDC* na kwa kuwa Waziri wa Miundombini alipojibu swali hapa Bungeni walikubali kwamba yatawekwa matuta katika maeneo haya ili kupunguza ajali hizi zinazotokea. Je, matuta hayo sasa yatawekwa lini ni mpaka tuishe ndiyo yawekwe?

Pili, kwa kuwa tatizo kubwa linatokana na wananchi kutokujua matumizi sahihi ya barabara hasa barabara yenye magari mengi kama hii tunayoizungumzia. Wizara ya Mambo ya Ndani haioni kwamba ni wakati sasa wa kufanya mafunzo ya makusudi kwa wananchi hawa na hasa watoto wa shule ili kuhakikisha ajali hizi zinapunguka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matuta barabarani hilo ni suala ambalo tutalijadili na wenzetu wa Miundombinu tuone ni jinsi gani tunaweza tukafanya. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada zinafanyika katika maeneo mengi, sio maeneo hayo tu lakini katika Tanzania nzima na hii inakwenda kufuatana na hali ya kifedha tuliyonayo lakini tutalipwa kipaumbele na tutalizungumza na wenzetu wa Wizara ya Miundombinu.

Kuhusu suala la pili, mafunzo ni kweli yanatolewa lakini isitizamwe kwamba ni suala la Serikali peke yake. Lakini tunataka ushirikiano kati ya wananchi na Serikali. Kwa sababu inatokea wakati ambapo kuna madereva ambao hawana leseni, kuna madereva ambao hawafuati taratibu, kuna madereva wanaendesha magari wakati wamelewa na kadhalika.

Kwa hiyo, sheria kweli zinakuwepo, lakini nafikiri kweli ni suala ambalo litataka kuwepo na ushirikiano wa karibu zaidi kati ya raia, wananchi na Serikali na kwa hiyo tutakuwa tayari kufanya lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la mafunzo na kuelimisha raia tutalifanya kwa nguvu zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 115

**Gharama za Kuwapeleka Washtakiwa Rumande/Mahakamani**

**MHE. ALOYCE B. KIMARO** aliuliza:-

Kwa kuwa, uhalifu umeongoezeka sana katika Kata mbalimbali za Jimbo la Vunjo; na kwa kuwa, ni wajibu wa Serikali kuwachukulia hatua kali za kisheria wahalifu hao pindi wananchi wanapotoa taarifa zao:-

(a) Je, Serikali inasemaje kwa kitendo cha kwamba, mwananchi aliyeibiwa na kutoa taarifa Polisi kutoa shilingi elfu saba (7,000/=) kama nauli kila wakati mshtakiwa anapotakiwa kupelekwa rumande au Mahakamani?

(b) Je, ni Wizara gani yenye jukumu la kuwapeleka wahalifu rumande au Mahakamani pale inapobidi; na ni kwa gharama ya nani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikijibu swali Na. 52 lililoulizwa na Mheshimiwa Esterina Julio Kilasi, Mbunge wa Mbarali siku ya tarehe 11 Aprili, 2008 nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba ni jukumu la Serikali kugharamia gharama zote

katika Makosa ya Jinai ikiwemo kuwakamata watuhumiwa, kuwasafirisha kwenda rumande au Mahakamani, kuwalipa mashahidi/walalamikaji, wazee wa baraza na huduma nyinginezo. Wizara yenye jukumu la kuwakamata wahalifu wa jinai na kuwapeleka kituo cha Polisi, Mahakamani na Rumande ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurudia wito wangu kwamba, iwapo wapo baadhi ya Askari Polisi na Askari Mgambo ambao hudai malipo kwa kutekeleza wajibu huo, basi wananchi wasisite kutoa taarifa katika vyombo vya Serikali katika maeneo yao ili hatua za kinidhamu na kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao ili kumaliza tatizo hili.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, Waziri anakubaliana na mimi kwamba ni vyema wale ambao walikwishatozwa shilingi 7,000/=, ili kuwapeleka wahalifu Mahakamani/Rumande wakadai Serikali iwarudishie fedha zao?

Je, Naibu Waziri ama Waziri mwenyewe atakubaliana na mimi nikimwomba aje jimbo la Vunjo ili tushirikiane wote kwa pamoja kuwasikiliza wananchi walio na kero kubwa za uhalifu ili tuweze kupata ufumbuzi wa matatizo yao kwa haraka?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwamba Serikali haina taarifa zozote kuhusu wananchi ambao wametozwa shilingi 7,000/=, 7,000/=. Kama nilivyosema ni wajibu wa Wizara kutoa huduma hiyo na wala si wananchi na kama zipo kesi za namna hiyo tutakuwa wa kwanza kusikiliza na kwa ushahidi wa kutosha na kufahamu ni vipi na kujua waliwapa watu gani ambao walipokea hizo shilingi 7,000/=, kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge.

Kuhusu suala la pili, mimi mwenyewe binafsi na naweza kusema kwa niaba ya Waziri na maofisa katika Wizara yetu tuko tayari kutembelea jimbo la Vunjo na kuwasikiliza wananchi. Kama nilivyowahi kusema ndiyo kazi yetu kusikiliza kilio cha wananchi, kusikiliza matatizo ya wananchi na kuona ni vipi tunaweza tukatatua matatizo ya wananchi. (*Makofi)*

Na. 116

**Sheria ya Ndoa Na. 5 ya Mwaka 1971**

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH** aliuliza:-

Kwa kuwa, Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inatambua kisheria ndoa ya mke mmoja, wake zaidi ya mmoja na ndoa za kimila:-

Je, ni kwa nini Serikali wakati wa mafao kama vile matibabu na kadhalika, huwa inatambua mke mmoja tu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA(K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Sheria ya Ndoa Na. 5 ya Mwaka 1971 ambayo kwa sasa ni Sura ya 29 ya Sheria za Nchi inatambua ndoa za aina tatu yaani ndoa za Kidini, Kimila na Kiserikali. Sheria hiyo imetoa haki kwa kila mtu kuchagua aina ya ndoa inayomfaa. Baadhi ya dini na baadhi ya makabila ya Tanzania yanaruhusu ndoa ya wake wengi kama inavyotambuliwa na Sheria ya Ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida maslahi au mafao ya mtumishi huwa ni makubaliano kati ya mwajiri na mwajiriwa. Hata hivyo ipo miongozo bayana inayoweka aina ya maslahi au mafao anayoweza kupata mtumishi kwa kuzingatia aina ya utumishi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na utaratibu wa kuweka idadi ya watu katika familia wanaostahili mafao kwa mujibu wa na kanuni za utumishi Serikalini. Utaratibu huo upo kwa madhumuni ya Serikali kuwa na uhakika wa kupanga mipango sahihi wa maslahi ya watumishi na mafao yanayowahusu pamoja na familia zao na kuwezesha kupanga bajeti kwa kuzingatia idadi ya wategemezi ambao wanapata stahili na wanaozidi namba hiyo hawapati. Suala la mafao kutolewa kwa mke mmoja, kwa idadi maalum ya watoto na kwa idadi maalum ya wategemezi inatokana na uwezo mdogo wa Serikali kifedha kuweza kuwahudumia wake wote, watoto wao wote pamoja na wategemezi wote wa mtumishi wa Serikali. Lakini pia utaratibu huo unalenga katika kuweka usawa wa mafao baina ya watumishi wanaostahili mafao yanayofanana.

Endapo Serikali haitaweka utaratibu maalum wa kudhibiti idadi ya wanufaika wa mafao kuna hatari ya Serikali kushindwa kupanga mipango madhubuti ya jinsi ya kuboresha maslahi au mafao ya watumishi kwa kupanga bajeti iliyosahihi.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza.

Kama alivyojibu Mheshimiwa Waziri kwamba kufuatana na uwezo wa Serikali ndiyo sababu ya kuweza kutoa idadi maalum kwa kipindi maalum kwa mafao ya mtumishi wa Serikali.

Je, kwa yule ambaye ana wake zaidi ya mmoja na watoto zaidi ya wanne anaweza kuwatumia wanne hawa wakati mwingine na mke mmoja hapa na mke mmoja wakati mwingine?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu umewekwa na katika utaratibu huo kwa hali ya kawaida mke wa kwanza ndio hupewa kipaumbele.

Kwa hiyo, yule mwenye wake wengi ni chaguo lake kwamba mtu anayetaka kuoa ajue kwamba mke wake wa kwanza ndio kawaida anafahamika na ndiyo atakayepata mafao hayo pamoja na watoto wake.

Na. 117

**Kuwasaidia Wachimbaji Wadogo Wadogo**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 Ibara ya 39 aya ya (d) na (e) inazozungumzia kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo na kujenga mahusiano mazuri kati yao na wananchi:-

(a) Je, Serikali inaweza kuwaambia wananchi wa Bukombe na Bunge hili kuwa, wachimbaji wadogo wadogo wa Kelezia, Shenda Katende na Mwabomba wamesaidiwaje?

(b) Kama hawajasaidiwa, na huku wana mahitaji makubwa sana ya vitendea kazi kama vile Jenereta, *Compressor na Water pumps.* Je, Serikali inawaambia nini wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwasaidia wachimbaji wadogo wa maeneo ya Katente na Kelezia Wilayani Bukombe, Kituo cha Biashara Adhimu ya Dhahabu (*Fair Trade Gold Centre*) kilijengwa Ushirombo. Kituo hiki kinachoendeshwa na Kampuni ya *Africa Precious Metals Ltd*.

Kampuni tanzu ya *FBME Bank Ltd.* ni matokeo ya ushawishi wa Serikali kwa kampuni binafsi kwa lengo la kuwasaidia wachimbaji wadogo. Kituo hiki kimelenga kuwasaidia wachimbaji wadogo wa Katente, Kelezia na maeneo mengine ya Wilaya ya Bukombe katika kuuza dhahabu yao, kupata mikopo ya kununua mashine na vifaa vya uchimbaji na huduma za Kibenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kikundi cha Ushirika wa Wachimba Madini cha Katente kiweze kutambulika na taasisi za fedha na hatimaye waweze kukopeshwa, Serikali imekipata kikundi hicho leseni tano za uchimbaji mdogo wa madini *(PML).*

Aidha, Wizara yangu kwa kutumia Maofisa Madini walioko katika Ofisi za Madini za Shinyanga na Kahama hutoa mafunzo kuhusu njia bora ya utafutaji, uchimbaji na uchenjuaji madini kwa wachimbaji wadogo wa madini wa Mkoa wa Shinyanga wakiwemo wa Kelezia, Shenda, Katente na Mwabomba.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika jibu la sehemu (a), Serikali inawasaidia wachimbaji wadogo wa Kelezia, Shenda, Katente na Mwabomba. Hata hivyo, naomba kutoa wito kwa wachimbaji wadogo wa maeneo hayo ambao wanahitaji vitendea kazi kama vile jenereta, *compressor* na pampu za maji kuendelea kuunda vikundi rasmi vya ushirika na kuanzisha mifuko ya madini ili waweze kupata mikopo kutoka Kituo cha Biashara Adhimu ya Dhahabu (*Fair Trade Gold Centre*) kilichopo Ushirombo na taasisi zingine za fedha. Aidha, Wizara yangu kwa kutumia Maofisa Madini walioko katika Ofisi za Madini za Shinyanga na Kahama wataendelea kutoa elimu ya kuwaelimisha wachimbaji hao jinsi ya kujijengea utamaduni wa kujiwekea akiba.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.Kwa kuwa katika jibu lake ameeleza hawa Kampuni ya *Africa Precious Metals Ltd.* kwamba wanasaidia, ninachotaka kusema kwamba hiyo ni nadharia kwa vitengo hawajasaidia kukopesha wachimbaji kwa Wilaya ya Bukombe. Je, Waziri anasema nini?

Pili, kwa kuwa pamoja na maeneo niliyoyataja wachimbaji wadogo wadogo yapo maeneo mengine ya Nyakasaluma, Bukandwe na Nyakafuru na maeneo mengine katika Wilaya ya Bukombe yana matatizo mengi sana…

**NAIBU SPIKA:** Professa Mwalyosi unakatisha kati ya Spika na msemaji. Lakini ndelea.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naaomba nirudie swali langu la pili. Kwa kuwa pamoja na maeneo niliyoyataja wachimbaji wadogo wadogo katika Wilaya ya Bukombe yapo maeneo mengine ya Nyakasaluma, Bukandwe Nyakafuru na maeneo mengine wana shida sana ya vitendea kazi kwa ajili ya kupata dhahabu zilizoko chini. Je, Naibu Waziri anaweza akakubaliana na mimi kabla ya Bunge la bajeti aje katika Wilaya ya Bukombe ili tuweze kuyajadili kwa pamoja kwa sababu nimeona kuyaeleza hapa itachukua muda mrefu? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba *APM* kwa jimbo la Bukombe hawajaanza kukopesha. APM wameanza shughuli zao kuanzia jimbo la Geita huko Nyarugusu na Rwamgwasi ambako tuna taarifa kwamba wameanza kukopesha kidogo kidogo lakini ahadi waliyoweka ni kwamba watafika mpaka Bukombe na kuendelea kuwakopesha wachimbaji wadogo wadogo haswa kwenye maeneo haya ya pampu na *compressor* kwa kutambua kwamba wachimbaji wadogo wadogo wa maeneo ya Mheshimiwa Luhahula wanakabiliwa sana na matatizo kwamba kwenye machimbo yao maji ni mengi sana. Kwa hiyo kwa kuwa hawa *APM* waliweka

ahadi hiyo naomba nimuahidi Mheshimiwa Luhahula kwamba Wizara yangu itaendelea kufuatilia ahadi hii ya kuwakopesha hawa imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili la Mheshimiwa Luhahula naomba nikubali kwamba kuna haja ya kufanyia tathmini ya mahitaji ya vitendeakazi ya wachimbaji wadogo wadogo kama alivyowataja wa Nyakasulama, Bugandwe na kadhalika na hivyo naomba nichukue ahadi kwamba baada ya Bunge hili kabla ya Bunge la Bajeti Wizara yangu na kwa kuwa mwaliko nimepewa mimi basi ninaahidi kwamba nitafanya kila ninaloweza ili niende huko kabla ya Bunge la Bajeti.

Na. 118

**Uzalishaji wa Umeme Nchini**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Nchi yetu ina rasilimali nyingi ikiwa ni pamoja na mito isiyokauka kwa kipindi chote cha mwaka na mito yenye maporomoko makubwa; na kwa kuwa, kuna maeneo yenye upepo unaovuma kwa kasi kubwa kwa kipindi kirefu cha mwaka:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, huu ni wakati mzuri wa kuondokana na ukiritimba wa *TANESCO* kwa kuwaruhusu watu binafsi kuzalisha na kusambaza umeme kwenye maeneo yaliyo katika rasilimali hizo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzalisha umeme kutoka Mto Ruvuvu unaokatiza katika Wilaya ya Ngara na kuingia katika Mto Kagera kwa ajili ya umeme wa uhakika kwa Wilaya za Ngara, Biharamulo na Muleba?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu katika Mkutano wa Bunge wa Kumi na Moja unaoendelea, Serikali itawasilisha Muswada wa Sheria ya Umeme ambayo moja ya maudhui yake ni kutambua na kuweka mwongozo wa kisheria wa kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa njia shirikishi na sekta binafsi. Aidha, kama alivyotaka kufahamu Mheshimiwa Mwijage kwenye swali lake sheria mpya ya umeme itaainisha utaratibu utakaotumika kwa wawekezaji binafsi wa kuzalisha na kusambaza umeme kwa wananchi na hivyo kama alivyoshauri kuiondolea mzigo *TANESCO* wa kufikisha huduma hii kwenye maeneo ambako umeme haujafika bado.

(b) Ni kweli kuwa Mto Ruvuvu unaokatiza katika Wilaya ya Ngara na kuingia katika Mto Kagera una maji mengi yasiyokauka kwa mwaka mzima. Hata hivyo, uzalishaji wa umeme kwa kuutumia nguvu ya maji licha ya kutegemea utengamavu wa

hydrolojia hutegemea pia urefu wa maporomoko (*water head)* ya maji. Utafiti uliofanyika unaonesha kuwa hakuna maporomoko ya kutosha katika Mto Ruvuvu kuruhusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme kwa misingi iliyo endelevu (*sustainable*).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inafanya jitihada za dhati kwa kushirikiana na nchi jirani za Rwanda, Burundi chini ya Mradi wa *Nile Basin Initiative* kutekeleza mradi wa umeme utokanao na maporomoko ya maji ya Rusumo yaliyopo katika Mto Kagera.

Baada ya Mradi kukamilika, mradi huo wa Rusumo, utaweza kuzalisha megawati 60 ambapo kila nchi tumekadiria itapata megawati 20 kila mmoja. Umeme wa Rusumo utapelekwa na kusambazwa katika Wilaya za Ngara, Biharamulo, Muleba na Kibondo ambapo mahitaji ya umeme kwa miji ya Ngara, Biharamulo na Muleba kama tulivyosema ni jumla ya megawati 3 tu.

**MHE. SAVELINA J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana mimi nina swali moja la nyongeza kwanza ninasikitika anavyosema kwamba maporomoko yale ni madogo. Halafu kitu ambacho ni masikitiko tutaendelea kutumia umeme wa kuchangia mpaka lini? Sasa hivi tunatumia umeme wa Uganda kwanini sisi wenyewe tusiwe na umeme wa kujitegemea Serikali inampango gani na suala hili la kukaa na kutegemea umeme wa jirani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maporomoko ya maji yanayohitajika kuzalisha umeme yanapimwa kwa taratibu nyingi na vigezo vingi na kwa kusema kweli hata kama macho yanaonyesha kwamba maporomoko ni makubwa lakini wataalam wamebaini kwamba maporomoko ya pale hayatoshi kuzalisha umeme ambao ni endelevu.

Kwa hiyo, imeonekana kwamba tuna maporomoko ya Rusumo ambayo yanaweza kuzalisha megawati 60. sasa kwa sababu ni joint project ya nchi tatu na kwa kusema kweli si kitu kigeni na tutakapozalisha umeme pale sisi kama Tanzania tunatarajia kuwa na mgao wa megawati 20. Eneo lile peke yake halina mahitaji ya megawati zaidi ya nne. Kwa hiyo mimi naamini kwamba mradi huu utakapotekelezwa basi maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyazungumzia yatapatau umeme wa kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umeisha, tathmini ya leo ya ujibuji maswali. Kwa kiwango kikubwa kabisa napenda niwapongeze watu wote kwa sababu swali la kwanza tumetumia dakika nne, la pili nane, la tatu nane, la nne sita, la tano tano, la saba nne, la nane sita, la tisa nane, la kumi sita, la kumi na moja saba, la kumi na mbili tano, kumi na tatu nne, kumi na nne tano, na la kumi

na tano dakika tano. Halafu Mawaziri karibu wote wamejibu page moja kwa majibu yao. (*Makofi*)

Mtaona kwamba angalau kila swali limepata maswali ya nyongeza angalau mawili haya mengine kwa sababu ya nature bado kidogo uulizaji wa maswali ya nyongeza ni tatizo mnasema mengi. Lakini Mawaziri sasa wamefanya kazi nzuri na tuna kwenda zaidi. Sasa tutadai font ya aina moja maana wengine wana font ndogondogo inakuwa page moja kumbe ni mbili. Kwa hiyo tutakuwa na standard font ya kujibu maswali.

Kwa hiyo, itakuwa page moja *standard font.* Kwa hiyo, bado maswali ya nyongeza mnatoa hadithi halafu kama Waziri amejibu mnauliza swali la nyongeza linafanana na jibu la msingi. Kwa hiyo, nalo hilo mnapoteza wakati wa watu wengi kuchangia. Kwa hiyo, *font* zitakuwa za aina moja Wabunge Maswali ya nyongeza yawe mafupi. Kwa hiyo, kwa ujumla naomba niwapongeze haitupi taabu sisi kuongoza kikao kwa maana hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa wageni. Tunao wageni kama ifuatavyo:-

Tunaye Ndugu D. Smith, *if you can stand up please,* yeye huyu Wabunge wa zamani wengi mtamfahamu. Miaka mitano iliyopita tulikuwa na mradi uliokuwa unaitwa *State University of New York* ambao ulikuwa ni mradi wa kuimarisha Bunge.

Mradi huu ulimalizika nafikiri mwaka huu mwanzoni. Sasa tumeingia kwenye mradi mwingine na *British Council* kuhusu hiyo hiyo kuimarisha mambo ya Bunge na yeye huyo ndiyo *Senior Consultant* wa mradi huo na tutakuwa naye kwa kipindi kirefu. Tunamfahamu kwa sababu kazi hii ameweza kufanya kwenye Bunge la Uganda na Mabunge mengine na Tanzania pia. Kwa hiyo, Wabunge wengi hamjafaidika lakini lengo letu ni hilo. Kwa hiyo, amekuja kuripoti nadhani kazi itaanza mapema. *Welcome and we are happy to see you*. (*Makofi*)

Jana nilitangaza kwamba kuna Mabalozi wetu wale Balozi wa Umoja wa Ulaya Mheshimiwa Tim Clerk amefuatana na Afisa wake Theo Cassipias, *please if you can sit.* Hawa pia tunao mradi mwingine wa *deepening democracy* ambao unafanyika kwa ushirikiano na Jumuiya ya nchi za Ulaya, pamoja na *UNDP* ambao pia unaangalia maeneo mbalimbali ya kuimarisha Bunge letu tukianzia na uwezeshaji wa Wabunge wenyewe *staff* yetu na pia nyenzo za kufanyia kazi. Tutashirikiana nao katika Mpango Mkakati ambao Bunge letu linaandaa tunafanya kazi pamoja. Wako na Mabalozi wengine jana niliwatangaza lakini kusudio lao ni hilo.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, Mbwana Haji Mbwana, aliwahi kuwa Mbunge zamani wa Micheweni, karibu sana. Halafu tuna mgeni wa Mheshimiwa Marombwa, Mheshimiwa Luteni Kanali Msumba kutoka Morogoro. Halafu tuna wakufunzi na wanafunzi wa *VETA* kanda ya kati naomba msimame. Karibuni sana. Tunao bado wanafunzi wa Tumaini ambao baadaye saa saba watakutana na Wabunge wa

Iringa katika Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, wapo wanafunzi kutoka Iringa, *Tumaini University.* Lakini watakutana na Wabunge wa Iringa saa saba katika Ukumbi wa Msekwa, karibuni sana.

Sasa nina wale wageni ambao nimeletewa vikaratasi ingawa nimekataa hivyo, kuanzia wiki ijayo vikaratasi vya wageni namna hii tutakuwa hatuvisomi. Tuna wageni wa Mheshimiwa Fuya Kimbita , ambapo ni mke wake Monica Fuya na watoto. Watoto ni Godwin na Gideon. Halafu tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Kimbita hao wanatoka Taasisi inaitwa *Global Action* ya Marekani yupo Miss Michelle Linden ndiyo Afisa Mtendaji, *can you please stand up*. Tunaye Dr. Mayunga ndiyo *Country Director.* Halafu tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mnyaa, ambaye ni mkewe Mrs Mnyaa Bi. Fatma, karibu sana. Kuna habari nyingine sitapenda kuitangaza hapa.

Matangazo ya kazi, kwanza kabisa Waheshimiwa Wabunge napenda kuwatangazia kwamba katika kikao ambacho Mheshimiwa Spika amehudhuriwa sasa hivi napenda kuwatangazieni kwamba katika kikao ambacho Mheshimiwa Spika anahudhuria sasa hivi huko *Cape Town* wenzetu wafuatao wamepata vyeo huko.

Kikao anachohudhuria Mheshimiwa Spika kinaitwa *Inter Parliamentary Union (IPU)* hii ni jumla ya Mabunge yote katika dunia huwa kuna Bunge moja linaitwa *IPU.* Katika Bunge hilo Mheshimiwa Kilonsti Mporogomyi, amechaguliwa kuwa Makamu Rais wa Kamati ya Fedha na Biashara yaani *Trade and Finance* ya *IPU.* Halafu na Mheshimiwa Susan Lyimo, amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji *Coordinating Committee* ya Wabunge wanawake kundi la Afrika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wenzetu wawili wamefanya vizuri na sisi tunapenda watu wakienda kuhudhuria Mikutano waje na vitu sio wanakwenda kuwa wasindikizaji. Tunawapongeza sana.

Nimeshatangaza Mkutano wa Wabunge wa Mkoa wa Iringa saa saba katika Ukumbi wa Msekwa. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Kwangw’ anaomba Wajumbe wake wakutane leo mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika chumba 428 kutakuwa na Mkutano huko. Halafu tuna Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Wilson Masilingi, anaomba Wajumbe wake wakutane saa sita na nusu katika Chumba namba 231.

Sasa kuna tangazo la uchaguzi Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba baada ya Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko ya Baraza lake la Mawaziri watu wengine walibahatika kuteuliwa kuwa Mawaziri au Manaibu Waziri kwa hiyo kusababisha mapendo katika nafasi walizokuwa wanasimamia moja ni ile ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Dr. James Wanyacha, alikuwa ndiyo Mjumbe Kwa hiyo, nafasi hiyo iko wazi matangazo yapo pale kwenye ubao mpaka sasa wamechukua fomu wawili bado muda wa kuchukua fomu ziko pale.

Lakini pia tuna nafasi ya Chuo cha Ufundi Arusha hii hakuna aliyechukua fomu. Kwa hiyo, mnaarifiwa kwenda kuchukua fomu. Hili Bunge la Afrika tuna nafasi mbili wazi kwa sababu Mheshimiwa Kabuye yeye alikuwa ndiyo Mbunge wa Bunge lile hata kama hahuzurii vikao vile lakini utakumbuka kwamba yeye aliondolewa kwa mujibu wa mahakama Kuu kama matokeo ya uchaguzi wake yalibatilishwa.

Lakini kwa sababu amekata rufaa kwenye Mahakama ya Juu zaidi hatuwezi kusema hapa lipo wazi. Kwa hiyo, nafasi hii hatuchagui bado. Kwa hiyo Waheshimiwa mkachukue fomu za kugombea nafasi hizo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na kazi ya leo. Katibu endelea na *Order Paper.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana wazungumzaji wote walikwisha sasa naomba mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi katika mambo yaliyoulizwa na kuchangiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kwa maazimio na itifaki nilizoziwasilisha jana hapa Bungeni. Kwa heshima kubwa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hoja hizo kwa kusema nao ni wanane.

Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalamo kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Herbert James Mntangi Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Juma Njwayo Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Godfrey Zambi Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela na Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Savelina Mwijage Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Basili Mramba Mbunge wa Rombo na leo hii asubuhi nimeupata wa Mheshimiwa Daina Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kusaidia kujibu hoja na kutoa ufafanuzi kidogo kwa hoja mbalimbali zilizotolewa. Wabunge wote waliochangia wameunga mkono hoja zote kwani wameona zina umuhimu kwa uchumi wa nchi yetu naomba niwashukuru sana. Mawazo yao yote ni mazuri yatazingatiwa kwani yanalengo ya kuboresha masuala ya uchukuzi katika nchi yetu. Sasa niseme Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mohamed Sinani na Mheshimiwa Mzindakaya walitoa hoja ambazo zinafanana. Mpango wa Serikali wa kuboresha huduma za Bandari na pia kuondoa msongamano Bandari ya Dar es Salaam. Niseme Serikali imeruhusu kampuni binafsi kuanzisha *ICD* hadi sasa zipo Kampuni sita ambazo zinapokea makontena moja kwa

moja na kampuni nyingine zaidi zitaruhusiwa. *Tanzania Road Haulage , AMI, MOFET, Malawi Cargo Centre, Ubungo Container Depot*, na *Dar es Salaam International Terminal*. Bandari kuongezewa maeneo mengine kuhifadhi kontena ndani ya Bandari litazingatiwa. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imenunua eneo la hekta 19.5 Kurasini kwa ajili ya kupanua Bandari ya Dar es Salaa. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ipo katika mchakato wa kujenga gati nyingine mbili za kuhudumia makontena ndani ya eneo la Bandari ambazo tunategemea kama mambo yatakwenda vizuri ujenzi wake utaanza mwakani.

Lakini napenda nisisitize jamani, wenzetu tumeshawasisitiza wa Bandari wafanye juhudi kwa kushirikiana na Sekta nyingine ambazo zinatumia Bandari kuona umuhimu wa matumizi ya Bandari. Wenzetu wa Singapole wanaishi kwa ajili ya Bandari ni kwanini na sisi tusifanye hivyo. Mheshimiwa Ludovick Mwananzila kwa niaba ya Mwanyekiti alitoa rai kuwa *TCAA* na *TAA* wasimamie usalama na wawe na wataalam wa kutosha aidha wahamasishe watoa huduma. Ushauri huu ni mzuri tunauchukua kwa utekelezaji. Vile vile Mheshimiwa Abubakary Shamis Faki yeye ametoa hoja kwamba je, wawekezaji wa nje wataruhusiwa kununua au kukopa vifaa vya ndege baada ya Tanzania kuridhia Mkataba na Itifaki ya Vifaa vya Ndege? Tunasema ndiyo, kampuni yoyote itaruhusiwa kukopa iwe ya umma au binafsi ili mradi kampuni iwe imesajiliwa nchini na makao makuu ya kampuni yawe nchini. Je, Itifaki ya Mkataba ipi ina nguvu pale ambapo tafsiri inatofautiana. Kwa mujibu wa Mkataba huu itifaki ina nguvu zaidi ya mkataba pale ambapo patatokea mkanganyiko katika tafsiri. Kuridhiwa kwa mkataba na itifaki kwa jumuiya za kikanda. Mkataba na Itifaki kwa jumuiya za kikanda. Mkataba na Itifaki kwa jumuiya za kikanda. Mkataba na Itifaki inataka nchi wanachama wa *ICAO* ziridhie nchi tatu kwa mkataba na nchi nane kwa Itifaki ili zianze kutekelezwa. Uchaguzi wa Mahakama alizungumzia pia Mheshimiwa Faki; tunasema Mkataba na Itifaki zinatoa fursa kwa mkopaji na Mkopeshaji kuchagua mahakama pale watakaposhindwa kuelewana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliuliza tena nini dhana ya Serikali kusaini Mkataba huu ikiwa kifaa chenyewe kinachokopeshwa ni dhamana? Kwa kuridhia Mkataba huu Serikali haitoa dhamana isipokuwa ipo kutoa ushirikiano endapo mkopaji atashindwa kutekeleza masharti waliyokubaliana wakati wa kukopa. Aidha Serikali itakuwa tayari kulinda maslahi ya pande zote mbili endapo mmoja atashindwa kutekeleza masharti ya mkopo. Pia Mheshimiwa Faki, alisema ni jinsi gani chuo chetu cha *DMI* kinanufaika na ushirikiano chini ya Mkataba huu wa *ICOS*. Chuo cha Mabaharia ndiyo chuo rasmi cha wataalam cha waendeshaji wa shughuli za bahari kwa Afrika Mashariki na kinatambuliwa na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Usafiri wa Majini Duniani. Serikali kupitia Chuo hiki imeandelea kuboresha mitaala ya ufundishaji katika chuo hicho ili kikidhi mahitaji ya wanaafrika mashariki na wanayo nia sasa ya kuanzisha digrii programu pale kwenye Chuo hiki. *DMI* inapokea wanafunzi wa kutosha kila mwaka kutoka Kenya Uganda na Tanzania na nchi nyingine na hivyo kuipatia nchi mapato yatokanayo na ada ya mafunzo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Zambi alizungumzia suala la usalama wa usafiri majini uimarishwe na *SUMATRA* ipewe nyenzo na nguvu kudhibiti vyombo vinavyokiuka Sheria na

kuhatarisha usalama. Hilo ni wazo zuri na tunalizingatia tayari *SUMATRA* imeshachukua hatua za awali ya kufunga mitambo ya mawasiliano ili kuboresha mawasiliano ya vyombo vya majini kwenye bahari, Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa ili kurahisisha uratibu wa ufuatiliaji wa safari za meli. Tunao mnara pale Magogoni, ukamilishaji wa mnara huo wa mawasiliano kwa ajili ya uokoaji na utafutaji pamoja na miendo ya meli katika Bahati ya Hindi unazidi kukamilishwa na tunategemea mnara huu utakamilika mwanzoni mwa mwezi ujao. Hata hivyo uimarishaji na ukaguzi na udhibiti wa vyombo vya usafiri majini unafanywa na *SUMATRA* ili vyombo hivyo vikidhi matakwa ya Sheria ya Usalama. *SUMATRA* inahamasisha wawekezaji wa nje na ndani kununua vyombo vipya na bora zaidi ili kutoa huduma bora zaidi ili kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na tayari mazungumzo yameanza kwa kushirikiana na *TIC* ili kuishawishi Serikali kuwekeza na kuweka vivutio maalum kwa ajili ya wawekezaji kwenye vyombo vya majini. Kuhusu uimarishaji wa usalama kwenye maji na bandari Tanzania hasa kudhibiti vitendo vya uharamia, Tanzania kwa kushirikiana na *IMO* imekuwa na Mikutano ya Kimataifa kuhusu kudhibiti uharamia huo baharini ukanda wa *Indian Ocean.* Tarehe 14 – 18 Mwezi huu na kama mchakato wa kuwa na mkataba wa ushirikiano katika ukanda huu suala hili pia alizungumzia Mheshimiwa Sinani tunalipa uzito unaofaa.

Kulikuwa na suala la Mkataba na Itifaki iliyoridhiwa itatumika pia kwa ununuzi wa vyombo vingine vya uchukuzi? Tunasema Mkataba utakaotumika kwa ajili ya manunuzi ya vyombo vya uchukuzi ni huu ambao unaridhiwa sasa hivi. Hata hivyo itifaki inayoridhiwa sasa inahusu vyombo vya usafiri wa anga tu. Lakini hapo baadae tukikuleteeni kwa vyombo vingine tutakuombeni muipitishe ili na kwenye vyombo vingine waweze kunufaika. Mkataba unatoa fursa kwa itifaki nyingine kuanzishwa zikiwemo itifaki za ununuzi wa vyombo vya usafiri wa reli, majini, vifaa vya kilimo na mitambo ya kuchimbia madini.

Mheshimiwa Mwijage yeye alitoa maoni yake mbalimbali kuhusu usafiri wa majini hasa Ziwa Victoria Bukoba kwenda Mwanza au Mwanza kwenda Bukoba. Ni kweli kuna uhaba wa vyombo vya usafiri majini kati ya Mwanza na Bukoba hasa baada ya *MV Bukoba* kuzama na pia kutokana na kuharibika kwa *MV Victoria* kutokana na umri wake kuwa mkubwa.

Lakini Meli hii imefanyiwa matengenezo makubwa ikiwa ni pamoja ya injini zake zote pamoja na ukarabati wa Meli yote kwa ujumla. Lakini baada ya matengenezo kufanyika na ikaanza majaribio yalijitokeza matatizo mengine ya *gear box* kwa hivyo imebidi meli hii tuisimamishe kidogo ili tuangalie masuala ya *gear box. MV Victoria* inaendelea kutengenezwa pale itakapohitajika ili kuhakikisha wananchi wanapata usafiri kati ya Mwanza na Bukoba na pale ambapo MV. Victoria itakuwa matengenezoni basi MV Serengeti itaendelea kutoa huduma hiyo. Ulizungumzia juu ya Boti mbili ziendazo kazi zilikuwa zinatoa huduma kati ya Mwanza na Bukoba tumezisimamisha baada ya kubainika kuwa sio salama kwa ajili ya kutoa huduma na Mkaguzi wa Serikali ameelekeza mapungufu yaliyopo yarekebishwe ambayo ikikamilika *SUMATRA* itaikagua na itaruhusu tena kutoa huduma hizo. Namwomba Mheshimiwa awe na uvumilivu

kidogo. Mheshimiwa Sinani alizungumzia kuhusu Bandari ya Mtwara kutotumika ipasavyo na wangine vilevile walizungumzia suala hili. Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu itawasiliana na Asasi zote zinazohusika na utoaji huduma katika Bandari si ya Mtwara tu bali pia na zingine kwa lengo la kuhakikisha kuwa Bandari zote zinatumika ipasavyo ili kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipata nafasi ya kubadilishana mawazo na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwamba sisi Bandari tuko tayari tuitumie Bandari ya Mtwara, basi tuombe na wenzetu wa Fedha watupe msukumo ili suala hili liweze kufanikishwa. Hapa nitapenda nitoe indhari kidogo kwamba ni vyema basi tujiridhishe kwamba vile vyombo vidogo vidogo ambavyo vitaondosha makontena kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam basi viwepo. Isije ikawa tena tunaondosha tatizo kutoka Dar es Salaam na kulihamishia Mtwara.

Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo yeye alisema Reli iliyong'olewa kusini mwa Tanzania irudishwe. Ni kweli nafikiri siku zile maamuzi yaliyofanyika yalifanyika kutokana na wakati ule. Lakini wakati huu reli hii tunaihitaji sana na ndiyo maana Serikali kupitia Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara ambao unashirikisha Tanzania Msumbiji Zambia na Malawi unatoa kipaumbele ujenzi wa mindombinu ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Reli kutoka Bandari ya Mtwara kwenda kwenye maeneo ya kiuchumi kama vile mgodi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na juhudi hizi zinaoana na malengo ya mpango kabambe wa uchukuwa ambao nao pia una malengo ya kujenga reli hiyo lakini katika kipindi cha muda mrefu.

Mheshimiwa Bakari Shamis alizungumzia kwamba Serikali iagize vivuko kupitia mkataba na itifaki inayohusu vifaa vihamishikavo ili kuimarisha usafiri. Tunakubaliana na wazo lake lakini kwa sasa kama nilivyosema Mkataba huu na itifaki iliyopo inayoanzisha kutekeleza ni vifaa vya usafiri wa anga ambayo imeanza kutekelezwa tangu mwaka 2006. Mkataba na Itifaki, vinatoa fursa kwa itifaki za usafiriwa majini, usafiri wa reli na itifaki za vifaa vya kilimo na mitambo ya kuchimba madini kuanzishwa na *ICAO* na ikafanya kazi. Ununuzi au uagizaji wa vivuko au injini zake utawezekana baada ya itifaki ya usafiri wa majini kuanzishwa na kuridhiwa. Lakini Wizara ya Miundombinu kwa kupitia TEMESA wataendelea kushughulikia masuala ya vivuko hapa nchini.

Mheshimiwa Mramba yeye alisema anaunga mkono hoja ametaka Serikali iimarishe miundombinu ya reli, bandari na barabara na matumizi ya *Faiber Optic* na aidha Serikali itumie bandari za Tanga na Mtwara kujenga bandari mpya Bagamoyo na kurahisha maamuzi. Sisi tunasema Mheshimiwa Mramba tunakubaliana naye kwa sababu alikuwa ni mwenzetu katika Sekta hii ya miundombinu tumepanga wote mambo yetu mengi haya mazuri kwa hivyo tutayazingatia hasa uimarishaji wa miundombinu pale ambapo bajeti itaruhusu. Aidha tutaendelea kuishawishi sekta binafsi ili ishirikiane na Serikali katika kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya yeye alisema Mwekezaji katika Reli ya Kati ameonyesha nia ya kufunga huduma za Reli ya kutoka Manyoni – Singida na Mpanda – Kaliua. Lakini tuwaridhishe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba

kulingana na Mkataba wa ukodishaji Mwekezaji amepewa jukumu la kutoa huduma na suala la uendelezaji wa miundombinu ya reli ni jukumu la Serikali. Hata hivyo suala la kusitisha huduma katika njia nilizozitaja halijaletwa rasmi Serikalini na kimsingi Serikali haitakubaliana na hatua ya kufunga huduma katika eneo haya. Kwa sababu tokea mapema tulisema reli hizi mbili Manyoni – Singida na Mpanda –Kaliua hazina faida kibiashara, tunatoa *service* na ni jukumu la Serikali kufanya *sevrice* kwa maeneo haya mawili.

## HOJA ZA SERIKALI

## M A A Z I M I O

*(Majadiliano yanaendelea)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Ni kweli fedha nyingi sana zinapotea kupitia uzembe wa Halmashauri za Wilaya wa kukusanya mapato. Ninakubaliana na Muswada huu kwamba, *TRA* wakusanye mapato haya. Hata hivyo, ninaomba nichangie yafuatayo:-

Kwanza, ninashauri kuwa Halmashauri ya Wilaya na *TRA,* hizi zote ni Serikali, ziwe na mahusiano mazuri ili waweze kufanya kazi kwa ushirikiano. Pili, maeneo mengi Bukombe hayana hati miliki za viwanja na nyumba zao; je, Serikali itawezaje kukusanya mapato wakati wananchi wake hawana miliki?

Tatu, ninashauri kila Halmashauri ifanye tathmini kujua ni majengo mangapi yaliyopo ndani ya eneo ili kujua mapato katika eneo husika. Vilevile Serikali izijengee uwezo Halmashauri, kwani kuendelea kutunga sheria za kuwaongezea majukumu *TRA,* tunaonyesha jinsi gani Halmashauri zisivyojua kukusanya mapato. Tunaiomba Serikali itoe Tamko la kuzitambua kisheria baiskeli na pikipiki. Usafiri huu ni siasa ndani ya Wilaya ya Bukombe na Kanda ya Ziwa kwa ujumla, waendesha baiskeli kama hatuwalindi kisheria; kwa nini tunawashirikisha katika kuchangia shughuli za maendeleo kama vile wafanyabiashara?

Ninaishauri Seriali iangalie uwezekano wa kukusanya mapato kupitia wanunuzi wa pamba. Halmashauri zinaonekana uwezo wao wa kukusanya fedha hizi toka makampuni ni mdogo sana, mapato mengi yanapotea. Hata hivyo, wanasheria kwenye Halmashauri zetu, uwezo wao wa kusimamia kesi ni mdogo.Ninaunga mkono hoja.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuanza kwa kuunga mkono hoja hii, kwa sababu Muswada huu umelenga moja kwa moja katika kuongeza uwezo wa Halmashauri zetu, kukusanya kodi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, *TRA* watatoa utaalamu wao kwa Watendaji wa Halmashauri tatu zilizoteuliwa katika *Pilot Project,* ninaishauri Serikali iwaelekeze *TRA* kutoa mafunzo ya nadharia ya mbinu za ukusanyaji kodi kwa Halmashauri nyingine zilizotengwa kuingizwa katika utaratibu huu, sambamba na utekelezaji wa *Pilot Project* katika Wilaya tatu zilizoteuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la ushauri huu ni kufupisha muda wa utekelezaji wa mafunzo kwa vitendo vya ukusanyaji wa kodi za majengo katika Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Serikali iielekeze *TRA* kuwasaidia Halmashauri kutambua *man power* halisi na vitendea kazi muhimu vinavyotakiwa wawe navyo ili ziweze kumudu kukusanya kodi za majengo hasa ukizingatia ukubwa na kusambaa kwa majengo katika Wilaya husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ninaamini *TRA* watafanikisha zoezi na malengo ya Muswada huu, ninaishauri ielekezwe kuchunguza maeneo mengine yanayotozwa kodi kubwa au zenye *potential* ya kukusanya kodi nyingi katika Halmashauri ambazo ingefaa pia wasaidie kuwapa au kuwafundisha mbinu za kuongeza makusanyo ya kodi husika. Lengo ni kuongeza mapato ya Halmashauri .

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uadilifu na uaminifu *(Friendly Approach)* ni lazima litiliwe mkazo maalum kwa wakusanyaji kodi ili wateja au walipa kodi, wasijione wanakarahishwa au kunyanyaswa wanapofuatwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi kwa Wizara ya Fedha kwa kuandaa Muswada huu, yapo mambo ya kuzingatia ili Halmashauri ziweze kupata mapato ya kutosha kuweza kuendesha shughuli za Halmashauri: Kuhakikisha kodi zinakusanywa kwa wakati; kuwabana wakorofi ambao hawataki kulipa kodi; kuhakikisha Halmashauri zinapata fedha hizo kwa wakati; kwa Sheria hii ni kwamba Halmashauri zifaidike sana kuliko awali; kuzuia mianya ya rushwa; kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi; na kuwe na utaratibu mzuri wa kulipa na sio kukaa foleni kutwa nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri za Dar es Salaam zinategemea sana kodi hii ya majengo ni vyema zikashirikishwa kwa karibu sana ili kuleta ufanisi na kuondoa dhana ya kuwa zimenyang'anywa chanzo chao cha mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Dar es Salaam Bajaji zilipe kodi lakini zisiingie mjini kubeba abiria, waendelee kufanya biashara zao huko huko kando kando ya Mji; Mwenge, Kunduchi, Kimara na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuchangia hoja katika maeneo mawili. Kabla sijachangia, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Ninaomba Serikali iwe makini kuhakikisha kwamba, *TRA* inafanya wajibu wake ipasavyo ili yale malengo ya marekebisho ya sheria hii yafikiwe ili tusije tukafundua tandu tukafundika nge, yaani tukarudia makosa yale yale.

Ninaomba niseme kwamba, kodi hizi au mapato ambayo yanatokana na jasho la wananchi ambao ni matarajio yao kwamba Halmashauri zitatumia mapato hayo ili kupunguza baadhi ya kero za wananchi, jambo ambalo litasaidia zaidi kuboresha maendeleo. Hivyo, *TRA* wafanye kweli na sio kukusanya kwa ajili ya kuwaibia walipa kodi badala ya kufaidika.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, kwa mambo yafuatayo:-

- Kwa kuwa Halmashauri nyingi hapa nchini zinajumuisha maeneo ya vijiji; je, wanananchi wa maeneo hayo (vijijini) watalazimika na wao kuchangia kodi ya majengo yao na kodi hiyo itafanana na wale wa mijini?

- Kwa kuwa hivi sasa Halmashauri imeanzisha utaratibu wa kuwapa wananchi waliojenga kwenye maeneo yasiyopimwa, leseni za makazi ya miaka miwili tu; sasa Serikali haioni kuwa itakuwa ni vyema muda huo ukaongezwa na kuwa wa angalau miaka 20 ili kurahisishia Halmashauri kupata mapato mengi ya majengo hayo ambayo yatakuwa yamethaminiwa *(evaluated)* kuliko ilivyo hivi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zisibweteke kwa kutegemea *TRA,* ni vyema wakashirikishwa katika kutayarisha mikakati na hata ukusanyaji wa kodi za majengo, ikiwa pamoja na kuwapatia mafunzo ya ukodishaji wa majengo ili kodi itakayolipwa na mwananchi, ilingane na thamani ya jengo hilo. Aidha, Wizara ichukue tahadhari kwa *TRA* kuwalipisha kodi kubwa ya majengo wananchi, isiyolingana na thamani halisi ya majengo yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba, Muswada huu una lengo kuu la kuzisaidia Halmashauri kupata makusanyo ya kodi, ambazo kwayo Halmashauri zenyewe zimeshindwa kuzikusanya. Muswada huu ni muhimu na mzuri, niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami ningependa kutoa ushauri ufuatao:-

Serikali kupitia *TRA* ni lazima wawe makini katika kufuatilia utendaji wa watendaji ambao watakuwa wanafanya uthamini wa majengo, kwani hapa kama hatutakuwa makini, tunaweza kuzalisha mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima sasa Serikali iandae utaratibu ulio mzuri, ambao hautakuwa na usumbufu kwa walipa kodi na hasa katika matumizi ya huduma za kibenki. La msingi zaidi ni kuhakikisha kwamba, kodi itakayokusanywa inarudi kwa wananchi katika kuwajengea miundombinu ya barabara, maji safi na majitaka, umeme, simu na kadhalika. Tukiweza kuhakiksha hayo yanatendeka, hapana shaka wananchi watakuwa tayari kulipa kodi hiyo.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia kwa maandishi na ninatoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Sheria hii iangalie kwa macho ya huruma, kodi zinazototozwa Wastaafu. Watumishi wa Serikali hawa wamedunduliza pesa kutoka kwenye mishahara yao midogo na ambayo ilikuwa inatozwa kodi kubwa. Sasa anapojenga nyumba yake ya kudumu; *TRA* na TAMISEMI tena kumtoza *Property Tax,* ninaona kama hii ni *double tax action*. Sheria hii pia imlinde.

Sheria hii iangalie kodi ya kumtoza mjane, yatima na walemavu wenye kumiliki majengo haya ya kutozwa kodi. Nina hakina pengine imegusia, kwa kuwa *Section 31 A(1)* inasema, *TRA shall assess, collect and account …* Ninaomba *assessment* hiyo pia iruhusu makundi makubwa niliyoyataja, yaani wajane, yatima na kadhalika.

Kifungu cha 31(A)(2) kinaweka *demarcation* ya *Geographical area ya* kutoza kodi ya majengo. Lakini kuna watu wenye uwezo na wamejenga *structures* za gharama kubwa kule vijijini *(interior villages),* ambako hii *geographical demarcation* haifiki. Pengine Sheria hii pia iangalie ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, *property* nyingine iko *acquired* kwa kutumia mikopo ambayo itakuwa imetozwa riba kubwa. Sasa je, kwa kutumia hii Sheria, Serikali haioni kuwa inawatoza watu hawa kodi mara mbili? Pengine ni vizuri Sheria ikaangalia eneo hili la *structures* za mikopo ya benki.

Kifungu cha 3(b) kinachooanisha aina ya watu watakaosamehewa "*…women who are completely dependent on their husbands or other persons for their livelihoods*." Hapa ninashauri iandikwe "*… and vice versa.*" Hii ni kwa sababu kuna wanaume pia wanaotegemea wake zao kwa kuishi, hata kama siyo *culture* ya Kiafrika, lakini hii ni sheria na hata kama sasa hivi hawapo watu wa namna hii, lakini *with time* watakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ndiyo mchango wangu mdogo, ninaomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kuleta Muswada huu muhimu kwa maendeleo ya nchi kupitia Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi, ninaomba yafuatayo yazingatiwe: Halmashauri zote nchini na hasa za Mkoa wa Dar es Salaam, ziwe na takwimu sahihi *(database)* za majengo yote yaliyoko katika kila Halmashauri husika ili kuwepo na mipango halisi kuliko ilivyo hivi sasa, ambapo uwezo wa Watendaji katika fani ya ukusanji wa mapato na uthamini wa majengo ni mdogo. Kuwe na ukaguzi wa mara kwa mara ili kuweza kuthamini majengo makubwa yanayojengwa kila siku hasa katikati ya Jiji la Dar es Salaam.

Marejesho ya mapato hayo yarejeshwe kwa wakati kwa Halmashauri husika ili Halmashauri ziweze kutoa huduma kwa wananchi kadri Ilani ya CCM ya 2005 inavyosema.

*TRA* ipewe eneo la kodi za mabango yote yaliyoko katika Mkoa wa Dar es Salaam ili waweke mfumo mzuri wa ukusanyaji kodi hizo, ambapo ni eneo muhimu na chanzo kikubwa cha mapato katika Halmashauri.

Vilevile Serikali iangalie uwezekano wa vyanzo vingine vya mapato kwa mfano, matangazo ya biashara yanayotangazwa kupitia kwenye televisheni, japo kwa asilimia ndogo kwa kila tangazo (Kampuni inayotangaza bidhaa husika ndiyo ichangie kodi hiyo).

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia 100.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unafaa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu hili ni vyema kukabidhiwa *TRA* na pia elimu zaidi itolewa kwa walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sheria ya faini, ninapendekeza tutumie maneno yasemayo “si chini ya asilimia ishirini” badala ya “isiyozidi kiasi fulani.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi zikusanywe kwa faida ya walipa kodi, badala ya kuwanufaisha wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ina vyanzo vingi vya mapato, lakini mbinu nzuri ya ukusanyaji wa mapato hayo hazijatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isitunge Sheria itakayowabana wananchi wa hapa Tanzania tu, bali iwabane mpaka wale wageni wanaomiliki hayo majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote, ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu, makusanyo ya *property tax* yamekuwa yakilegalega. Halmashauri zimekuwa hazifahamu majengo yote ambayo yalipaswa kulipa kodi hii na kwa kiasi gani.

Pili, Halmashauri nyingi hazina wataalam wa kutosha kufanya kazi hiyo na nyingine hazina kabisa wataalam hao. Ninashauri Halmashauri zianze mchakato wa kusomesha wataalam wake wa kufanya kazi hizo. Misamaha ichujwe vizuri. Ninashauri majengo yote ya Serikali na Mashirika ya Umma yalipe kodi ya majengo isipokuwa nyumba za Ibada na Hospitali tu. Serikali kama inavyolipa *VAT,* basi ilipe pia Kodi ya Majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri pia Halmashauri itumie fedha hizo kuboresha huduma kwa maeneo yaliyopo majengo hayo kama vile ukusanyaji wa taka.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninamshukuru Mungu, kwa kunijalia leo kuweza kuchangia Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kutoa pole kwa wale wote waliopoteza jamaa zao Mererani na majeruhi wote Mungu awaponeshe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza sasa kutoa mchango wangu. Ninaunga mkono kuwa kodi zote za majengo zikusanywe na *TRA*. Sababu kubwa ni kuwapunguzia mzigo Halmashauri zetu na kuwaondolea malalamiko kuwa pesa zinaliwa au zinatumika vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kodi za majengo ziangaliwe, kwa sababu kuna nyumba za ghorofa na nyumba za kawaida, kwa vile wengine nyumba zao ni ndogo na uwezo wao ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii, ila ninaomba maneo yafuatayo yafanyiwe marekebisho: *Hotel Levy* ya asilimia 20 ni kubwa mno, hailipiki na imeleta migogoro sana kwenyeHalmashauri na wafanyabiashara wa hoteli. Hili ni tatizo ambalo linawaumiza wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Road Licence Fee* ziko juu sana, hasa kwenye magari madogo; liangaliwe upya. Gari kubwa linalipa kidogo sana ila gari dogo ni mateso. Ninashauri suala hili liangaliwe upya.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu sana. Mapato ya Halmashauri kutokana na Kodi; katika Mji wa Moshi Kampuni ya *Vodacom* imekuwa ikipiga rangi za *blue* mji mzima; kwenye maofisi, mabaa na

makazi ya watu; ni kwa jinsi gani Halmashauri hizi zinapata kodi kutoka kwa *Vodacom* kujitangaza au wanajitangaza bure?

Pamoja na Halmashauri kujaribu kukusanya kodi kwa *parking* za magari *especially,* Dar es Salaam kuna magari mabovu yanayochukua magari hayo. Panahitajika kuwepo na wasimamizi wa kuhakikisha kodi hizi zinapelekwa Halmashauri. Kuhusu pikipiki za tani tatu *(Bajaj),* hii itakuwa ni njia nzuri ya kupata mapato mengi, ukiangalia zipo *Bajaj* nyingi sana; zikisimamiwa vizuri Halmashauri zitapata kodi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji wa kodi za majengo; ni vizuri Halmashauri zikakusanya zenyewe badala ya kutumia wakala. Halmashauri zimekuwa zikitumia wakala kukusanya kodi na wakala hawa huwa wanaongeza kodi hiyo.

Mwisho, wananchi wajulishwe katika *Full Council* ni kiasi gani cha kodi kinakusanywa na zitafanya shughuli gani katika Halmashauri husika.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya II *(i) TRA to collect rates in LGA*. Sheria ni nzuri sana naipongeza Wizara kuileta Bungeni leo kwani itaongeza ufanisi wa makusanyo ya kodi husika.

Je, Serikaloi ina mkakati gani wa kusaidia maeneo mengine ambapo Halmashauri zinaonekana kushindwa kabisa kukusanya baadhi ya kodi?

Kwa kuwa TRA atafanya kazi ya kukusanya kodi ya mali zisizohamishika kwa niaba ya Serikali za mitaa. Je, kutakuwa na malipo yoyote kama yapo itakuwa asilimia ngapi ya mapato?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu V. Sheria mpya inatambua kisheria pikipiki za magurudumu matatu kusafirisha abiria kibiashara. Kwa kuwa pikipiki za magurudumu mawili pamoja na baiskeli zinatumika kusafirisha abiria na kwamba ni msaada sana kwa wananchi hasa vijijini mfano kuwahi matibabu na shughuli zingine za kiuchumi.

Je, Serikali inasema nini kuleta Muswada wa kuzipa nguvu kisheria vyombo hivi vya usafiri ili wananchi wanufaike zaidi vijijini ambako hakuna magari kikiwemo kituo cha daladala za baiskeli Mwandoya na sehemu zingine.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninaipongeza Wizara hii kwa kuwasilisha Muswada huu, pamoja na kazi zao nzuri chini ya usimamizi wa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara. Ninawaomba Wabunge wenzangu, tuupitishe Muswada huu wa Sheria kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Naibu Spka, kodi za mapato zisimamiwe vizuri zisiende kiholela. *TRA* na Halmashauri za Serikali za Mitaa, zisimamie vyema ukusanya wa kodi za majumba kwa faida ya nchi, isiwe kwa maslahi ya Bodi au Wataalam fulani tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali, sheria hii ikipita, itumike vizuri kuhakikisha maslahi kwa nchi yetu yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni muhimu katika kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema tukavitumia vyanzo vya mapato vya ndani ili kuongeza Pato la Taifa, badala ya kutegemea zaidi vyanzo kutoka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* wameonyesha ujuzi, uwezo na ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo ni vyema, kodi ya majengo katika Halmashauri zikakusanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili *TRA* ipewe jukumu la kukusanya kodi ya majengo, sheria iliyopo ni lazima ifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* ifanye kazi za kukusanya kodi ya majengo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ili Halmashauri ziweze kupata uwezo wa kukusanya kodi ili baadaye waweze kupata ujuzi na uwezo wa kukusanya mapato hayo wao wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa imefika wakati wananchi waruhusiwe kutumia baskeli za miguu miwili, hasa vijijini ambako usafiri mkubwa na rahisi ni baiskeli.

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, ninamshukuru Naibu Waziri, kwa maelezo yake yenye nia ya kudhibiti mapato katika nchi yetu. Kitendo cha kudhibiti pato letu, ndio kupatikana maendeleo ya nchi na wananchi wetu kwa ujumla. Tukiangalia uwezo wa Halmashauri zetu, tunaelewa kuna utofauti wa uwezo wa kiuchumi ndani ya Halmashauri zetu. *TRA* ni chombo kilicho na uwezo mkubwa juu ya ukusanyaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walio wengi kilio chao ni matumizi gani yanayotumiwa juu ya fedha zao za kodi. Tatizo la kutoelewa wananchi wetu, linatokana na Serikali yenyewe, kwani zama za uchaguzi tulisema Serikali itaendelea kujenga rasilimali watu wenye elimu na maarifa ya kufanya kazi ikiwemo kilimo, biashara na stadi mbalimbali. Laiti kama haya yangelifanyika, ninadhani kusingalitokea haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia ya Serikali kuikabidhi *TRA* kusimamia ukusanyaji mapato ndani ya Halmashauri zetu, wakati umefika sasa Serikali kusimamia mapato ili wananchi wetu waone jasho lao. Hii leo hakuna mwananchi anayeona matumizi ya kodi ndani ya Serikali yao. Barabara zetu mbovu, mashule hayatoshi, hospitali mbovu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tupige hatua, kazi ya *TRA* ionekane kimaendeleo na sio Serikali imeingiza pesa nyingi kupitia kodi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu hayo, ninasema ninaunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mimi ninashukuru kwa Muswada kwa sababu kila Mkoa, pamoja na Manispaa, kujipangia kodi yao sijui ni elimu au ndio rushwa. Pamoja na kupitisha Sheria hii, uwepo ufuatiliaji mkubwa. Sasa tumeona mengi; pesa zinavyokusanywa na kutumika isivyo. Kwa mfano, unakuta mfanyakazi wa *TRA* anakuwa anazungukia kwa wafanyabiashara anawaambia usilipe, nipe chochote nitakulinda. Ofisi ikipanga kwenda kwenye ukaguzi, anawapa siri wanafunga duka au anampa risiti za uwongo za kumlinda. Suala la baiskeli na pikipiki, kama sisi Wabunge tunaotoka Mkoa wa Kagera, wananchi wetu wanatulalamikia sana. Wenyewe wako tayari kulipa kodi itakayopangwa na kufuata sheria yoyote itakayopangwa. Kwanza, litasaidia ajira kwa vijana wetu. Jambo la kushangaza, Polisi huzikamata baiskeli zao na kuzilundika, jambo linalosababisha hasara kwa wananchi. Sasa pamoja na hayo, kama haiwezekani basi *TRA* iishawishi *SUMATRA,* itunge au ipitishe sheria ipitishwe kuliko kutudanganya na kuwanyang'anya mali zao ambazo zingekuwa zinaingiza kipato kikubwa sana.

Ninaupongeza Muswada huu ila ninaomba masuala yangu niliyoyaainisha kwenye maandishi yashughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kutoa ushauri na kupata maelelzo kuhusiana na Muswada huu katika mambo yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa viwango vya kodi za majengo vilishapitishwa na Halmashauri mbalimbali chini ya Sheria zao ndogo ndogo bila ya kufanya tathmini halisi za majengo na kutenganisha kodi za majengo kwa majengo yanayotumika kwa biashara au kukodishwa na majengo ya matumizi binafsi; je, *TRA* kama Wakala ataendelea kufanya makusanyo kwa viwango hivyo hivyo licha ya upungufu huo?

Pili, mfumo wa Kodi ya Mapato unaotumika sasa ndio kigezo cha viwango vya Kodi za Mapato Kitaifa, lakini katika baadhi ya Halmashauri viwango vya Kodi za Majengo ni kubwa zaidi ya mapato halisi ya majengo husika. Kwa msingi huo, kuna migongano katika ukadiriaji wa kodi Kitaifa kwa kuwa tu Halmashauri zimepewa uwezo wa kuwa na sheria zake ndogo ndogo na bila kujali mfumo wa Kitaifa kupanga viwango vikubwa na kufanya ukusanyaji wa kodi kama hizo kuwa mgumu. Bila ya kufanya marekebisho ya kodi kulingana wa Viwango vya Kitaifa kama msingi wa viwango vya kodi, basi *TRA* kama Wakala hata kwa mabadiliko ya sheria hii, itapata tabu kukusanya kodi halali bila kutumia mabavu na vitisho. Ni vyema basi, *TRA* ikapitia kwanza mpango mzima wa kodi hii ya majengo, kupanga viwango stahili, ndio ikachukua jukumu la kukusanya kodi hii ambayo wao pia wameshiriki na kuridhika katika viwango vyake.

Pamoja na kuchukua jukumu hilo ni vyema *TRA* ikaweka vigezo vya nyumba zitakazopewa msamaha wa kulipa kodi hii, ikiwa ni pamoja na Nyumba za Ibada, Shule za Serikali na Binafsi, Zahanati na Hospitali za Serikali na Binafsi, nyumba zilizojengwa kwa miti na tope (sio za matofali ya kuchoma). Pia tuangalie nyumba za wajane na wakongwe na wastaafu wasiokuwa na kipato chochote hata kutoka katika nyumba walizoachiwa kama urithi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ninapenda nichukue nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwasilisha vyema hoja yake mbele ya Bunge lako. Niseme kwamba, Muswada huu umechelewa kidogo, kwa sababu Halmashauri zetu zimekuwa na matatizo makubwa ya kupata mapato ya kutosha kuendesha shughuli zao. Jambo ambalo kama sheria hii ingelikuwepo mapema, Halmashauri zetu zingelikuwa zimepiga hatua kubwa kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa nami kutoa ushauri wangu kuboresha Muswada huu: Serikali ni lazima ihakikishe kwamba, kodi itakayokadiriwa ni lazima izingatie na uwezo wa walipa kodi. Hii ikitekelezwa, itawapa motisha walipa kodi kulipa bila kinyongo na usumbufu wowote. Jambo lingine ni kwamba, Serikali ihakikishe kwamba, inazijengea uwezo Halmashauri ili hatimaye ziweze kusimamia ukusanyaji wa kodi zenyewe. Aidha, Serikali kupitia *TRA*, iandae utaratibu ulio murua, ambao utawezesha kufanya marejesho ya kodi hizo kwa Halmashauri husika ili Halmashauri hizo ziweze kutumia kodi hizo kwa maendeleo yao. Pasiwepo na mizengwe yoyote.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninapenda kuunga mkono hoja hii.

*TRA* kupewa jukumu la ukusanyaji kodi wa majengo, itasaidia sana kupatikana kwa fedha ambazo wananchi wanachanga lakini hazifiki kunakohusika. Katika ukusanyaji wa fedha inaelekea kuna ubadhirifu katika Halmashauri zetu katika suala zima la ukusanyaji wa kodi hizi; kuna ubadhirifu na uzembe unaofanywa na baadhi ya watendaji. Hawa wengine wanakuwa na vitabu vya aina mbili za stakabadhi; kuna stakabadhi zinazoenda Halmashauri na nyingine zinaliwa tu. Kuna wengine walipao wanapewa stakabadhi ambazo hazina nembo za Halmashauri na wananchi wetu wengine hawana ufahamu, bora yeye apewe stakabadhi tu. Hii pia itasaidia kupata tathmini halisi ya majengo tuliyonayo na kuweza kudhibiti fedha vizuri. *TRA* itasaidia kuwapa uzoefu Watendaji wa Halmashauri wa mfumo bora wa ukusanyaji wa kodi na udhibiti wake. Ninaunga mkono hoja hii ya udhibiti wa fedha za umma ambazo zitatumika kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu, ingawa kwa kuanzia itaanzia katika Wilaya tatu za Mkoa wa Dar es Salaam, ninaiomba Serikali iharakishe baada ya Muswada kuridhiwa katika Mikoa yote ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha unaofanywa na Halmashauri zetu ambazo ndio chanzo cha kuwafanya wananchi wawe wavivu katika uchangiaji wa kodi, ambao ni wajibu wa kila mwananchi na wanatambua hivyo.

**MHE. ATHUMANI S. JANGUO:** Ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa marekebisho ambao shabaha yake ni kuboresha mapato ya Serikali za Mitaa kwa kutumia Uwakala wa *TRA* katika ukusanyaji wa kodi ya mali isiyohamishika. Kwa kuwa *TRA* wanao uzoefu wa ukusanyaji wa kodi na wameonyesha mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa kodi za Serikali Kuu, ninaamini kuwa, Uwakala wao kwa Serikali za Mitaa utaongeza mapato ya Serikali hizo. Ninapenda kuishauri Serikali kuwa, sheria hii iende pamoja na kanuni ambazo zitazingatia yafuatayo:-

(i) Utaratibu huu uwe na manufaa kwa wenye mali, kwani msingi wa kodi ni huduma zinazotolewa kwa watu zikiwemo miundombinu ya barabara, huduma za mifereji ya maji machafu, ukusanyaji wa takataka, ulinzi na usalama. Kwa hiyo ni muhimu, wakati kodi hizo zinathaminiwa na kusimamiwa, mamlaka hizo husika na wakala wao, yaani *TRA,* wahakikishe kuwa huduma hizo zinalingana na kodi.

(ii)Katika kukadiria kodi za mali hizo ni muhimu hasa katika maeneo ya miji kama Jiji la Dar es Salaam ambako sheria hii itaanza kutumika, pawe na uangalifu, kodi ziangalie maeneo ambapo mali hizo zipo kwa msingi ule ule wa namba moja hapo juu, yaani pale ambapo Serikali ya Mitaa inatoa huduma, kodi itozwe kufuatana na huduma zitolewazo. Penye huduma hafifu, kodi iwe chini na pale ambapo Serikali haitoi huduma yoyote si haki kuzitoza mali hizo kodi ya mapato.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, hayo yakitekelezwa, sina pingamizi na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. BASIL P. MRAMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono Azimio la Ununuzi wa Vyombo vya Usafiri Angani na *Central Corridor Transit Facilitation Agency* kwa sababu:-

(1) Mashirika ya Ndege Tanzania yatawezeshwa kuokoa gharama za kukodi ndege.

(2) Ajali za ndege zitapungua kutokana na ukodishaji wa ndege mpya kutumia fursa za mikataba hii.

(3) Kuhusu *Central corridor*, kutafungua uwezekano wa nchi husika kushirikiana kwa vitendo, mfano ubia, kuimarisha miundombinu husika ili itumike kikamilifu kwa faida zao. La msingi sana ni kuimarisha reli ya kati kwa kuipanua na kukamilisha mawasiliano ya *optic fibre* hadi Rwanda, Burundi na Kongo.

(4) Ni muhimu bandari ya Dar es Salaam kuimarishwa kwa hara kwa kuondoa matatizo yaliyopo ya siku nyingi na kutumia zaidi bandari za Tanga na Mtwara na pia bandari kavu (*dry ports)* zaidi ya iliyopo. Aidha, bandari ya Bagamoyo ingeweza kuimarishwa na kupewa jukumu mahususi.

(5) Inasikitisha na kustaajabisha kuwa ingawa wawekezaji ni wengi, maamuzi ya kibiashara hasa kuhusu bandari ya DSM yanacheleweshwa mno wakati ina majukumu kwa nchi jirani pia.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Miundombinu kuhusu Maazimio haya, lakini bado nina wasiwasi. Pamoja na masikitiko makubwa kuhusu usafiri wa majini nadhani Wizara hii itaona umuhimu kuwa na sheria kwa ajili ya vyombo hivyo. Kama mnavyoona mara kwa mara matatizo ya meli kwa mfano meli/boti zilizoletwa ziendazo kasi kwa mfano matatizo ya MV Bukoba, kwa kweli matatizo ni mengi. Na juzi zilitolewa shilingi milioni 400, je, hizo pesa zilifanya nini kama si kuendelea kuyaharibu maisha ya wananchi? Pili, ni aibu kwenye nchi pesa zinatolewa kuimarisha bandari ya Kamondo Bukoba mjini zisifanye kitu cha maana. Nadhani ikiwekwa sheria mambo mengi yatakwenda vizuri. Kuhusu meli ya mizigo Umoja sijui iliishia wapi.
Naomba nijibiwe masuala haya kuniridhisha mimi pamoja na wananchi wa Kagera ambao wana matatizo makubwa ya usafiri wa MV Bukoba mfano kama kusafirisha mizigo ni shida kubwa sana kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Baada ya Mradi kukamilika, mradi huo wa Rusumo, utaweza kuzalisha megawati 60 ambapo kila nchi tumekadiria itapata megawati 20 kila mmoja. Umeme wa Rusumo utapelekwa na kusambazwa katika Wilaya za Ngara, Biharamulo, Muleba na Kibondo ambapo mahitaji ya umeme kwa miji ya Ngara, Biharamulo na Muleba kama tulivyosema ni jumla ya megawati 3 tu.

**MHE. SAVELINA J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana mimi nina swali moja la nyongeza kwanza ninasikitika anavyosema kwamba maporomoko yale ni madogo. Halafu kitu ambacho ni masikitiko tutaendelea kutumia umeme wa kuchangia mpaka lini? Sasa hivi tunatumia umeme wa Uganda kwanini sisi wenyewe tusiwe na umeme wa kujitegemea Serikali inampango gani na suala hili la kukaa na kutegemea umeme wa jirani?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba maporomoko ya maji yanayohitajika kuzalisha umeme yanapimwa kwa taratibu nyingi na vigezo vingi na kwa kusema kweli hata kama macho yanaonyesha kwamba maporomoko ni makubwa lakini wataalam wamebaini kwamba maporomoko ya pale hayatoshi kuzalisha umeme ambao ni endelevu.

Kwa hiyo, imeonekana kwamba tuna maporomoko ya Rusumo ambayo yanaweza kuzalisha megawati 60. sasa kwa sababu ni joint project ya nchi tatu na kwa kusema kweli si kitu kigeni na tutakapozalisha umeme pale sisi kama Tanzania tunatarajia kuwa na mgao wa megawati 20. Eneo lile peke yake halina mahitaji ya megawati zaidi ya nne.

Kwa hiyo mimi naamini kwamba mradi huu utakapotekelezwa basi maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyazungumzia yatapatau umeme wa kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umeisha, tathmini ya leo ya ujibuji maswali. Kwa kiwango kikubwa kabisa napenda niwapongeze watu wote kwa sababu swali la kwanza tumetumia dakika nne, la pili nane, la tatu nane, la nne sita, la tano tano, la saba nne, la nane sita, la tisa nane, la kumi sita, la kumi na moja saba, la kumi na mbili tano, kumi na tatu nne, kumi na nne tano, na la kumi na tano dakika tano. Halafu Mawaziri karibu wote wamejibu page moja kwa majibu yao. (*Makofi*)

Mtaona kwamba angalau kila swali limepata maswali ya nyongeza angalau mawili haya mengine kwa sababu ya nature bado kidogo uulizaji wa maswali ya nyongeza ni tatizo mnasema mengi. Lakini Mawaziri sasa wamefanya kazi nzuri na tuna kwenda zaidi. Sasa tutadai font ya aina moja maana wengine wana font ndogondogo inakuwa page moja kumbe ni mbili. Kwa hiyo tutakuwa na standard font ya kujibu maswali.

Kwa hiyo, itakuwa page moja *standard font.* Kwa hiyo, bado maswali ya nyongeza mnatoa hadithi halafu kama Waziri amejibu mnauliza swali la nyongeza linafanana na jibu la msingi. Kwa hiyo, nalo hilo mnapoteza wakati wa watu wengi kuchangia. Kwa hiyo, *font* zitakuwa za aina moja Wabunge Maswali ya nyongeza yawe mafupi. Kwa hiyo, kwa ujumla naomba niwapongeze haitupi taabu sisi kuongoza kikao kwa maana hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa wageni. Tunao wageni kama ifuatavyo:-

Tunaye Ndugu D. Smith, *if you can stand up please,* yeye huyu Wabunge wa zamani wengi mtamfahamu. Miaka mitano iliyopita tulikuwa na mradi uliokuwa unaitwa *State University of New York* ambao ulikuwa ni mradi wa kuimarisha Bunge.

Mradi huu ulimalizika nafikiri mwaka huu mwanzoni. Sasa tumeingia kwenye mradi mwingine na *British Council* kuhusu hiyo hiyo kuimarisha mambo ya Bunge na yeye huyo ndiyo *Senior Consultant* wa mradi huo na tutakuwa naye kwa kipindi kirefu. Tunamfahamu kwa sababu kazi hii ameweza kufanya kwenye Bunge la Uganda na Mabunge mengine na Tanzania pia. Kwa hiyo, Wabunge wengi hamjafaidika lakini lengo letu ni hilo. Kwa hiyo, amekuja kuripoti nadhani kazi itaanza mapema. *Welcome and we are happy to see you*. (*Makofi*)

Jana nilitangaza kwamba kuna Mabalozi wetu wale Balozi wa Umoja wa Ulaya Mheshimiwa Tim Clerk amefuatana na Afisa wake Theo Cassipias, *please if you can sit.* Hawa pia tunao mradi mwingine wa *deepening democracy* ambao unafanyika kwa ushirikiano na Jumuiya ya nchi za Ulaya, pamoja na *UNDP* ambao pia unaangalia maeneo mbalimbali ya kuimarisha Bunge letu tukianzia na uwezeshaji wa Wabunge wenyewe *staff* yetu na pia nyenzo za kufanyia kazi. Tutashirikiana nao katika Mpango

Mkakati ambao Bunge letu linaandaa tunafanya kazi pamoja. Wako na Mabalozi wengine jana niliwatangaza lakini kusudio lao ni hilo.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa, Mbwana Haji Mbwana, aliwahi kuwa Mbunge zamani wa Micheweni, karibu sana. Halafu tuna mgeni wa Mheshimiwa Marombwa, Mheshimiwa Luteni Kanali Msumba kutoka Morogoro. Halafu tuna wakufunzi na wanafunzi wa *VETA* kanda ya kati naomba msimame. Karibuni sana. Tunao bado wanafunzi wa Tumaini ambao baadaye saa saba watakutana na Wabunge wa Iringa katika Ukumbi wa Msekwa. Kwa hiyo, wapo wanafunzi kutoka Iringa, *Tumaini University.* Lakini watakutana na Wabunge wa Iringa saa saba katika Ukumbi wa Msekwa, karibuni sana.

Sasa nina wale wageni ambao nimeletewa vikaratasi ingawa nimekataa hivyo, kuanzia wiki ijayo vikaratasi vya wageni namna hii tutakuwa hatuvisomi. Tuna wageni wa Mheshimiwa Fuya Kimbita , ambapo ni mke wake Monica Fuya na watoto. Watoto ni Godwin na Gideon. Halafu tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Kimbita hao wanatoka Taasisi inaitwa *Global Action* ya Marekani yupo Miss Michelle Linden ndiyo Afisa Mtendaji, *can you please stand up*. Tunaye Dr. Mayunga ndiyo *Country Director.* Halafu tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mnyaa, ambaye ni mkewe Mrs Mnyaa Bi. Fatma, karibu sana. Kuna habari nyingine sitapenda kuitangaza hapa.

Matangazo ya kazi, kwanza kabisa Waheshimiwa Wabunge napenda kuwatangazia kwamba katika kikao ambacho Mheshimiwa Spika amehudhuriwa sasa hivi napenda kuwatangazieni kwamba katika kikao ambacho Mheshimiwa Spika anahudhuria sasa hivi huko *Cape Town* wenzetu wafuatao wamepata vyeo huko.

Kikao anachohudhuria Mheshimiwa Spika kinaitwa *Inter Parliamentary Union (IPU)* hii ni jumla ya Mabunge yote katika dunia huwa kuna Bunge moja linaitwa *IPU.* Katika Bunge hilo Mheshimiwa Kilonsti Mporogomyi, amechaguliwa kuwa Makamu Rais wa Kamati ya Fedha na Biashara yaani *Trade and Finance* ya *IPU.* Halafu na Mheshimiwa Susan Lyimo, amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji *Coordinating Committee* ya Wabunge wanawake kundi la Afrika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wenzetu wawili wamefanya vizuri na sisi tunapenda watu wakienda kuhudhuria Mikutano waje na vitu sio wanakwenda kuwa wasindikizaji. Tunawapongeza sana.

Nimeshatangaza Mkutano wa Wabunge wa Mkoa wa Iringa saa saba katika Ukumbi wa Msekwa. Halafu Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Mheshimiwa Omar Kwangw' anaomba Wajumbe wake wakutane leo mara baada ya kipindi hiki cha maswali katika chumba 428 kutakuwa na Mkutano huko. Halafu tuna Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Wilson Masilingi, anaomba Wajumbe wake wakutane saa sita na nusu katika Chumba namba 231.

Sasa kuna tangazo la uchaguzi Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba baada ya Mheshimiwa Rais kufanya mabadiliko ya Baraza lake la Mawaziri watu

wengine walibahatika kuteuliwa kuwa Mawaziri au Manaibu Waziri kwa hiyo kusababisha mapendo katika nafasi walizokuwa wanasimamia moja ni ile ya Uchaguzi wa Bunge la Afrika.

Mheshimiwa Dr. James Wanyacha, alikuwa ndiyo Mjumbe Kwa hiyo, nafasi hiyo iko wazi matangazo yapo pale kwenye ubao mpaka sasa wamechukua fomu wawili bado muda wa kuchukua fomu ziko pale.

Lakini pia tuna nafasi ya Chuo cha Ufundi Arusha hii hakuna aliyechukua fomu. Kwa hiyo, mnaarifiwa kwenda kuchukua fomu. Hili Bunge la Afrika tuna nafasi mbili wazi kwa sababu Mheshimiwa Kabuye yeye alikuwa ndiyo Mbunge wa Bunge lile hata kama hahuzurii vikao vile lakini utakumbuka kwamba yeye aliondolewa kwa mujibu wa mahakama Kuu kama matokeo ya uchaguzi wake yalibatilishwa.

Lakini kwa sababu amekata rufaa kwenye Mahakama ya Juu zaidi hatuwezi kusema hapa lipo wazi. Kwa hiyo, nafasi hii hatuchagui bado. Kwa hiyo Waheshimiwa mkachukue fomu za kugombea nafasi hizo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na kazi ya leo. Katibu endelea na *Order Paper.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana wazungumzaji wote walikwisha sasa naomba mtoa hoja aweze kutoa ufafanuzi katika mambo yaliyoulizwa na kuchangiwa.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwanza napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie kwa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge mbalimbali kwa maazimio na itifaki nilizoziwasilisha jana hapa Bungeni. Kwa heshima kubwa naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hoja hizo kwa kusema nao ni wanane.

Mheshimiwa Ludovick John Mwananzila, Mbunge wa Kalamo kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Herbert James Mntangi Mbunge wa Muheza, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga Mbunge wa Tabora Mjini, Mheshimiwa Juma Njwayo Mbunge wa Tandahimba, Mheshimiwa Godfrey Zambi Mbunge wa Mbozi Mashariki, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela na Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Savelina Mwijage Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Basili Mramba Mbunge wa Rombo na leo hii asubuhi nimeupata wa Mheshimiwa Daina Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kusaidia kujibu hoja na kutoa ufafanuzi kidogo kwa hoja mbalimbali zilizotolewa. Wabunge wote waliochangia wameunga mkono hoja zote kwani wameona zina umuhimu kwa uchumi wa nchi yetu naomba niwashukuru sana. Mawazo yao yote ni mazuri yatazingatiwa kwani yanalengo ya kuboresha masuala ya uchukuzi katika nchi yetu. Sasa niseme Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mohamed Sinani na Mheshimiwa Mzindakaya walitoa hoja ambazo zinafanana. Mpango wa Serikali wa kuboresha huduma za Bandari na pia kuondoa msongamano Bandari ya Dar es Salaam. Niseme Serikali imeruhusu kampuni binafsi kuanzisha *ICD* hadi sasa zipo Kampuni sita ambazo zinapokea makontena moja kwa moja na kampuni nyingine zaidi zitaruhusiwa. *Tanzania Road Haulage , AMI, MOFET, Malawi Cargo Centre, Ubungo Container Depot*, na *Dar es Salaam International Terminal*. Bandari kuongezewa maeneo mengine kuhifadhi kontena ndani ya Bandari litazingatiwa. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imenunua eneo la hekta 19.5 Kurasini kwa ajili ya kupanua Bandari ya Dar es Salaa. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ipo katika mchakato wa kujenga gati nyingine mbili za kuhudumia makontena ndani ya eneo la Bandari ambazo tunategemea kama mambo yatakwenda vizuri ujenzi wake utaanza mwakani.

Lakini napenda nisisitize jamani, wenzetu tumeshawasisitiza wa Bandari wafanye juhudi kwa kushirikiana na Sekta nyingine ambazo zinatumia Bandari kuona umuhimu wa matumizi ya Bandari. Wenzetu wa Singapole wanaishi kwa ajili ya Bandari ni kwanini na sisi tusifanye hivyo. Mheshimiwa Ludovick Mwananzila kwa niaba ya Mwanyekiti alitoa rai kuwa *TCAA* na *TAA* wasimamie usalama na wawe na wataalam wa kutosha aidha wahamasishe watoa huduma. Ushauri huu ni mzuri tunauchukua kwa utekelezaji. Vile vile Mheshimiwa Abubakary Shamis Faki yeye ametoa hoja kwamba je, wawekezaji wa nje wataruhusiwa kununua au kukopa vifaa vya ndege baada ya Tanzania kuridhia Mkataba na Itifaki ya Vifaa vya Ndege? Tunasema ndiyo, kampuni yoyote itaruhusiwa kukopa iwe ya umma au binafsi ili mradi kampuni iwe imesajiliwa nchini na makao makuu ya kampuni yawe nchini. Je, Itifaki ya Mkataba ipi ina nguvu pale ambapo tafsiri inatofautiana. Kwa mujibu wa Mkataba huu itifaki ina nguvu zaidi ya mkataba pale ambapo patatokea mkanganyiko katika tafsiri. Kuridhiwa kwa mkataba na itifaki kwa jumuiya za kikanda. Mkataba na Itifaki kwa jumuiya za kikanda. Mkataba na Itifaki kwa jumuiya za kikanda. Mkataba na Itifaki inataka nchi wanachama wa *ICAO* ziridhie nchi tatu kwa mkataba na nchi nane kwa Itifaki ili zianze kutekelezwa. Uchaguzi wa Mahakama alizungumzia pia Mheshimiwa Faki; tunasema Mkataba na Itifaki zinatoa fursa kwa mkopaji na Mkopeshaji kuchagua mahakama pale watakaposhindwa kuelewana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aliuliza tena nini dhana ya Serikali kusaini Mkataba huu ikiwa kifaa chenyewe kinachokopeshwa ni dhamana? Kwa kuridhia Mkataba huu Serikali haitoa dhamana isipokuwa ipo kutoa ushirikiano endapo mkopaji atashindwa kutekeleza masharti waliyokubaliana wakati wa kukopa. Aidha Serikali itakuwa tayari kulinda maslahi ya pande zote mbili endapo mmoja atashindwa kutekeleza masharti ya mkopo. Pia Mheshimiwa Faki, alisema ni jinsi gani chuo chetu cha *DMI* kinanufaika na

ushirikiano chini ya Mkataba huu wa *ICOS*. Chuo cha Mabaharia ndiyo chuo rasmi cha wataalam cha waendeshaji wa shughuli za bahari kwa Afrika Mashariki na kinatambuliwa na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Usafiri wa Majini Duniani. Serikali kupitia Chuo hiki imeandelea kuboresha mitaala ya ufundishaji katika chuo hicho ili kikidhi mahitaji ya wanaafrika mashariki na wanayo nia sasa ya kuanzisha digrii programu pale kwenye Chuo hiki. *DMI* inapokea wanafunzi wa kutosha kila mwaka kutoka Kenya Uganda na Tanzania na nchi nyingine na hivyo kuipatia nchi mapato yatokanayo na ada ya mafunzo.(*Makofi*)

Mheshimiwa Zambi alizungumzia suala la usalama wa usafiri majini uimarishwe na *SUMATRA* ipewe nyenzo na nguvu kudhibiti vyombo vinavyokiuka Sheria na kuhatarisha usalama. Hilo ni wazo zuri na tunalizingatia tayari *SUMATRA* imeshachukua hatua za awali ya kufunga mitambo ya mawasiliano ili kuboresha mawasiliano ya vyombo vya majini kwenye bahari, Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa ili kurahisisha uratibu wa ufuatiliaji wa safari za meli. Tunao mnara pale Magogoni, ukamilishaji wa mnara huo wa mawasiliano kwa ajili ya uokoaji na utafutaji pamoja na miendo ya meli katika Bahati ya Hindi unazidi kukamilishwa na tunategemea mnara huu utakamilika mwanzoni mwa mwezi ujao. Hata hivyo uimarishaji na ukaguzi na udhibiti wa vyombo vya usafiri majini unafanywa na *SUMATRA* ili vyombo hivyo vikidhi matakwa ya Sheria ya Usalama. *SUMATRA* inahamasisha wawekezaji wa nje na ndani kununua vyombo vipya na bora zaidi ili kutoa huduma bora zaidi ili kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi na tayari mazungumzo yameanza kwa kushirikiana na *TIC* ili kuishawishi Serikali kuwekeza na kuweka vivutio maalum kwa ajili ya wawekezaji kwenye vyombo vya majini. Kuhusu uimarishaji wa usalama kwenye maji na bandari Tanzania hasa kudhibiti vitendo vya uharamia, Tanzania kwa kushirikiana na *IMO* imekuwa na Mikutano ya Kimataifa kuhusu kudhibiti uharamia huo baharini ukanda wa *Indian Ocean*. Tarehe 14 – 18 Mwezi huu na kama mchakato wa kuwa na mkataba wa ushirikiano katika ukanda huu suala hili pia alizungumzia Mheshimiwa Sinani tunalipa uzito unaofaa.

Kulikuwa na suala la Mkataba na Itifaki iliyoridhiwa itatumika pia kwa ununuzi wa vyombo vingine vya uchukuzi? Tunasema Mkataba utakaotumika kwa ajili ya manunuzi ya vyombo vya uchukuzi ni huu ambao unaridhiwa sasa hivi. Hata hivyo itifaki inayoridhiwa sasa inahusu vyombo vya usafiri wa anga tu. Lakini hapo baadae tukikuleteeni kwa vyombo vingine tutakuombeni muipitishe ili na kwenye vyombo vingine waweze kunufaika. Mkataba unatoa fursa kwa itifaki nyingine kuanzishwa zikiwemo itifaki za ununuzi wa vyombo vya usafiri wa reli, majini, vifaa vya kilimo na mitambo ya kuchimbia madini.

Mheshimiwa Mwijage yeye alitoa maoni yake mbalimbali kuhusu usafiri wa majini hasa Ziwa Victoria Bukoba kwenda Mwanza au Mwanza kwenda Bukoba. Ni kweli kuna uhaba wa vyombo vya usafiri majini kati ya Mwanza na Bukoba hasa baada ya *MV Bukoba* kuzama na pia kutokana na kuharibika kwa *MV Victoria* kutokana na umri wake kuwa mkubwa.

Lakini Meli hii imefanyiwa matengenezo makubwa ikiwa ni pamoja ya injini zake zote pamoja na ukarabati wa Meli yote kwa ujumla. Lakini baada ya matengenezo kufanyika na ikaanza majaribio yalijitokeza matatizo mengine ya *gear box* kwa hivyo imebidi meli hii tuisimamishe kidogo ili tuangalie masuala ya *gear box. MV Victoria* inaendelea kutengenezwa pale itakapohitajika ili kuhakikisha wananchi wanapata usafiri kati ya Mwanza na Bukoba na pale ambapo MV. Victoria itakuwa matengenezoni basi MV Serengeti itaendelea kutoa huduma hiyo. Ulizungumzia juu ya Boti mbili ziendazo kazi zilikuwa zinatoa huduma kati ya Mwanza na Bukoba tumezisimamisha baada ya kubainika kuwa sio salama kwa ajili ya kutoa huduma na Mkaguzi wa Serikali ameelekeza mapungufu yaliyopo yarekebishwe ambayo ikikamilika *SUMATRA* itaikagua na itaruhusu tena kutoa huduma hizo. Namwomba Mheshimiwa awe na uvumilivu kidogo. Mheshimiwa Sinani alizungumzia kuhusu Bandari ya Mtwara kutotumika ipasavyo na wangine vilevile walizungumzia suala hili. Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu itawasiliana na Asasi zote zinazohusika na utoaji huduma katika Bandari si ya Mtwara tu bali pia na zingine kwa lengo la kuhakikisha kuwa Bandari zote zinatumika ipasavyo ili kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilipata nafasi ya kubadilishana mawazo na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwamba sisi Bandari tuko tayari tuitumie Bandari ya Mtwara, basi tuombe na wenzetu wa Fedha watupe msukumo ili suala hili liweze kufanikishwa. Hapa nitapenda nitoe indhari kidogo kwamba ni vyema basi tujiridhishe kwamba vile vyombo vidogo vidogo ambavyo vitaondosha makontena kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam basi viwepo. Isije ikawa tena tunaondosha tatizo kutoka Dar es Salaam na kulihamishia Mtwara.

Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo yeye alisema Reli iliyong’olewa kusini mwa Tanzania ilirudishwe. Ni kweli nafikiri siku zile maamuzi yaliyofanyika yalifanyika kutokana na wakati ule. Lakini wakati huu reli hii tunaihitaji sana na ndiyo maana Serikali kupitia Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara ambao unashirikisha Tanzania Msumbiji Zambia na Malawi unatoa kipaumbele ujenzi wa mindombinu ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Reli kutoka Bandari ya Mtwara kwenda kwenye maeneo ya kiuchumi kama vile mgodi wa Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na juhudi hizi zinaoana na malengo ya mpango kabambe wa uchukuwa ambao nao pia una malengo ya kujenga reli hiyo lakini katika kipindi cha muda mrefu.

Mheshimiwa Bakari Shamis alizungumzia kwamba Serikali iagize vivuko kupitia mkataba na itifaki inayohusu vifaa vihamishikavo ili kuimarisha usafiri. Tunakubaliana na wazo lake lakini kwa sasa kama nilivyosema Mkataba huu na itifaki iliyopo inayoanzisha kutekeleza ni vifaa vya usafiri wa anga ambayo imeanza kutekelezwa tangu mwaka 2006. Mkataba na Itifaki, vinatoa fursa kwa itifaki za usafiriwa majini, usafiri wa reli na itifaki za vifaa vya kilimo na mitambo ya kuchimba madini kuanzishwa na *ICAO* na ikafanya kazi. Ununuzi au uagizaji wa vivuko au injini zake utawezekana baada ya itifaki ya usafiri wa majini kuanzishwa na kuridhiwa. Lakini Wizara ya Miundombinu kwa kupitia TEMESA wataendelea kushughulikia masuala ya vivuko hapa nchini.

Mheshimiwa Mramba yeye alisema anaunga mkono hoja ametaka Serikali iimarishe miundombinu ya reli, bandari na barabara na matumizi ya *Faiber Optic* na aidha Serikali itumie bandari za Tanga na Mtwara kujenga bandari mpya Bagamoyo na kurahisha maamuzi. Sisi tunasema Mheshimiwa Mramba tunakubaliana naye kwa sababu alikuwa ni mwenzetu katika Sekta hii ya miundombinu tumepanga wote mambo yetu mengi haya mazuri kwa hivyo tutayazingatia hasa uimarishaji wa miundombinu pale ambapo bajeti itaruhusu. Aidha tutaendelea kuishawishi sekta binafsi ili ishirikiane na Serikali katika kuboresha miundombinu.

Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya yeye alisema Mwekezaji katika Reli ya Kati ameonyesha nia ya kufunga huduma za Reli ya kutoka Manyoni – Singida na Mpanda – Kaliua. Lakini tuwaridhishe Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba kulingana na Mkataba wa ukodishaji Mwekezaji amepewa jukumu la kutoa huduma na suala la uendelezaji wa miundombinu ya reli ni jukumu la Serikali. Hata hivyo suala la kusitisha huduma katika njia nilizozitaja halijaletwa rasmi Serikalini na kimsingi Serikali haitakubaliana na hatua ya kufunga huduma katika eneo haya. Kwa sababu tokea mapema tulisema reli hizi mbili Manyoni – Singida na Mpanda –Kaliua hazina faida kibiashara, tunatoa *service* na ni jukumu la Serikali kufanya *sevrice* kwa maeneo haya mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni Mheshimiwa Diana Chilolo ambayeamezungumzia msongamano wa mizigo bandarini ambapo ni kitu nimekwishakielezea. Lakini yeye alizidisha zaidi kwamba *TICTS* ifutwe. Mimi nasema *TICTS* isifutwe, lakini kama kuna hitilafu ambazo zinatokana na utendaji wa *TICTS* basi zitolewe hitilafu na *TICTS* iimarishwe iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuimarishwa bandari ya Tanga na Mtwara, nakubaliana naye. Serikali inunue meli kubwa kwa safari za kibiashara za masafa marefu, ni wazo zuri. Lakini tulikubalina kimsingi kwamba shughuli za kibiashara sasa zifanywe na sekta binafsi na natoa wito kwa wale ambao wanao uwezo wachangie katika kufanya shughuli hizi za safari za meli. Wanunue meli kubwa kwa ajili ya safari za masafa marefu ili nchi nayo iweze kunufaika na iweze kujidai kwamba tunazo meli za Watanzania zinafanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, alizungumzia juu ya wizi wa mizigo na vifaa vya magari kung'olewa, *radio cassettes*. Pale bandarini tumeweka utaratibu mzuri tu kwamba tuna fomu, kabla gari lako halijateremshwa ndani ya meli, linachekiwa na watu wa meli na watu wa bandari na ku-*tick* kila kitu kilichomo ndani ya meli. Kama kuna hitilafu tunajua kwamba hao ni watu wa ndani ya meli au ni bandari na hatua zinazofaa zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, amezungumzia juu ya usafiri wa ndege kwamba tuko nyuma sana kuliko nchi ya Kenya. Nchi ya Kenya ina ndege nyingi. Sasa mimi niseme ni kweli nchi ya Kenya wamefaidika, wana ndege nyingi, lakini na sisi kupitia Itifaki hii tuliyoipitisha jana, tutapata nafsi kwa kampuni yetu ya *ATCL* kukopa ndege kwa sababu imo katika masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni Serikali kukuza usafiri wa anga ili kuinua mapato. Nipende tu kusema kwamba usafiri wa anga una nafasi yake kubwa katika kuchangia uchumi wa nchi hii. Sasa tunauona umuhimu wake na Serikali inatoa msukumo ipasavyo kwa usafiri wa anga ili uweze kuchangia katika uchumi wa nchi hii. Amesema kwamba wakati umefika sasa kuthubutu kujenga reli ya Tanga na Musoma na kuimarisha usafiri wa reli. Nakubaliana naye, na siku zote nilipokuwa Naibu Waziri wa Miundombinu, nilikuwa nasisitiza umuhimu wa kuwekeza mara moja katika reli ili tuweze kuvuna matunda makubwa. Unapo-*invest* mara moja kwenye reli, unakaa zaidi ya miaka 20 huja-*invest* tena, ni kwa sababu reli ile haihitaji matengenezo makubwa. Lakini unapo-*invest* katika barabara, *after every two years*, lazima barabara uzibe viraka au uifanyie *reserves*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, yakiletwa maoni ya masuala ya reli kuimarisha, tutakuombeni sana mtupe msukumo. Katika Bunge lililopita tulisema tutatoa reli za 80 *pounds*, tuweke za 120 *pounds*. Kwa hiyo, hiyo inahitaji *investment* kubwa ambayo lazima Serikali ibebe. Kwa hiyo, bajeti hii ikija kwamba reli iimarishwe, tutakuombeni sana mtusaidie. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Kaboyonga, anakerwa sana pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Reli hii. Matatizo ya Reli ya Kati ni matatizo yetu sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa hoja kwamba Itifaki na Mikataba niliyowasilisha sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba Ulioanzisha Kamati ya Kudumu ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini ya Mwaka 2006 *(Protocol Amending the Agreement Establishing the Inter-GovernmentalStanding Committee on Shipping – ISCOS for the Year 2006)***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Kamati ya Kiserikali ya Usafiri wa Baharini wa Mwaka 2006 liliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wa Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati wa Mwaka 2006 *(Agreement for Establishment of the Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency – TTFA, 2006) na* Azimio la Bunge Kuridhia Mkataba wa Shirika la Kimataifa Linalosimamia Usafiri**

**wa Anga Duniani – *ICAO* wa Mwaka 2001 Kuhusu Vifaa vinavyohamishika**
***(Convention on Intrenational Interest in Mobile Equipment***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Wakala wa Uwezeshaji na Uchukuzi wa Mizigo Ukanda wa Kati wa Mwaka 2006 na Azimio la Bunge la Kuridhiwa Mkataba wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani wa Mwaka 2001 yaliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba Kuhusu Masuala Maalum yahusuyo Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika *(The Protocol to the Convention on International Interest in Mobile Equipment on Matters Specific to Aircraft Equipment)***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Masuala ya Vifaa vya Ndege Vinavyohamishika liliridhiwa na Bunge*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, Maazimio haya yote matatu yamepita na yaendelee kwa wakati unaostahili. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ujasiri na uhodari wako katika kujibu, unafanya kazi! *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007
### *(The Electricity Bill, 2007)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Umeme ya Mwaka 2007 *(The Electricity Bill, 2007)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika, kwa kutupatia muda wa kutosha kuandaa Muswada wa Sheria ya Umeme. Natoa shukurani za pekee kwa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kwa ushauri, maoni na kutoa michango ya mawazo thabiti iliyoboresha upeo na mwelekeo wa Muswada huu. Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wao wa dhati katika maandalizi ya Muswada huu kupitia Semina tulizoendesha Dodoma, Februari, 2008 na Dar es Salaam Machi, 2008. Hakika ushirikiano mlionipa mimi binafsi, Naibu Waziri wa Nishati na Madini, watumishi wa Wizara pamoja na mashirika/taasisi zake ni kielelezo na mfano wa kuigwa katika maandalizi ya Miswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandalizi ya Muswada huu, Wizara yetu imejifunza mambo mengi yanayojenga umakini na umahiri wa utendaji katika kushughulikia masuala muhimu kama vile nishati ya umeme ambayo ni muhimu katika kusukuma uchumi na maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msingi wa Muswada wa sheria inayopendekezwa unatokana na Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003 na Mwelekeo wa Sekta ya Umeme *(New Power Sector Direction)* wa mwaka 1999. Sera ya Taifa ya Nishati inatoa mwongozo wa kurekebisha sekta ya umeme kwa kutenganisha majukumu ya kisera, usimamizi, na uendeshaji wake kibiashara. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa kuongeza kasi ya uwekezaji katika sekta ya umeme, Sera inasisitiza umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi katika kuendeleza sekta ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Muswada wa Sheria mpya ya Umeme, mchakato wa kuandaa Muswada huu ulianza rasmi mwaka 2003. Rasimu ya Muswada wa Sheria mpya iliwasilishwa kwa wadau mbalimbali kupitia semina zilizoandaliwa na Wizara ya Nishati na Madini chini ya usimamizi wa iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara na Kamati ya Nishati na Madini kwa sasa. Maoni ya wadau yamezingatiwa katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu wa 2008, Wizara ya Nishati na Madini iliandaa Semina mbili kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge ili kupata maoni yao kabla Muswada huu haujawasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini. Maoni ya Kamati yamezingatiwa katika kuboresha Muswada huu kabla ya kuuwasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maudhui na mpangilio wa Muswada huu, naomba kutoa ufafanuzi kuhusu misingi ya kutunga sheria hii inayopendekezwa, hususan Sera ya Taifa ya Nishati, Mwelekeo wa *TANESCO*, Mpango wa Kuimarisha Hali ya Kifedha ya *TANESCO*, Umeme Vijijini, na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Sera ya Taifa ya Nishati: Dira ya sekta ya nishati ni kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa Taifa, na hivyo kuboresha hali ya maisha ya wananchi katika hali endelevu bila kuathiri mazingira. Dhamira ya Sera ya Nishati ni kujenga hali bora kwa ajili ya utoaji wa huduma za nishati zilizo salama, za uhakika, zenye ufanisi na za gharama nafuu kwa sekta zote katika misingi endelevu. Sera ya Nishati inatambua umuhimu wa kuwa na Sheria ya Umeme ambayo inakidhi mahitaji ya washiriki wote kwenye sekta pamoja na utaratibu mzuri wa kusimamia na kudhibiti maendeleo ya sekta ya umeme. Sera ya Nishati inatambua umuhimu wa kurekebisha sekta ya umeme ili kuweka mazingira bora ya kushirikisha sekta binafsi katika uendelezaji wa sekta iliyo endelevu. Nishati ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Taifa. Katika kipindi cha miaka mitatu ijayo Sekta ya umeme inatarajiwa kukua kutoka asilimia 8.5 hadi 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme vijijini, Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003 inatambua kuwa umeme vijijini ni moja ya changamoto za sekta ya nishati

na upatikanaji wa umeme vijijini ni suala la maslahi ya Taifa na ni muhimu kwa ukuaji wianishi wa uchumi na maendeleo ya kijamii. Kwa sasa hivi katika asilimia kumi (10%) ya wananchi wanaopata huduma ya nishati ya umeme nchini ni asilimia moja (1%) tu kati ya hao ndio walio maeneo ya vijijini. Waliobaki ni watumiaji waishio mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1997, *TANESCO* iliwekwa chini ya Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* kwa lengo la kubinafsishwa. Matarajio ya Serikali katika kipindi hicho yalikuwa ni kukamilisha maandalizi ya kurekebisha sekta ya umeme na hatimaye kubinafsisha *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Septemba 2005, Serikali iliamua kuiondoa *TANESCO* kwenye orodha ya mashirika ambayo yalikuwa yanasubiri kubinafsishwa ili kutekeleza mipango ya kuimarisha na kupanua miundombinu ya *TANESCO* katika kipindi cha mpito, na kubuni mkakati mpya wa kurekebisha sekta ya umeme. Hivyo basi, Muswada huu haulengi kuibinafsisha *TANESCO* bali unalenga kuweka mazingira bora kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika biashara ya umeme kwa ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 2 Februari, 2007, Serikali iliridhia Mpango wa Kuimarisha Hali ya Kifedha ya *TANESCO (Financial Recovery Plan 2006 – 2010)*. Serikali inatambua kwamba mafanikio ya Mpango huu yanategemea sana kufikiwa kwa vigezo muhimu *(assumptions).* Lengo la Mpango huu ni kuiwezesha *TANESCO* kujiendesha kibiashara bila kutegemea msaada wa Serikali na kuipa nguvu ya kuchangia katika ukuaji wa sekta na uchumi kwa ujumla na hatimaye iweze kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua kadhaa kulisaidia Shirika la *TANESCO* kufikia malengo ya utekelezaji wa Mpango huu. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Kuiwezesha *TANESCO* kupata mitambo ya kufua umeme ya kudumu yenye uwezo wa MW 145 (Ubungo *MW* 100 na Tegeta *MW* 45) na kukodi *(MW* 185) ili kukabili uhaba mkubwa wa umeme uliojitokeza kuanzia mwaka 2003 hadi mwanzoni mwa mwaka 2006.

(ii) Kulipia gharama *(capacity charge) kwa* mitambo ya kukodi na kuendelea kugharamia nusu ya *capacity charge* ya *IPTL*.

(iii) Kubadili jumla ya shilingi bilioni 1.132 ya madeni ya *TANESCO* kuwa mtaji.

(iv) Kuidhamini *TANESCO* kukopa shilingi bilioni 300 kutoka muungano *(syndication)* wa benki na mashirika ya kifedha nchini.

(v) Kuendeleza juhudi za kununua deni la wakopeshaji wa *IPTL* na kubadilisha mitambo ya *IPTL* ili iweze kutumia gesi asilia badala ya mafuta.

(vi) Kuimarisha na kulinda vyanzo vya maji kwenye mabwawa ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chini ya Mpango wa *FRP*, imetayarishwa Programu ya Uwekezaji *(Capital Investment Program – CIP)* inayolenga kuboresha na kupanua miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na huduma nyingine za umeme itakayogharimu takriban shilingi trilioni 1.6. Serikali itashirikiana na Washirika wa Maendeleo, taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi, sekta binafsi na *TANESCO* katika kupata fedha stahiki ili kufanikisha utekelezaji wa Programu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ndiyo yenye majukumu ya msingi ya kuvutia, kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa umeme vijijini na ndilo chimbuko la kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Agency-REA)* pamoja na Mfuko wa Nishati Vijijini *(Rural Energy Fund – REF). TANESCO* itaendelea kushiriki kupeleka umeme vijijini kama ilivyokuwa awali isipokuwa katika mazingira mapya. *TANESCO* itashiriki katika miradi isiyo na mvuto ya kibiashara, baada ya kupewa ruzuku kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini kulingana na taratibu zilizopo. *TANESCO* itashiriki moja kwa moja katika miradi yenye faida kibiashara. Mahitaji ya fedha kwa sasa kuhusu uendelezaji wa miradi ya umeme vijijini yanazidi kiasi cha shilingi trilioni 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kuna wazalishaji binafsi wanaozalisha umeme kwa ajili ya mahitaji yao. Miongoni mwa vituo vinavyozalisha umeme kutoka sekta binafsi ni kama vifuatavyo:- Kitai na Peramiho (Ruvuma); Nyangao (Lindi); Ndanda (Mtwara); Isoko na Rungwe (Mbeya); Uwemba, Bulongwa, Ikonda, Mavunga, Lugarawa, Imivaha *Convent*, Uwemba *Mission*, Matembwe, Kisinga *Mission*, Maduda na *TanWatt* (Iringa), Kaengesa (Rukwa), Ngaresero (Arusha), Sakare (Tanga), Ndolage (Kagera), na Kilombero *Sugar Company* (Morogoro). Vituo vyote hivi vina uwezo wa kuzalisha zaidi ya megawati 10.

Baadhi ya vituo hivi vina uwezo wa kuzalisha na kusambaza umeme kwenye vijiji vya jirani lakini vinashindwa kufanya hivyo kutokana na kutokuwepo mwongozo katika sheria ya sasa. Aidha, kuna wawekezaji binafsi ambao wameonesha nia ya kuzalisha umeme kwa mtindo huu wanaosubiri mwongozo wa sheria, kwa mfano, kampuni ya *Sao Hill* iliyoko Mkoani Iringa ambayo ina uwezo wa kuzalisha hadi megawati 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Kabambe wa kuendeleza Sekta ya Umeme (*Power System Master Plan - PSMP)* unaweka dira ya kuendeleza sekta ya umeme kwa kipindi cha miaka 25 (2007-2031) kulingana na matakwa ya Sera ya Nishati ili kukidhi mahitaji ya umeme ya nchi kwa kipindi kirefu na kwa gharama nafuu kwenye uchumi wa nchi yetu. Uandaaji wa *PSMP* unazingatia hatua zifuatazo:-

(i) Kuainisha ukuaji wa mahitaji ya umeme nchini kwa kipindi kirefu (*load forecast*).

(ii) Kuainisha hali halisi ya kihaidrolojia kwa kutumia takwimu za kipindi kirefu cha nyuma *(hydrological study).*

(iii) Kuainisha miradi ya kuzalisha umeme ambayo imefanyiwa upembuzi yakinifu.

(iv) Kushindanisha miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali na teknolojia tofauti kwa kuzingatia mahitaji ya kutunza mazingira.

(v) Kuzingatia sera za sekta na maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *PSMP* uliandaliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1985 na umekuwa ukidurusiwa kwa vipindi mbalimbali kulingana na uzito wa matukio muhimu ya kiuchumi na kijamii. Rasimu ya Ripoti ya *PSMP* inatayarishwa na itawasilishwa Serikalini mwishoni mwa mwezi Aprili, 2008. Warsha ya wadau imepangwa kufanyika ili kuwapatia fursa ya kuipitia kabla ya Serikali kuiridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa, biashara ya umeme inasimamiwa na Sheria ya Umeme (Sura ya 131) ya mwaka 1931, kama ilivyokuwa ikirekebishwa. Sheria ya Umeme ya sasa ni moja kati ya sheria za zamani sana nchini, ina umri wa miaka 76. Sheria hiyo Ilitungwa kusimamia biashara ya umeme katika sekta iliyokuwa changa na yenye washiriki wachache waliokuwa wanahudumia maeneo madogo madogo. Ili kukidhi mahitaji mapya yanayotokana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii, Sheria hii imefanyiwa marekebisho mara kumi na moja kati ya mwaka 1931 na 2001. Hata hivyo, marekebisho hayo hayakuweza kukidhi mahitaji yaliyotokana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kijamii yaliyoanza miaka ya 1980, hivyo kuwepo umuhimu wa kutungwa kwa Sheria mpya ya Umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya sasa inayosimamia masuala ya umeme nchini ina upungufu ufuatao:-

(i) Sheria ya sasa inakinzana na sheria nyingi nyingine husika *(conflict with other applicable laws)* na ina taswira ya kutofautiana na sera inayoongoza maendeleo ya sekta ya umeme. Kwa mfano, Kifungu cha 7 (2) cha Sheria ya sasa ya Umeme kinazuia kampuni mpya kushindana kutoa huduma ya kusambaza umeme kwa wateja katika maeneo ambayo yamekwishatolewa leseni. Hali hii inakinzana na malengo na matarajio ya sera za nchi za kujenga uchumi imara kwa kutambua ushirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi. Pamoja na kukinzana na baadhi ya Sheria kama vile Sheria ya Ushindani wa Haki ya Mwaka 2003 (*Fair Competition Act, 2003)* na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ya Mwaka 2001 (*Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act, 2001).*

(ii) Sheria iliyopo sasa haiainishi majukumu ya wadau wapya katika sekta ya umeme kama vile *EWURA*, *REA* na Baraza la Ushindani wa Haki *(FCT)*. Sheria mpya itawatambua wadau wapya wa sekta na majukumu yao kama yalivyoainishwa katika Sheria zilizounda vyombo hivyo.

(iii) Sheria ya sasa haina masharti yanayoainisha kwa kina uwepo wa *EWURA* kama mdhibiti mkuu wa maendeleo ya sekta ya umeme. *EWURA* inakosa nguvu za sheria ya sekta ya umeme kuiwezesha kufanya kazi zake ipasavyo.

(iv) Sheria ya sasa inatoa madaraka kwa *TANESCO* kupandisha bei za umeme hadi asilimia kumi (10%) kwa mwaka kwa kutangaza kwenye Gazeti la Serikali. Kiwango zaidi ya hapo kilihitaji ridhaa ya Waziri anayeshughulika na masuala ya umeme. Utaratibu huu unapingana na Sheria ya *EWURA* ambayo inatoa utaratibu na mchakato wa kupandisha bei za umeme kwa kushirikisha wadau wote, na unaziba mwanya kwa *TANESCO* kupandisha bei za umeme bila kupata ridhaa ya mdhibiti mkuu.

(v) Viwango vya adhabu vilivyopo katika Sheria ya sasa havikidhi madhumuni yaliyokusudiwa na vimepitwa na wakati. Kwa mfano, vifungu vya 73 na 74 vya sheria ya sasa vinaelekeza kuwa iwapo huduma ya umeme itakatishwa bila taarifa, kampuni husika itatozwa faini isiyozidi shillingi 500 kwa kila siku ambayo huduma itakuwa imekatishwa.

(vi) Sheria bado inawatambua wadau muhimu wa zamani wa sekta ambao wengine uwepo wao ulikwishafutwa kisheria.

Kwa mfano, *Postmaster General* wa iliyokuwa Tanzania *Posts and Telecommunication Corporation (TPTC)* ambaye uwepo wake ulikoma mwaka 1994 na *Commissioner for Lands and Surveys* wa Wizara ya Ardhi ambaye naye kisheria hayupo tena.

(vii) Ushirikiano wa Kikanda katika biashara ya umeme haujaainishwa katika sheria ya sasa na hivyo kukosa mwongozo wenye nguvu za kisheria katika kusimamia masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya nishati ni gurudumu la maendeleo ya kiuchumi na kijamii la nchi. Sekta ya nishati inahitaji rasilimali fedha nyingi ambazo Serikali peke yake haiwezi kuzimudu. Hivyo, Serikali imekuwa ikiomba misaada mingi kutoka kwa washirika wetu wa maendeleo.

Mheshimwiwa Spika, leo hii tunawasilisha Muswada huu mbele ya Bunge lako Tukufu tukiwa tumezingatia maoni ya Kamati inayosimamia sekta hii na Waheshimiwa Wabunge waliyoyatatoa wakati wa Semina zilizofanyika Dodoma Februari, 2008 na Dar es Salaam Machi, 2008 pamoja na maoni ya wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umezingatia mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Sera ya Taifa ya Nishati ya mwaka 2003 imezingatiwa kwa kuainisha wajibu na majukumu ya watendaji.

(ii) Kuainisha shughuli zote muhimu za masuala ya umeme.

(iii) Kuweka taratibu za usajili na utoaji wa leseni za kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme pamoja na taratibu za kufuata ili kupata usajili na haki ya kukata rufaa.

(iv) Kuweka taratibu za ukusanyaji na utoaji wa taarifa na takwimu za shughuli na masuala ya umeme.

(v)Kuainisha makosa na adhabu mbalimbali zitakazotolewa pindi ukiukwaji wa Sheria inayopendekezwa utakapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mambo muhimu yaliyojumuishwa kwenye Muswada huu, Muswada umegawanyika katika sehemu kuu kumi.

Sehemu ya Kwanza, inahusu masharti ya jumla yanayojumuisha jina la Sheria, kuanza kutumika, na tafsiri ya baadhi ya maneno na misemo muhimu iliyotumika katika Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Pili, inahusu masuala ya utawala. Sehemu hii ina vifungu vinavyoainisha kazi na mamlaka ya Waziri, na kazi na mamlaka ya mdhibiti mkuu wa biashara hii, kwa maana ya *EWURA*.

Sehemu ya Tatu, inahusu usimamizi wa Sekta ya Umeme ambayo inajumuisha masuala ya leseni za muda, leseni za kawaida, haki na wajibu wa wamiliki leseni. Mojawapo ya masharti ya leseni zitakazotolewa chini ya sehemu hii ni kumtaka mwekezaji/mtoa huduma kutoa taarifa *(notice)* kwa Mdhibiti *(EWURA)* isiyopungua mwaka mmoja endapo atakuwa na nia ya kutohuisha *(renew)* leseni yake. Kipindi hiki kitaiwezesha *EWURA* kusimamia vizuri suala la hatima ya miundombinu atakayokuwa amewekeza na uhifadhi wa mazingira. Sharti jingine katika sehemu hii ni kutoziruhusu kampuni zenye leseni kubadilisha umiliki *(transfer/assignment)* bila ya idhini ya maandishi itakayotolewa na Mdhibiti *(EWURA)*. *(Makofi)*

Sehemu ya Nne inaainisha masuala yanayohusu kodi na ushuru. Sehemu hii pia ina masharti yanayohusu haki na kinga kwa mteja.

Sehemu ya Tano inaweka masharti yanayohusu uperembaji, ukaguzi, uchunguzi na utekelezaji wa masharti mbalimbali yanayohusiana na Sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya Sita inahusu upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekaji wa mindombinu ya usambazaji wa umeme.

Sehemu ya Saba inaainisha masuala yanayohusu usambazaji umeme vijijini ambayo inampa Waziri Mamlaka ya Udhibiti *(EWURA)* na Wakala wa Nishati Vijijini wajibu wa kutayarisha Mpango na Mikakati ya Usambazaji Umeme Vijijini.

Sehemu hii pia ina vipengele vinavyowapa wawekezaji binafsi majukumu ya kusambaza umeme katika maeneo ya vijijini ambako njia zao za umeme zinapita (Ibara ya 39(4) ya Muswada). Tumeweka sharti hili ili sekta binafsi isaidie moja kwa moja juhudi za Serikali kufikisha huduma ya nishati ya umeme kwa Watanzania takribani asilimia 80 waishio vijijini. *(Makofi)*

Sehemu ya Nane inahusu mabadiliko ya sekta ndogo ya umeme. Sehemu hii ina masharti yanayohusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika sekta ya umeme na mabadiliko ya soko la umeme nchini. Sehemu hii pia ina masharti yanayotoa kipaumbele maalum kwa Shirika la *TANESCO* kuwa na haki ya kutoa huduma kwa watumiaji wakubwa wote wa umeme nchini (Ibara ya 41(6) ya Muswada).

Sehemu ya Tisa inahusu masuala ya utatuzi wa migogoro. Sehemu hii inaweka masharti ya utatuzi wa migogoro na ya ukataji wa rufaa kwenye Baraza la Ushindani wa Haki.

Sehemu ya Kumi inatoa masharti ya jumla ambayo yanajumuisha mamlaka ya Waziri kutengeneza kanuni kwa maana ya *regulations* uwezo wa yeye kutengeneza kanuni kwa maana ya *rules*, masuala yanayohusu kinga kwa wafanyakazi, kufutwa kwa sheria ya umeme ya sasa na masharti ya mpito.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Muswada huu kwanza haulengi kubinafsisha shirika la *TANESCO*, Serikali itaendelea kusaidiana na bodi na uongozi wa *TANESCO* kuhakikisha kwamba shirika linaendelea kuimarika na kuimarisha huduma kwa wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, muswada huu unatoa kipaumbele kwa shirika la *TANESCO* kutuoa huduma kwa watumiaji wakubwa wote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, muswada huu ni utekelezaji wa Sera ya Nishati ya mwaka 2003 ambayo, pamoja na mambo mengine, inatambua ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Muswada huu haukwamishi utekelezaji wa mpango wa usambazaji wa umeme vijijini. Tano, Muswada huu kwa vyovyote vile haukwamishi utekelezaji wa mpango wa usambazaji umeme vijijini. Sita, Muswada huu unatambua nafasi ya Sheria ya Nishati Vijijini *(Rural Energy Act)* ya mwaka 2005, wakala wa Nishati Vijijini na Mfuko wa Nishati Vijijini kupitia ibara za 37, 38 na 39 za muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la Saba Muswada huu unatoa majukumu kwa sekta binafsi kusaidia kwa kasi zaidi mpango wa usambazaji wa umeme vijijini, na nane Muswada huu unalenga kufuta sheria ya umeme ya sasa ya mwaka 1931 ambayo kimsingi na ukweli imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. SAID A. ARFI**: Mwongozo wa Spika! Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate mwongozo kuhusu kifungu namba 56(10)(2), naomba nisome, "hoja au marekebisho au mabadiliko ya hoja yoyote yanahitaji kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua 10." Idadi ya Mawaziri haitimii kuunga mkono hoja hii iliyotolewa, wako saba, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Hoja yenyewe inasema, 56(1): "Mbunge atakapoitwa na Spika kutoa hoja atasimama mahali pake na kutoa hoja yake." Fasili ya (2) inasema: "hoja au mabadiliko ya hoja yoyote yatahitaji kuungwa mkono na wabunge wasiopungua kumi na endapo hayataungwa mkono, hoja au marekebisho ama mabadiliko hayo yatatenguka na Katibu ataweka kumbukumbu kwenye taarifa rasmi kwamba kwa kuwa hoja au marekebisho au mabadiliko hayo hayakuungwa mkono basi hayakujadiliwa. Fasili ya (3) inasema: "Mbunge anaweza kuunga mkono hoja kwa kusimama tu mahali pake bila kusema lolote kuhusu hoja hiyo kisha akakaa, lakini Mbunge aliyefanya hivyo bado atakuwa na haki ya kuizungumzia hoja hiyo".

Sasa hapa inazungumzia Wabunge 10, siyo Mawaziri 10, kwa hiyo, hata Wabunge wengine wangeweza hata kusimama walipo, kwa hiyo, tunaendelea, namwita Mwenyekiti wa Kamati iliyohoji jambo hili. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. WILLIAM SHELUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Muswada wa Sheria ya Umeme wa mwaka 2007 *(The Electricity Bill, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5), Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 *(The Electricity Bill, 2007)"* unaokusudia kufuta Sheria ya Umeme ya mwaka 1931 iliyofanyiwa marekebisho kumi na moja mpaka sasa, pamoja na kuweka masharti ya jumla na mpito wa Sheria iliyofutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba Muswada huu uliwahi kujadiliwa na iliyokuwa Kamati ya Uwekezaji na Biashara na ulitarajiwa kuwasilishwa Bungeni Mwezi Januari 2008. Kutokana na hoja zilizotolewa kwenye Semina ya Wabunge wote tarehe 10 Februari, 2008 hapa Dodoma, Muswada huu haukuwasilishwa. Kwa kutambua umuhimu wa Muswada huu, Kamati yangu iliujadili kwa mara nyingine tena katika Ofisi

Ndogo ya Bunge Dar es Salaam tarehe 3 Aprili, 2008, chini ya Kamati mpya ya Nishati na Madini.

Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa mapendekezo yaliyokusudiwa yaliyowasilishwa na Mheshimiwa William M. Ngeleja (Mb), Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, maoni ya Wadau, Waheshimiwa Wabunge pamoja na maoni ya Kamati katika Muswada huu yamezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuupitia Muswada huu kwa lengo la kuuboresha katika hatua za awali, Kamati iliwaalika Wadau mbalimbali kwa majadiliano ya kina kuhusu Muswada wenyewe. Majadiliano hayo yalisaidia sana kuibua mawazo mapya, maoni na hoja nzuri za kuboresha Muswada huu. Nakiri kuwa maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu ni matokeo ya mchakato huu wa kubadilishana mawazo na Wadau mbalimbali. Napenda kuwashukuru wadau wote ambao waliitikia mwaliko wa Kamati na kuja kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada ulio mbele yetu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, changamoto na hoja mbalimbali zilizojitokeza wakati wa kujadili Muswada huu kupitia Semina iliyoandaliwa na Wizara ya Nishati na Madini na vikao mbalimbali vya Kamati, zimesaidia kwa kiasi kikubwa kufanyika kwa marekebisho makubwa ndani ya Muswada huu.

Aidha, majibu kuhusiana na hoja hizo yaliyotolewa, yamesaidia sana Kamati kupata uelewa na ufafanuzi mzuri. Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Waziri wa Nishati na Madini, Naibu wake, Katibu Mkuu, Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wataalamu wote wa Wizara ya Nishati na Madini, Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*), Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Nishati na Maji (*EWURA*). Wote kwa pamoja walifanya kazi kubwa kufikia hatua ya kuuleta Muswada huu sasa ujadiliwe mbele ya Bunge lako Tukufu. Tunawashukuru kwa dhati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kuweka masharti bora ya usimamizi wa Sekta Ndogo ya Umeme nchini kutokana na mfumo wa biashara huria na changamoto zilizojitokeza hivi karibuni katika kusimamia sekta hiyo. Aidha, Muswada huu utavutia kwa kiasi kikubwa sekta binafsi kuwekeza katika kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme nchini. Zaidi ya hayo, Muswada huu utaiwezesha Serikali kuingiza na kutoa huduma ya umeme ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2003 inatamka wazi juu ya kuiendeleza Sekta ya Nishati ili ikue na kuvutia wawekezaji binafsi kuwekeza katika sekta hii. Sera hii pia inaainisha umuhimu wa kuendeleza vyanzo vya nishati ili kupunguza makali ya bei za umeme. Aidha, Dira yake inaelezea umuhimu wa Sekta ya umeme katika kuchangia kukua kwa uchumi wa nchi.

Changamoto za Sera hii zinasisitiza kukaribisha wawekezaji binafsi kuwekeza katika kuzalisha, kusambaza na kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati yangu kuchambua kwa kina Muswada huu, kutafakari kwa undani Sera ya Nishati ya Taifa ya mwaka 2003 na kubaini upungufu uliopo, Kamati imejiridhisha na kuona umuhimu wa kufutwa kwa Sheria iliyopo na kutunga Sheria mpya itakayoendana na Sera ya Taifa ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, Sheria hii kwa kiasi kikubwa itasimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Nishati na Maji (*EWURA*). Kazi za Mamlaka katika usambazaji wa umeme zimeanishwa kati Kifungu 6(1)(a)-(h).

Pia Mamlaka itasimamia masuala ya Leseni, bei za umeme, haki na wajibu wa wamiliki leseni, kodi na ushuru, haki na kinga kwa wateja, ufuatiliaji, ukaguzi, uchunguzi na utekelezaji wa masharti mbalimbali yanayohusiana na sheria hii. Upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji wa miundombinu ya usambazaji na uzalishaji umeme vijijini yatashughulikiwa na Mamlaka hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Sheria hii mpya, *TANESCO,* Shirika ambalo Serikali inalimiki kwa asilimia mia moja (100%) litaingia katika ushindani wa haki na makampuni mengine yatakayowekeza katika kuzalisha umeme. Marekebisho katika Muswada huu kama yanavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho Ibara ya 41(6) na (7) yamezingatia kwa kiasi kikubwa maslahi ya *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba wateja wa umeme hawapati usumbufu wa aina yoyote pale wanapoamua kununua umeme unaozalishwa na mwekezaji binafsi, Muswada huu umebainisha haki na usalama kwa wateja chini ya Ibara ya 26(1)-(5) na marekebisho ya kuongeza Ibara ndogo ya (6) hadi (8) kama zinavyoonekana kwenye Jedwali la Marekebisho. Hii itasaidia kumfanya mzalishaji wa umeme asitumie nafasi aliyonayo kutekeleza wajibu wake visivyo na hata kutoa huduma isiyoendana na mahitaji ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa awali *TANESCO* ilikuwa ikipata usumbufu wa kupitisha nyaya za umeme katika baadhi ya maeneo kama vile kwenye madaraja, barabara na miundombinu mingine, ni kwa sheria hii sasa kupitia Ibara ya 35(4) kwamba, mwenye leseni ya kuzalisha umeme anaweza kuweka, kuunganisha na kusimamia njia za usambazaji umeme kama vile nyaya za juu, nyaya za chini ya ardhi (*cable*), mabomba ya gesi, maji, mafuta na vifungasho vingine vitakavyothibitishwa na Mamlaka (*EWURA*). Kwa msingi huo Kamati ina maoni kuwa ni vyema Waziri mwenye dhamana akatunga Kanuni itakayomtaka mwekezaji mara baada ya kukamilisha ufungaji wake kuiweka ardhi ya mahali husika katika hali yake ya awali ili kuepukana na madhara ya uharibifu wa mazingira na miundombinu iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 37(2) ya Muswada huu, Waziri mwenye dhamana anatakiwa kupitia Bunge lako Tukufu, kuwasilisha taarifa ya

maendeleo, mafanikio na matatizo ya usambazaji umeme vijijini kupitia Mpango Mkakati wa Umeme Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11(4) ya Muswada huu inamtaka kuwa mwenye leseni kutokuhamisha leseni yake mpaka apate kibali kutoka kwenye Mamlaka (*EWURA*). Mhamishaji leseni atatakiwa kulipa kwenye Mamlaka(*EWURA*) ada *(fee)* ya uhamishaji wa leseni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na malengo mazuri ya Muswada huu, umuhimu wake utaonekana iwapo Wadau wataelimishwa vizuri kuhusu faida za uwekezaji binafsi katika sekta ya umeme kwa maslahi yao na Taifa zima. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa ngazi mbalimbali kuwaelimisha wananchi waelewe vizuri Sheria hii na waipokee ili waweze kufaidika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, Kamati imefarijika na kuwepo kwa Sheria hii. Kwa kuzingatia kuwa Sera ya Taifa ya Nishati (2003) iliyopo, ilikuwa haiendani na Sheria inayofutwa, Kamati inashauri kuwa Sheria Mpya itumike vyema katika kuboresha Sera tuliyonayo ili iweze kukidhi mahitaji ya sasa na wakati ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, biashara yoyote ikiwemo biashara ya umeme, hutegemea mambo mbalimbali zikiwemo gharama za uzalishaji, manunuzi, na nyinginezo. Kamati inashauri kwamba, kwa kupitia Mamlaka (*EWURA*) uwepo usimamizi makini wa Ibara 25(3)(d) ya Muswada huu inayohusu kupanga bei za umeme ili ziendane na uwiano wa vyanzo vya uzalishaji wa nishati husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa elimu kuhusu matumizi ya umeme ni muhimu kwa wananchi, hivyo Kamati inasisitiza kuwa Ibara ya 29(3) ya Muswada huu isimamiwe ipasavyo na Mamlaka ili kuepuka athari zitokanazo na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia kilio cha wananchi kuhusiana na gharama ambazo Taifa limekuwa likiingia kulipia gharama ya uwezo wa ukodishaji wa mitambo *(capacity charges)* kupitia mikataba ya umeme iliyopo. Kwa sheria hii mpya, wawekezaji watakaoingia ni kwa hiari yao wenyewe na hivyo gharama za *capacity charge* hazitakuwepo. Aidha, Ibara ya 41, Ibara ndogo mpya ya (7) kwenye Jedwali la Marekebisho inatoa sharti kwa wawekezaji waliopo sasa kutoruhusiwa kujiingiza katika kutumia sheria hii mpya baada ya kumalizika kwa mikataba yao. Wawekezaji hao watatakiwa kukaa kwa kipindi cha miaka mitano ndipo waombe leseni mpya chini ya Sheria hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 41(6) kwenye Jedwali la Marekebisho, Kamati yangu inapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba chini ya Sheria hii mpya *TANESCO* itapewa kipaumbele katika miradi mikubwa ya uzalishaji na usambazaji wa umeme. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuiandaa vyema *TANESCO* ili kuiwezesha kutekeleza azma hiyo. Maandalizi hayo yahusishe kukamilisha haraka

mipango yake ambayo ni pamoja na Mpango Mkakati ambao unahusu kuiimarisha kifedha (*Power System Master Plan)* na *Financial Recovery Plan.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kusimamia na kudhibiti rasilimali zilizopo nchini kama vile gesi, makaa ya mawe, mafuta, maji, nishati taka, nishati ya mimea na kadhalika. Rasilimali hizi zisimamiwe ipasavyo na zitumike kuongeza uzalishaji wa umeme wa bei nafuu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa gesi unaoendelea hivi sasa katika baadhi ya maeneo, umiliki na uendeshaji wake haupo wazi. Hii ni kutokana na kutokuwepo kwa Sheria ya Nishati ya Gesi. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba inaleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Nishati ya Gesi ili uweze kupitishwa na Bunge. Sheria hiyo ya gesi itasaidia kuweka misingi na taratibu bora katika kutafuta na kutumia ipasavyo gesi inayopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilitafakari kwa undani Ibara ya 19(1) inayotamka kuhusu muda wa leseni. Tafakari hiyo ilikuja kutokana na kubaini kwamba endapo atatokea mwekezaji ambaye ataamua kutoendelea *(renew)* na leseni yake na kuamua kutoa miundombinu ambayo atakuwa ameiwekeza tayari na kuhamishia sehemu nyingine.

Kamati inashauri kuwa Mamlaka iandae Kanuni zitakazozingatia na kuweka masharti ya kumtaka mwenye leseni kabla ya kufikia uamuzi huo atoe taarifa *(notice)* ya muda usiopungua miezi 12 ili kutoa nafasi kwa wateja wake kujiandaa kufanya maamuzi mengine na kuiwezesha Mamlaka (*EWURA*) kuangalia jinsi ya kuendeleza uwekezaji uliokwishafanywa. Aidha, Ibara ya 11(1) na (4) ya Muswada huu itekelezwe kwa makini ili masharti hayo yatamke mwenye leseni ya miundombinu atumie Ibara ya 11(1) na (4) ya Muswada huu kuhamisha leseni yake kwa mwekezaji mwingine anayetambulika kuwa na uwezo wa kifedha, utaalam na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kwamba suala la ajira kwenye maeneo ya uwekezaji katika Sekta ya Nishati liangaliwe kwa jicho kali lizingatiwe sambamba na Sheria ya Kazi na Ajira kwa Wageni ya mwaka 2004. Kamati inatamka hivi kwa sababu yamejitokeza matukio katika utafutaji wa gesi, mafuta hapa nchini ambapo watu wenye ujuzi *(skilled labour)* hawaajiriwi na makampuni yanayohusika kuajiri wageni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) amewekewa vyanzo finyu vya mapato. Kamati inaishauri Serikali kuviangalia upya vyanzo hivyo. Waziri mwenye dhamana aandae Kanuni ambazo zitatamka wazi namna ambavyo wawekezaji watakavyochangia katika mapato ya *REA*. Aidha, asilimia 5% iliyowekwa kwenye Sheria ya *REA* ni ndogo mno hivyo Kamati inashauri Serikali kuongeza kiwango hiki kufikia asilimia 10% ili kuiwezesha *REA* kutekeleza majukumu yake ya kupeleka umeme vijijini kwa kasi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza awali, Muswada huu ulikuwa na changamoto nyingi hasa ikizingatiwa kuwa Bunge limetoka kwenye kipindi cha mpito cha sakata la *Richmond*. Hoja mbalimbali zilijitokeza kupitia vikao vya Kamati na Semina zilifanyiwa kazi ipasavyo na Wizara ya Nishati na Madini. Hadi kufikia hatua hii kazi kubwa imefanyika na tunashukuru sana. Jedwali la Marekebisho lililopo mbele ya Bunge lako Tukufu lina marekebisho mengi ambayo yametokana na ushauri wa Kamati na yameridhiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashukuru kuona kuwa Wizara ilizingatia na kupokea ushauri wa Kamati moja kwa moja wakati wa mchakato wa kuchambua na kujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Muswada ulio mbele yetu. Pia nimshukuru Mheshimiwa William M. Ngeleja, (Mb.), Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake, Mheshimiwa Adam K. Malima, (Mb.), kwa ushirikiano wa dhati walioutoa wakati wa kuwasilisha Muswada huu kwenye Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu Arthur Mwakapugi, Wataalamu wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Nishati na Maji (*EWURA*), Ndugu Haruna Masebo, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*) Dk. Idris Rashid, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini(*REA*), Dk. Lutengano Mwakahesya na Wataalamu wote kutoka Wizara ya Nishati na Madini, *EWURA* na *TANESCO,* kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipokutana kuujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hii kuwashukuru wajumbe wa Kamati hii kwa michango yao ya kina iliyouboresha Muswada huu.

Naomba niwatambue kama ifuatavyo**:-** Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Faida M. Bakar, Mheshimiwa Samuel M. Chitalilo, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Halima M. Mamuya, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Rita Louis Mlaki, Mheshimiwa Mohammed H. J. Mnyaa, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Dk. James A. Msekela, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Mohammed S. Sinani na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Wabunge ambao si Wajumbe wa Kamati walishirikiana nasi vyema katika kuuchambua Muswada huu kwenye Kamati, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunamshukuru Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashillilah na Ofisi yake kwa kuwezesha Kamati yetu kufanya kazi bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba niwashukuru Makatibu wa Kamati yetu, Ndugu Lina Kitosi na Ndugu Emmanuel Mpanda kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuhudumia Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Muswada huu, na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tunakushukuru kwa kuwasilisha. Sasa nitamwita msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mnyaa, ndiyo maana Mama alikuja kukusikiliza jinsi unavyotoa vitu. (*Kicheko*)

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UMEME WA MWAKA 2007:** Mheshimiwa Naibu Spika,napenda kutoa shukrani zangu za dhati na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu za kutuwezesha kuendelea kuwatumikia wananchi. Aidha, natoa shukrani zangu kwako kwa ushirikiano na Kambi ya Upinzani Bungeni katika kutimiza majukumu yetu kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la 2007, Kanuni ya 53 (6)(c) na 86(6), naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Umeme wa Mwaka 2007 *(The Electricity Bill, 2007).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikiri kwamba muswada huu umefanyiwa marekebisho mengi baada ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge katika semina mbili tofauti pamoja na wadau kutoka katika taasisi mbalimbali. Kutokana na hoja hizo muswada huu umeboreshwa tofauti na ulivyokuwa hapo mwanzoni. Hata hivyo, napenda kutoa dukuduku langu na ushauri unaohusika katika vifungu ambavyo Kambi ya Upinzani haijaridhishwa navyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda napenda kwenda moja kwa moja kwenye vifungu ambavyo Kambi ya Upinzani ina wasiwasi navyo na kuliomba Bunge lako Tukufu pamoja na Wizara husika kuvifikiria kwa makini zaidi na baadae kuvifanyia marekebisho kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia kwenye tafsiri ya maneno katika Jedwali la Marekebisho, Sehemu C, Kifungu cha 3, maneno, *low voltage* na *high voltage* katika mstari wa pili kabla ya neno "*plus*" kwa kila tafsiri kuna neno *volts/voltage* linakosekana. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwekwa kwa neno hilo ambalo tuna uhakika limesahaulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 4(1)(g) kinampa mamlaka Mheshimiwa Waziri kutengeneza kanuni kuhusu kununua na kuuza umeme nje ya nchi, Kambi ya Upinzani inasema, kutengeneza sera ambapo umeme unaweza kuagizwa kutoka nje ya

nchi (*imports*) au kusafirishwa kwa kuuzwa (*exports*) iwe ni kazi ya Mamlaka na sio kazi ya Mheshimiwa Waziri.

Hii ni kwa kuangalia kuwa japokuwa Serikali ni moja lakini kwa uzoefu uliopo kumekuwa na maamuzi ambayo yanapingana, lakini Mamlaka ipo pale na muda wote kazi zake ndiyo kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nyingine ni kwamba Mamlaka ndiyo yenye dhamana ya ku-*regulate* bei kwa makampuni yote nchini hivyo hata hizo kanuni zitengenezwe na mamlaka yenyewe. Waziri apunguziwe kazi, na hivyo yeye atoe idhini na mwongozo wa lini zianze kutumika rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5(d) kinachosema kuwa Mamlaka ndiyo itakuwa na uwezo wa Uthibitisho wa manunuzi kwa ajili ya mitambo mipya ya kuzalisha na kusambaza umeme au kusafirisha, Kambi ya Upinzani ina uhakika kuwa Mamlaka inayozungumzwa katika muswada huu ni *EWURA*, Je, *PPRA* inawekwa wapi? Ingekuwa vyema na *PPRA* ikatamkwa bayana majukumu yake ya msingi au washirikiane na *EWURA* ili kuepuka Mamlaka kupinga uamuzi wa *PPRA* kama tulivyoona kwa *Richmond.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6(1)(b) nanukuu: " *promote access to, and affordability of electricity services particularly in rural areas.*" Kwa mujibu wa muswada huu, hii ni moja ya kazi za Mamlaka. Lakini kifungu hiki hasa kinahusu Wakala wa Nishati Vijijini kwani wao ndio wenye jukumu la kufanya upembuzi yakinifu kuona kama vipato halisi vya wananchi wa vijijini vinalingana kwa udogo au la ili waweze kupatiwa umeme kutokana na gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 8(1)(f) kinachohusu shughuli zitakazohitajika kukatiwa leseni, nanukuu: **"***cross border trade in electricity,***"** Kambi ya Upinzani inaona hili ni kosa kubwa kwani endapo atatokea mwekezaji ambaye kwa urahisi wake amewekeza mashine za uzalishaji umeme kandokando mwa mipaka ya Tanzania, hivyo itakuwa kwake yeye ni rahisi kupelekea umeme nchi jirani na kufanya biashara. Muswada huu hauna kipengele kinachosema sharti la kwanza kabla ya kuuza nje, Tanzania iwe imejitosheleza kwa angalau asilimia zaidi ya 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu hautakuwa na maana ikiwa watajitokeza wazalishaji umeme ambao watajali zaidi kutengeneza faida yao kuliko kuangalia mahitaji halisi ya nchi. Hivyo basi, watauza umeme nje ya nchi wakati idadi kubwa ya Watanzania iko gizani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 11 kinachohusu "*transfer of license,***"** Kambi ya Upinzani inatoa angaliazo kwa Serikali kuhusiana na kifungu hiki kuwa kwa kuwa tumepata uzoefu kupitia *Richmond* na *Dowans* na lengo ni kupata wawekezaji makini, hivyo basi kifungu hiki kinatoa mwanya kwa wawekezaji wababaishaji na matapeli kuingia nchini na kuacha wawekezaji makini. Kama mwekezaji ameshindwa ni bora anyang'anywe leseni badala ya kuhamisha umiliki.

Hii ni kufanya biashara ndani ya biashara. Je, ni mara ngapi uhaulishwaji huu unaweza kufanyika? Hapajaelezwa, pamoja na utaratibu uliowekwa kupitia Mamlaka lakini bado hatujakuwa na uhakika kwa asilimia 100 kuwa watendaji wetu ni wazalendo kwa kiwango gani. Aidha, kifungu kinasema ku-*transfer License* tu, Kambi ya Upinzani inataka kuelewa kuhusu *"transfer of liabilities"* Muswada huu unasema nini au unaweka utaratibu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 12(6) kuhusu *Provisional Licence* kuhaulishwa haina haja kwa sababu inatoa nafasi kwa wawekezaji matapeli kuingia kwenye ushindani bila sababu, Kambi ya Upinzani inatoa sababu zile zile kama zilizotolewa kwenye kifungu cha 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 13(b) kinachosema kuhusu haki za mwenye leseni, ku-*plan, develop, install, maintain and refurbish the facilities and equipment required to undertake licensed activities",* Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki kina walakini kwani *Planning and Development* ya aina yoyote lazima iendane na *Power System Master Plan* ya nchi.

Hivyo basi tunaona kifungu hicho kingeweka wazi kuwa *Planning* na *development* za *individual companies* zisiende kinyume na mipango ya nchi badala yake ziende kwa kufuatana na *National Power System Master Plan*, ambayo hadi hivi leo unawasilishwa Muswada huu *Master Plan* hiyo haijawasilishwa Bungeni kama ilivyoshauriwa katika taarifa ya mwaka 2006 ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 14(5)(c) kinachosema, nanukuu: *"employ a sufficient number of qualified personnel to ensure compliance with the licence terms",* Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke utaratibu wa kuwa kwanza Watanzania wenye sifa wapewe kipaumbele kabla ya wageni. Hili liwekwe wazi vinginevyo wageni ndio watakaokuwa wanapewa umuhimu wa kwanza na sheria hii itakuwa ni kuwatafutia ajira watu wa nje zaidi kuliko Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kuwa kuna sheria mama ya kazi, Sheria ya Uhamiaji na Sheria ya Uwekezaji lakini pamoja na kuwepo kwa sheria hizo bado matatizo ya wageni kuchukua nafasi zote za kitaaluma (*skilled technicians),* mafundi wazoefu au wafanyakazi wazoefu wenye fani husika, na kuwaacha wanataaluma wetu bila kazi ni kubwa na kuna mifano mingi, mmoja wapo ni ule wa wafanyakazi wa makampuni ya mafuta *(OILOT)* vitengo vya *RIGS* ambao wameachwa na kampuni kuajiri watu kutoka nchi za jirani.

Jitihada zao za kuona viongozi wa Wizara husika hazijafua dafu pia wameweza kuwasilisha malalamiko yao kwa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini hapo tarehe 4 Aprili, 2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15(8) kinasomeka, nanukuu: ***"…….**liable to a fine not exceeding four million…………,**"*** Kambi ya Upinzani inaona hapa adhabu inayotolewa hailingani na makosa yaliyoainishwa, hivyo basi ingesomeka kuwa: *"…Should not be less than four million"*. Aidha, adhabu hiyo ya faini iende sambamba na kifungo kwa kipindi kilichotajwa na kifungu hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18(4) kinacho mtaka mtu yeyote atakayezalisha umeme chini ya megawati moja kuwa asifuate masharti yaliyoorodheshwa kwenye kifungu cha (8) cha Muswada huu, Kambi ya Upinzani inaona kuwa hili ni jambo la kushangaza sana kwani mzalishaji huyo atakuwa na uwezo mkubwa sana wa kufanya biashara bila ya leseni. Aidha, inaonyesha kuwa wataalamu wa Wizara hii wameshindwa kuona umuhimu au ukubwa wa umeme wa megawati moja ambao unaweza kutumiwa na takriban nyumba zaidi ya 300 kwa matumizi ya kijijini au wamechukua vigezo vya India ambao wao ni *sub-continent* na ni tofauti na hali yetu ya Kitanzania. Hivyo tunataka kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na kifuate masharti yaliyomo kwenye kifungu cha (8).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu hiki kiwape unafuu *(exemption)* kwa wale Watanzania watakaozalisha umeme usiozidi 50 *KW*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 19, muda wa leseni *(duration of the license),* ambacho kimetoa fursa ya ku-*renew license* lakini hakitoi fursa au maelezo yoyote iwapo mwekezaji hataki tena kuendelea kuwekeza nchini na anahitaji kuondoka. Muswada huu umekaa kimya kuhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata kama suala hili litawekewa katika masharti ya leseni bado haitoshi hata kidogo kwa kuzingatia kwamba uwekezaji wa namna hii unajumuisha mitambo au miundombinu yenye gharama kubwa sana, na kwamba baada ya kubakia katika *service* na wananchi kuzoea huduma hiyo, siyo rahisi kwa mwananchi kuona mwekezaji anang'oa mitambo yake na kuhamishia nchi nyingine. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri suala hili liwemo katika sheria na iainishwe waziwazi kwamba kwa mwekezaji aliyewekeza kwa muda usiopungua miaka 20 na hahitaji ku-*renew license* yake asiruhusiwe kung'oa mitambo au miundombinu aliyoiweka. Katika kipindi hicho atakuwa amekwisha jilipa gharama zake zote za uwekezaji *(Investment costs),* au hata kama amedumu kwa miaka mitano na kuamua kuondoka na mitambo yake muswada huu haujasema chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 20(1) kinachomhusu huyu mtu anayepewa kazi ya kuwa "*System Operator*" kwa majukumu anayopewa mtu huyo, Kambi ya Upinzani inaona ni majukumu yanayohitaji vifaa vya kisasa na vyenye uwezo wa kuingilia kati mzunguko wa umeme kati ya gridi na mteja. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaona kuwa kazi hii si ya mtu kuomba na kupewa kama Muswada unavyosema bali ni ya mtu/kampuni kuipata kwa njia ya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 20 (2) kinahusu *System Operator* kutengeneza na kutangaza *(Power System Expansion Plan)* mpango wa utanuzi wa umeme. Hii si kazi ya kumpatia mtu ambaye ameomba kuwa *system operator* bali ni malengo mahususi ya nchi ambayo yanatakiwa yawemo kwenye *Power System Master Plan* ambayo inatakiwa isimamiwe na mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, Kifungu cha 22(1) *(cross border licenses)*, Kambi ya Upinzani inaitaka Mamlaka kutengeneza Kanuni au utaratibu maalumu kuwa na vifaa madhubuti vya kupimia bila udanganyifu wa aina yoyote idadi ya umeme unaoingia au unaotoka nje ya nchi pamoja na upotevu wake wa aina zote *(Energy imported or exported with all types of power losses)*. Hii inaweza kufananishwa na *"Flow Meter"* za kupimia mafuta yanayoingizwa nchini pale Kurasini zilivyokuwa zinatumika kuikosesha nchi mapato. Na hilo ni fundisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, ikiwa marekebisho hayo yatafanywa, sioni kwa nini nisiunge mkono Muswada huu. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa kuwasilisha vizuri. Waheshimiwa Wabunge, orodha ya wachangiaji wamefika 50. Sasa ninachorajibu kutaka kuelewa ni moja, mkisoma maudhui ya Sheria kabisa kabisa sielewi nyinyi 50 mnataka nini? Lakini ukienda kwa haraka haraka mtaanza kuomba umeme vijijini kwenu, sijui kwangu, kikaenda huku, hayo atakayekuwa amekaa Mezani hapa atawaambia siyo. Maana yake naona ndiyo mchezo wenyewe huo. Sasa watu 50 mnataka kuchangia nini? *(Kicheko/Makofi)*

Haya kwa vyovyote vile tutaendelea na Muswada huu leo na Jumatatu. Kwa hiyo, ninamwita mchangiaji wangu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, akifuatiwa na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri kwa muda tulionao na naomba aanze Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa sababu atakaa Mezani. Kwa hiyo, atakuwa msemaji wa kwanza. Halafu na hiyo orodha niliyosema, Mheshimiwa Jenista Mhagama!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa ya kuweza kuchangia Muswada huu ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niipongeze sana Serikali kwa kutuletea Muswada huu. Niseme kwamba Muswada ulibeba mazingira ya namna tofauti katika kuuandaa. Lakini leo unapokuja katika Bunge lako Tukufu, naomba niseme

Muswada huu umefika katika wakati muafaka na sisi tunajua na kutambua umuhimu wa Muswada huu katika kuhakikisha umeme unawafikia wananchi wetu na hasa walioko vijijini. Naomba niipongeze Serikali na ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba marekebisho yaliojionyesha kwenye Jedwali yameonyesha na kudhihirisha wazi kwamba Serikali imekubali ushauri kwa kiasi cha kutosha na kuzingatia matakwa ya wananchi wa Tanzania katika kuhakikisha tatizo hili la umeme linaweza kutatuliwa katika nchi yetu ya Tanzania tukizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi na mpango halisi uliowekwa na Serikali yetu wa maendeleo ya umeme katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kuupitia Muswada wenyewe, nimefurahi sana kuona kwamba Muswada huu umebainisha dhahiri kwamba sasa tunapotunga Sheria itasaidia sana katika azima nzima na kilio cha wananchi cha siku nyingi kuhakikisha kuwa bei za umeme katika nchi yetu ya Tanzania sasa zitakuwa na usimamizi yakinifu na ili Watanzania waweze kugawiwa umeme na kupata umeme katika bei inayoendana na wakati tulionao na sio bei holela zinazopanda na kushuka kama homa za vipindi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana Muswada huu umejikita katika kutoa maelekezo, pamoja na kwamba tunataka sasa kufanya sekta hii ya umeme iwe sekta pia inayohusishwa na ubinafsishaji. Ninasema kwamba ni wakati muafaka kabisa. Tumeona ni namna gani tulivyoingia katika mifumo ya ushindani kwenye sekta nyingine katika nchi yetu ya Tanzania na mafanikio yamekuwa makubwa sana. Naamini kabisa sekta hii ya umeme ikiingia katika suala zima la ushindani lakini ikasimamiwa sawa sawa sina shaka sasa wananchi wa nchi yetu wataweza kupatiwa umeme. Lakini naomba sana *EWURA* iangalie suala la msingi la utoaji wa leseni na hasa kwa wawekezaji binafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu gani? Mara nyingi tumejifunza tunapoingia katika biashara hii huria mara zote wawekezaji wetu wamekuwa na tabia ya kujikita maeneo ya kutoa huduma mbalimbali bila kuangalia usawa wa kimaendeleo katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotegemea katika suala zima la utoaji wa leseni kwenye biashara hii mpya na sheria tunayoiunda mpya ya kusimamia uwekezaji katika sekta ya umeme ningeomba sana *EWURA* ianze kutoa leseni kwa wawekezaji ambao watakuwa na *interest* ya kuwekeza katika umeme maeneo ya vijijini na siyo maeneo ya mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika Shirika letu la *TANESCO* likiwezeshwa vizuri kama inavyojieleza kwenye Muswada wenyewe, litafanya kazi nzuri sana katika Makao Makuu ya Wilaya, katika miji yetu midogo lakini pia katika miji yetu mikubwa na wawekezaji wakiongeza nguvu kule vijijini kwa kusaidiana pia na *TANESCO* tutafika. Nina imani tutafika lakini usimamizi uangaliwe na iwe ni kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 37(2) inamtaka Waziri mwenye dhamana kutoa taarifa ya maendeleo na mafanikio na matatizo ya usambazaji wa umeme hasa vijijini. Sheria hii imeweka kitu cha msingi sana. Hapo ndipo tunapoona uwajibikaji wa Serikali na kwa kweli tunakuomba Mheshimiwa Waziri kifungu hiki sisi kama Wabunge tutakitumia sana kukuhoji na kujua ni namna gani kwa Sheria hii tunayoipitisha leo wananchi wa vijijini wataweza kufanikiwa na kupatiwa umeme kama vile kile kifungu kidogo cha pili kinavyoeleza.

Tuna tatizo kubwa sana na wewe unafahamu Mheshimiwa Waziri hata mimi ni miongoni mwa watu ambao nimekuwa nikililia sana Sheria hii ipite na kifungu hiki kiwemo ili niweze kukuhoji umeme kule Muhukuru, Peramiho, Madawa, Uwino, Mahanje na maeneo mengine unafanya nini na wawekezaji hao watafanya nini kwa sababu tunavyo vyanzo vya maji. Tunao uwezo wa kuwekeza katika maeneo mengine ili kuhakikisha kwamba umeme unafika huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuamua kuweka kifungu hiki cha 37 na hasa kile kifungu kidogo cha 2 ambacho kitawapa nafasi Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla kuweza kuhakikisha kwamba Sheria inawalinda wananchi katika kuhakikisha kwamba wanapatiwa umeme kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kifungu cha 11 katika Muswada wetu kinatoa nafasi kwa mwekezaji kuhamisha uwekezaji wake kutoka sehemu moja kwenda eneo lingine. Mimi naomba niunge mkono kwamba kifungu hiki ni kizuri, kwenye suala la umeme ni kifungu kizuri kwa sababu kitatusaidia kuhamisha uwekezaji kutoka eneo lenye wawekezaji wengi na kupeleka maeneo yasiyo na wawekezaji na hasa mikoa ile ya Kusini ambako tumekuwa tukiangalia wawekezaji sana kwenye sekta ya umeme. Lakini nadhani hapa ni mahali muhimu katika kutunga Kanuni. Mheshimiwa Waziri ahakikishe Kanuni hiyo italinda sana maslahi ya Watanzania katika kuhamisha uwekezaji huu. Usiwe uwekezaji holela bali uwe uhamishaji wa uwekezaji makini katika kuleta uwiano wa maendeleo katika sekta ya umeme kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana pia nizungumze kidogo kwenye suala zima la kifungu cha 13(b) kinachosema kuhusu haki za wenye leseni, ku-*plan* na kufanya *development* kutengeneza f*acilities* na *equipment* zozote zile ambazo zinaweza kushughulika na shughuli zao ambazo zitafanyika kwenye sekta nzima hii ya kuwekeza kwenye umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali kwamba ili kuleta ushindani wa uzalishaji na kuongeza viwanda vya kuzalisha vifaa mbalimbali vya kutengeneza umeme katika nchi yetu, kifungu hiki kinaweza kuwasaidia sana wawekezaji kuongeza ushindani wa viwanda katika nchi yetu. Lakini nirejee tena kusisitiza, naomba sana ni lazima Kanuni, na *EWURA* watusaidie kuhakikisha kwamba vifaa hivyo vitakavyotengenezwa viwe ni vifaa thabiti na kweli vinavyoweza kutumika na wananchi bila kuleta madhara na kuleta

athari zozote zile kwa watumiaji wa umeme katika maeneo ambayo vitakuwa vinatumika vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapongeza suala zima la kuangalia mazingira katika suala zima la uwekezaji, Muswada umeeleza vizuri sana. Mazingira hayatunzwi. Tumejifunza kwenye maeneo ya machimbo, mazingira yanaharibiwa sana sana. Kwa hiyo, *installations* zozote zitakazofanyika kama zitakuwa ni *under ground* ama ni kwa namna yoyote, tunaomba kabisa Muswada kama ulivyojieleza mazingira yetu yaendelee kutunzwa na kuthaminiwa kwa kadri itakavyowezekana.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa sana kengele ya pili iweze kugonga na ikanikuta bado nazungumza, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri, niwapongeze na timu nzima. Kwa kweli mchakato huu wa kuleta Muswada mbele yetu umekuwa ni mzito. Naamini sasa huo ndio watakaouchukulia wenzetu katika kusimamia Sheria hii mpya. Nikumbushe tu kwamba wananchi wa Jimbo la Peramiho katika maeneo niliyoyataja wanaendelea kusubiri umeme huu kupitia Sheria hii mpya tunayoipitisha leo. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu hatuna uhaba wa wachangiaji, naomba msiniandikie kuomba kutaka uchangie leo, sijui Jumatatu, hapana! Atakayekuwepo ataitwa, asiyekuwepo na lake halipo. Kwa hiyo, naomba vibarua hivyo muache kabisa, kusema sijui mimi leo naenda wapi. Mimi sina uhaba wa wachangiaji. Kwa hiyo, kama haupo wewe, wengine wapo. Kwa hiyo, naomba hilo tuelewane. Tunaendelea! Sasa nitamwita Mheshimiwa Suleiman Kumchaya na Mheshimiwa Dr. Luka Siyame ajiandaye, akifuatiwa na Mheshimiwa Rwilomba Kabuzi.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ningependa nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu mpya wa Sheria ya Umeme katika nchi yetu. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wale wote ambao wameshiriki katika kutengeneza Muswada huu, wameuleta wakati muafaka, wakati ambao nchi yetu inahitaji mabadiliko makubwa ya uchumi ambayo yatabebwa na upanuaji ama uenezwaji wa umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kutoa mifano kuhusu umuhimu wa umeme katika nchi. Mwaka 1917 nchi ya Urusi ambayo ilikuwa inaitwa *Soviet Union,* kitu cha kwanza kabisa ambacho walifanya ni kuwa na ratiba ama programu ya kueneza umeme katika nchi yao *(Electrification Programme)* ambayo iliwasaidia kujenga viwanda haraka haraka na ndiyo maana vita vyote vilivyotokea vya Kwanza na vya Pili walipokuwa wanapigana walikuwa na uwezo mkubwa wa kuhamisha viwanda na kupeleka katika sehemu nyingine yoyote ile kwa sababu umeme ulikuwa mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wenzetu Wachina walifanya hivyo hivyo, waliweka mbele uenezaji wa umeme katika nchi yao na ndio maana leo hii China imekwishaanza

kupiga *indicator* kwa nchi zilizoendelea kwamba na sisi tunakuja. Lakini kitu ambacho kiliwasukuma ama kinawasukuma ni kusambazwa kwa umeme katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania sasa hivi ni miaka 47 bado kuna maeneo mengine hayana umeme. Muswada huu utasaidia sana katika kupeleka umeme katika maeneo mengine. Kwanza kabla sijafika huko na mimi ningependa kupongeza maana watu wengi walikuwa na wasiwasi kufikiria kwamba kupitishwa kwa Muswada huu ati tunaweza tukaiua *TANESCO*.

Hapa tumeambiwa na Serikali kupitia kwa Waziri kwamba *TANESCO* itaimarishwa na mimi nasema imarisheni *TANESCO* ili iweze kuendelea kufanya kazi ya kusambaza umeme katika nchi yetu. Kwa hiyo, kama wenzetu wa *TANESCO* walikuwa na wasiwasi Dr. Idrisa atulie, mambo mazuri yanakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kupongeza na kufurahi kwamba wawekezaji wanatakiwa wapeleke umeme vijijini na hata katika Sheria hii katika kipengele cha 37 mpaka 39 someni vizuri mtaona kwamba wametilia mkazo kupelekwa umeme vijijini. Kwa hiyo, kama kulikuwa na wasiwasi kwamba Sheria hii ikipita umeme hautapelekwa vijijini ati kwa sababu hao watakaokuja watakuwa wanafanya biashara tu, si kweli hata kidogo. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, tusiwe na wasiwasi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu kama ilivyosemwa katika kifungu cha 7 hauhusishwi hata kidogo katika masuala ya *Richmond*. Tunaambiwa kwamba wale ambao waliingia mkataba kabla ya Muswada huu kupitishwa hawataruhusiwa kwa kipindi cha miaka mitano. Kwa hiyo, kama kulikuwa na mawazo kwamba pengine Muswada huu utasaidia masuala ya *Richmond* na wengine wengine, hapa suala hili halipo. Kwa hiyo, ni matarajio yangu makubwa kwamba Waheshimiwa Wabunge wale ambao walikuwa na wasiwasi watauunga mkono Muswada huu ili uweze kupita kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapata Uhuru katika nchi yetu mwaka 1961 wananchi walikuwa milioni 9. Dar es Salaam walikuwa 300,000 tu. Maana yake nini? Maana yake ni kwamba sasa hivi Tanzania tunakaribia milioni 40 na Watanzania tunajua nini maana ya umeme. Kwa hiyo, si kweli hata kidogo kwamba kazi hii inaweza ikafanywa na *TANESCO* peke yake kusambaza umeme. Tuko wengi, kwa hiyo, kuruhusu Muswada huu maana yake ni kwamba tutapiga hatua ya kasi katika kuleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Tumeambiwa hapa kwamba mpaka hivi sasa umeme vijijini ni asilimia 1 tu, hii ni hatari kweli kweli na ndiyo inayosababisha watu wengi wa vijijini kukimbilia mijini. Lakini kama tutasambaza umeme katika nchi nzima na hasa vijijini nina hakika vijana wengi hawatakuja mijini kwa sababu watautumia umeme huu kwa shughuli mbalimbali, useremala, kusaga mahindi na vitu chungu nzima.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana wenzangu ambao walikuwa mguu nje, mguu ndani waunge mkono Muswada huu. Nataka kusema kitu kimoja kwamba wakati mwingine sisi tunakuwa na wasiwasi bure tu. Nasema hilo kwa sababu gani? Tunawaogopa sana wawekezaji kutoka nje, hivi kwa nini tunawagopa? Tunawaogopa kwa sababu hatuwatungii Sheria ambazo wao zitawabana. Nataka nitoe mfano, wenzetu katika nchi zingine wanayafanya haya, wanakwambia wewe mwekezaji unataka kuwekeza ndiyo, sisi Sheria zetu katika nchi hii ni hizi, sasa kama utapenda kuwekeza wekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu hao wanachofanya kwa mfano, kwanza wanaandaa miundombinu yao yote ya lazima halafu pili, wanatunga Sheria zote kama leo tunavyotunga hapa. Halafu tatu, hao wanaokuja kuwekeza, wanapokuja kuwekeza kama ni katika kuzalisha vitu mbalimbali wanaambiwa kwamba vitu hivyo ukizalisha, anza kuuza kwako huko huko kuthibitisha kwamba utakachozalisha hapa kina thamani. Kwa hiyo, utaratibu huu tutautumia katika Sheria hii kama ilivyoelezwa katika Sheria. Hao wanaokuja kuwekeza tutawaambia kwamba Sheria ni hii. Tunataka umeme uende vijijini, usipopeleka vijijini hatukupi leseni hiyo.

Hapa ndipo ninapotaka kuwaambia wenzetu wa *EWURA* wasifanye mchezo hata kidogo katika hili. Wasibabaishe babaishe hata kidogo. Mifano tumekwishaiona, tumeiona kwa wenzetu wa *Richmond,* wamekuja hawana uhakika, hawana uwezo kiasi hicho. Sasa tusingependa kurudi tena huko. Tunachotaka tupige hatua. Nchi isiyokuwa na nguvu za umeme maendeleo yake yanakwenda kwa kususasua kweli. Kwa hiyo, wenzetu wa *EWURA* watatoa mchango mkubwa katika kuhakikisha kwamba hawa wanaokuja kuwekeza wana uwezo kama sheria hii inavyosema.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechoka kuonekana kwamba sisi Watanzania na Bara la Afrika kwa ujumla hatuna mipango mizuri ya maendeleo. Kazi yetu sisi ni kubahatisha bahatisha tu. Sasa tunachotaka ni kuona kwamba sheria hii tunayoipitisha leo ioneshe kwamba Watanzania tuna mipango mizuri. Watanzania tunafahamu umuhimu wa umeme ili nchi yetu iweze kupiga hatua katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimefurahi kuona kwamba ule mfuko wa umeme vijijini bado unatiliwa mkazo, na mimi naomba kuutilia mkazo. Mfuko huu uimarishwe, usaidie kuleta umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 47 tulitakiwa tupige hatua kubwa kweli kweli. Wenzetu wengine walioendelea baada ya miaka 20 tu ya uhuru wao, mifano iko chungu nzima, waliweza kutusaidia. Sisi tuna miaka 47 mpaka hivi sasa ya Uhuru wetu bado mwendo wetu ni mdogo sana. Wakati mwingine unajiuliza, hivi ni nini hiki hasa? Wanakuja watu hapa wanatubabaisha babaisha, ni nini hiki?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, kwa kauli moja tuunge mkono muswada huu. Mengine yanayozungumzwa yatashughulikiwa

kwa utaratibu. Nyote nyinyi mnaufahamu, tusiwe na wasiwasi hata kidogo, uwezo tunao, nia tunayo na sababu tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa Jimbo langu la Lulindi, kwa muda mrefu sana wameomba umeme, miaka 15 iliyopita. Lakini kwa sababu ya uwezo mdogo wa *TANESCO* mpaka leo hii ninvyozungumza hawajapata umeme. Kwa hiyo, leo wananisikia hapa wanasema Suleiman Kumchaya huyo anauleta umeme. Kama Lulindi iko hivyo nina hakika na katika maeneo mengine ya nchi yetu tunahitaji umeme haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisije nikasahau kwanza niwatake Waheshimiwa Wabunge wote waunge mkono muswada huu na mimi mwenyewe ninaunga mkono kwa moyo wangu wote. Asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Asante, sasa nitamwita Dr. Luka Siyame. Hayupo! Anayefuatia ni Mheshimiwa Lilombwi Kabuzi. Kabuzi Rwilomba!

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Asante sana, umeniita vizuri sasa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kuniruhusu nami nichangie hoja ya muswada ulio mbele yetu. Mimi ni kati ya wale ambao walikuwa hawakubaliani kabisa na muswada huu tangu awali. Lakini baada ya marekebisho na baada ya maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nimeshawishika sana kuona kwamba muswada huu nilikuwa nakosea, nilikuwa siutendei haki.

Nimshukuru sana Mheshimiwa waziri, kwanza kwa kuwa mvumilivu. Nilikuwa nadhani angekimbia na kujiuzulu na kuacha kazi ya uwaziri kwa sababu suala hili lilikuwa gumu sana. Lakini kwa ujasiri wake na uvumilivu hakufanya hivyo, nadhani muswada huu ulikuwa ni sehemu ya *training* kwake na mafundisho kidogo. Kwa hiyo, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nasema nauunga mkono kwa nguvu zote muswada huu. Nilikuwa na wasiwasi kwamba sasa tunakaribisha wengine, ajali inaingia tena. Lakini baada ya maelezo ya kwanza aliyoeleza hasa kuilinda *TANESCO* mimi nimefarijika na ninaomba afanye hivyo na naiomba Serikali ifanye hivyo. Kwa kweli maelezo yale sina haja ya kuyarudia, kipengele hicho kinajitosheleza na nina imani bwana *TANESCO* atafanya kazi. Lakini napenda nitoe tahadhari na ndiyo kitu kikubwa nilichotaka nikizungumzie hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa *TANESCO* sasa na wenyewe wakibebwa wabebeke. Siyo unaambiwa uwashikilie basi uwashikilie, na wenyewe washike waende. Kuna hela nyingi zimeelezwa kwenye maelezo mbalimbali hapa, nilikuwa nahudhuria vikao vyake. Kuna hela nyingi zitaingia kwenye *TANESCO.* Hela hizi siyo za kutumbua ni za kufanya kazi. Kama mfanyakazi wa *TANESCO* jitahidi uoneshe nia anayoonesha Waziri na Serikali inayoonesha kuwasaidia. Siamini kwamba *TANESCO* tangu ilipoanza ilikuwa haina pesa, ilikuwa na pesa. Lakini matumizi yamekuwa mabaya mpaka yamekuja kulalamikiwa huku. Mtu unaingia *TANESCO* unajua sasa nitawasomesha

watoto wangu Ulaya, nitanunua magari ya kifahari, nitafanya hiki, kile, fedha haziendi zinakotakiwa. Sasa Serikali imeahidi kuwaletea fedha, tunaomba *TANESCO* fanyeni kazi mhakikishe mnazitumia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja yako na nina imani ndiyo ilikuwa wasiwasi wa Wabunge wengi kwamba hawa tunaowakaribisha ni nani watakaoingia? Nawaomba *EWURA* waelewe kwamba tunawategemea sana. Muswada unaweza kuwa mzuri lakini kama *EWURA* kuna watu wa ajabu wanaofikiri sasa ndio wakati wa kupata mapato, tunaweza kweli tusifanikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *EWURA* mhakikishe wanapokuja muwadhibiti kweli kweli na muwe *transparent,* kama mtu hawezi hawezi. Siyo mtu hawezi, anapewa kazi kwa sababu ameweka mambo vizuri na hicho ndicho kinachotuangusha Tanzania, tunajidai tunakimbia haraka. Jana Mzee Mzindakaya, alitoa neno la kukimbia, tunazungukazunguka na kajina kale nimekasahau, sijui kadudu gani kale? Tunazunguka spidi kubwa lakini hatufiki popote. Kwa hiyo, *EWURA* tusaidieni. Katika muswada huu nimefurahishwa sana kuna maelekezo kwamba unaelekea utasaidia vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunambana Mheshimiwa Ngeleja, alitoa hata siri ya vijiji, akaleta orodha kubwa sana ya vijiji. Ingawa orodha ya vijiji kwangu naona kweli amekwenda vijijini lakini sehemu zingine ni vijiji vya mjini. Kwa mfano, Nyegezi, Mwanza, Nyegezi, Mkolani, sasa hapa si mjini, hivi vijiji gani? Nimeangalia na Tanga, vijiji vya mjini, Morogoro nimeangalia Kihonda, sasa Kihonda vijiji gani hivi? Nimeangalia mpaka Mbeya, Dodoma, Bahi hapana! Afadhali Bahi kidogo. Lakini bado tunahitaji mwangalie vijijini, kwa sababu vijiji vya mjini vina uwezo hata wa kuvuta lakini vijijini kuna shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba Mheshimiwa Waziri wakati wa ku-*wind up,* atueleze *REA* itafikaje katika vijiji vilivyo pembeni kama vijiji vilivyotajwa ambavyo nina uhakika navyo. Vijiji vya Buselesele, Nkome, Nungwe, Wangasa, Bukondo, Nyarugusu, Nyangh'wale, Msalala, Bukoli, Nzela, Katowo, Nyamalimbe na Chigunga.

Hivi ni vijiji ambavyo ni vya wachimbaji, hawa wachimbaji ni watu wako Mheshimiwa Waziri. Wanahitaji umeme na bahati nzuri umevitaja, hapo umetumia akili sana kutaja labda ulikuwa unajua nitakuwa mbishi lakini hapa siwezi kubisha kwa sababu nitakuwa nabisha pua nasahau mdomo. Hivi ni vijiji vya wachimbaji, umekwenda kule Mheshimiwa umewaambia naleta umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mdogo wangu Mheshimiwa Msabaha alikwenda kule akasema analeta umeme, alipita kwenye vijiji hivi. Mheshimiwa Yona naye alipita akasema naleta, sasa mimi nashindwa kusema kwa sababu nyinyi mmekeishasema lakini nadhani sasa kwa sababu mmeleta kwa maandishi si uongo, tutaulizana wakati wa Bajeti. Lakini angalau tudokeze *REA* ataingiaje kule? Naomba tumwezeshe *REA*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba sana muswada huu kama utakuwa kama ulivyoandikwa na ukatekelezwa kama ulivyoandikwa nina imani hapatakuwa na ujambazi wowote unaompa mtu wasiwasi. Lakini watu wetu tulionao kama watafika kule wakatugeuka muswada huu utakuwa mbaya.

Naomba mikataba inayopangwa iwe wazi na iwe ya uhakika kwamba tunapata umeme kunakotakiwa na kihalali. Tatizo ni mikataba. Hata kwenye madini kuna tatizo. Kwenye madini kuna tatizo kwa sababu mikataba, unakuta sheria vipengele vidogo tu, vipengele vidogo ndivyo vyenye makosa lakini mikataba ndiyo inakuwa tatizo. Sasa kwenye umeme hapa, umeme ni uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri na Serikali, naomba sasa uwe mwisho wa kutuambia jamani safari hii kuna upungufu na kadhalika. *MCC* imetusaidia kwa mfano, vijiji nilivyovitaja viko kwenye *MCC,* kweli wanaweza kuwa wametudanganya, si fedha zipo? Sasa mje mtuambie kasungura kadogo, ni nini. Sungura huyu aletwe mzima, asiondolewe maini wala figo na moyo, tuje tumgawe hapa vizuri. Asante sana. Naunga mkono hoja kwa nguvu zote. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Niungane tu na wenzangu kwa kuukubali muswada kwa asilimia 100. Huu muswada umekuja wakati ambapo kwa kweli kuna ukuaji wa uchumi mkubwa pamoja na maendeleo ya kijamii makubwa kiasi kwamba shirika lililokuwepo *TANESCO,* limeshindwa kukidhi haja ya mahitaji ya wananchi wetu. Sasa kulingana na sheria hii ambayo tunaipitisha leo, mimi naamini tunaipitisha kwa sababu haina mizengwe yoyote ya kutokupitishwa. Ni kama walivyozungumza wenzangu kwamba ni Watanzania wengi mpaka sasa hivi hawajafikiwa na umeme, kwa hiyo, lazima tuwe na mikakati madhubuti ya kufikisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa la nchi hii ni moja tu. Sheria tutatunga hata zijae lakini usimamizi wa sheria zenyewe ndiyo tatizo.

Mipango tunayoipanga inachelewa mno. Kwa mfano, hii mpango tunaambiwa hii *PSMP,* kuna tatizo gani? Mpango unatumia miaka kuandaliwa na kufikishwa Bungeni, kuna tatizo gani? Mpango wa *REA. REA* tulipitisha sheria yake, *Rural Energy Act* ya mwaka 2005, mpaka leo hatujaona mafanikio. Mwaka jana Serikali ilibajeti shilingi bilioni 10, sawa, mahitaji shilingi trilioni 1.2. Sasa kweli tuna mkakati wa kuwafikishia wananchi wetu umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ukifanya pale hesabu, *fraction* yake unaweza uka-*ignore equal to zero* kwa sababu *is zero point zero one.* Sasa kasi hiyo tutawafikishia umeme kwa miaka mingapi? Tutakaa na hizo ahadi za umeme kila siku. Tutawaahidi hao wananchi umeme tunawapelekea lakini hatuwezi kuwapelekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hiyo kuwadanya wananchi kuwapa matumaini kwamba tutawapelekea huduma ile ni ufisadi. Shirika letu la *TANESCO* liko kwenye hali ambayo siyo nzuri kwa sababu kwanza limeshindwa kujiendesha, tumekuwa tukilifadhili fedha za ruzuku kila mwaka.

Hesabu za mwaka 2006 Shirika hili lilipata hasara ya shilingi bilioni 183 na hata hivyo *auditor* alishindwa ku-*form opinion.* Yaani ilionekana hesabu ni chafu mno. Sasa hata hiyo tu? Kwa sababu hesabu chafu siyo hasara, unaweza ukawa umepata hasara lakini hesbabu zikawa safi. Walipata *disclaimer opinion,* ina maana kwamba *auditor* alishindwa ku-*form opinion basing of forming opinion ilishindikana.* Sasa ile nayo tutasema kwamba ni kwa sababu *TANESCO* imepewa mzigo au uzembe wa watendaji? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi najiuliza, ni kwa nini mashirika ya umma yanajiendesha kwa hasara lakini mashirika ya watu binafsi yanajiendesha kwa faida? Kuna tatizo gani? Je, mashirika haya ya umma yanasimamiwa na nani? Kwa sababu katika mtizamo wa hotuba mbalimbali za Serikali, msajili wa mashirika, wote wanalalamika. Sasa inafika mahala Bunge linalalamika, Serikali inalalamika, na wananchi wanalalamika. Sasa nchi inalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo, lazima tupitie upya usimamizi wa mashirika yetu ya umma. Je, uhuru yaliyopewa mashirika ya umma hautumiki vibaya? Usimamizi wa fedha uko sawasawa, manunuzi uko sawasawa? Je, mikataba hii sasa mibovu ambayo tunaingia kila mwaka tunajirekebishaje? Lakini je, watendaji tulionao kule wanaosimamia mashirika yetu, ni kweli wana utashi na machungu ya nchi yao? Au kama yale aliyoyasema ndugu yangu kwamba watu wanajipanga, kuhujumu tu. Ni kuhujumu tu, kwa nini? Mashirika tumekwishaona mengi yanapotoka katika mikono ya umma yanapokwenda kwa mtu binafsi yanafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niweze kusema kwamba uzoefu unaonesha kwamba ubinafsishaji na ukaribishaji wa wawekezaji binafsi sio mbaya. Kwa sababu kutoka mwaka 1993 tulipoanza kuwakaribisha wawekezaji binafsi pamoja na ubinafsishaji, nchi yetu iliweza ku-*shoot* katika ukusanyaji wa mapato, kutoka shilingi bilioni 25 mpaka bilioni 300, 2007. Kwa hiyo, tangu mwaka 1993 mpaka kufikia 2007 tumekwisha-*shoot* mpaka shilingi milioni 300 lakini hii yote imeletwa na changamoto kubwa ya ubinafsishaji wa mashirika lakini pamoja na kukaribisha wawekezaji binafsi. Wawekezaji binafsi, tumetanua ajira lakini pia tumeongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzuri wa muswada, yale mengine yote yametajwa na wenzangu kupitia Kifungu cha 41, kifungu kidogo cha 6 pamoja na kile cha 39, kifungu kidogo cha 4, wamefafanua vizuri. Lakini faida ya muswada huu baada ya hapa ni kasi ya kuwafikishia umeme wananchi wetu. Naamini kwamba tuwafikishia wananchi mapema sana. Lakini ajira zinaongezeka na ninaamini kwamba hata hizo bei za umeme kwamba nazo zitashuka. Nashukuru sana kwa sheria ambazo zimewekwa kwa ajili ya kulilinda shirika letu la *TANESCO.* Shirika linayumba lakini *we have no alternatives,* lazima

tulilinde. Na mazingira ambayo limewekewa basi ni wao washindwe. Nasema *there is no traffic jam along the side of extra mile.* Hakuna msongamano kama utaamua kwenda hatua za ziada. Kwa hiyo, sina wasiwasi na *TANESCO* kama wanaweza kuyumba katika mashindano haya, lakini *TANESCO* anazo changamoto kubwa tu ambazo anatakiwa kuzifanya ili aweze kuingia katika hili soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kubwa, ni suala hili la umeme vijijini kama nilivyoligusia pale awali. Ni kwamba tunatakiwa tuoneshe mikakati yetu ya dhati. Tusiwe tunapoteza muda wa kukaa hapa tunatunga sheria ambazo haziwasaidii wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na hiki chanzo cha mapato kilichowekwa cha asilimia tano cha kupeleka umeme vijijini, asilimia tano ya mapato ya wazalishaji wa umeme wenye leseni haitoshi. Naomba Mheshimiwa Waziri wakati ana *wind-up,* kwanza aniambie kwamba ni shilingi ngapi zitapatikana kupitia leseni hizo? Lakini napendekeza kwamba tungeweza kuweka hata tozo walau la shilingi tano katika muda wa maongezi wa simu za mkononi zikajaza katika ule mfuko wa umeme vijijini ambao naamini kwamba hiyo kasi ya kuwafikishia wananchi umeme vijijini itaongezeka kwa kasi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kengele ya kwanza imelia lakini ulisema nisiseme umeme wa Mwandoya lakini nakuomba tu niseme. Mheshimiwa Waziri, nimwombe sana kwamba atakapokuwa ana-*wind-up* aseme sasa hii *line* ya umeme ya wananchi wa Mwandoya inayoanzia Momboko, Semu, Mbalagane, Lubiga na Mwandoya penyewe ni lini umeme huu utakwenda? Kwa sababu ameniahidi muda mrefu sana na leo nadhani wananchi wangu wanamsubiri kwa hamu awaambie umeme wao sasa hatima yake ni lini? Lakini pia umeme katika jimbo langu umepita kwenye kijiji kimoja tu cha Itinje. Napo kwenye vituo, kwenye zahanati haujafika mpaka sasahivi, kwenye shule ya sekondari haujafika mpaka sasa hivi. Waziri aniambie utafika lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye *amendments,* Ibara ya 15, ukurasa wa 16. Ibara ya 15(2) wameandika *proper records and books of accounts,* mnaweza mkaangalia pale. Nilikuwa nashauri kwamba pale tungeweka maneno *proper records.* Halafu kule ameandika neno *accounts* tu, kaandika *proper records and books of accounts.* Ibara ya 15(5) kuna neno *reports* limetumika. Mimi naomba iwe labda *audit report because always we place reliance on audited financial reports* na sio *report* ya aina yoyote. Kwa hiyo, nilifikiri kwamba pale tungeongeza maneno *audit report.* Lakini ibara nyingine ya 16(6) *separate accounts,* mimi ningefirkiri ingekuwa *separate books of accounts.* Baada ya hizo *ammendments* zangu niweze kusema sasa naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Asante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda huu hautoshi lakini tukirudi mchana atakuwa Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na wengineo. Angalau kwa leo tutakuwa na 14, Jumatatu 19,

pengine lazima tufike mpaka Jumanne kwa sababu hakuna namna. Sasa Waheshimiwa Wabunge, kama mna marekebisho yoyote mnayotaka kufanya katika muswada huu, upo muda wa kutosha sana, tumieni kifungu cha 86 ama kifungu cha 89, fanya marekebisho. Kwa sababu kama hivi mko hamsini na ngapi hapa, kila mtu amsemee Waziri kwa kusema tu, hawezi kuyashika yote haya. Kwa hiyo, tumieni maandishi , nafikiri tubadilishe kifungu hiki kisomeke hivi na muwasilishe kwa Katibu kusudi yaweze kuingia hapa. Inaruhusiwa hiyo.

Tangazo lingine ni kwamba, Bunge hili la 11tumepata Kamati mpya na viongozi wa Kamati wapya. Hata kama wengine wako mlemle lakini ni Kamati mpya. Kwa utaratibu ambao tulikuwanao hawakuwa wametoa taarifa zile, Kamati zilizomaliza hazikuwa zimetoa taarifa zao katika kipindi walichokuwa nacho. Sasa tukisema waweke Mezani na zijadiliwe, kutatokea tatizo kwamba kuna Kamati zingine zimegawanyika. Na hata kama hazikugawanyika wale walikokuwa wamehusika na ripoti zile si hawa waliopo. Kwa hiyo, tumekubaliana kwenye Kamati ya Uongozi kwamba taarifa zile kama ziko tayari zitakuwa-*laid on the Table* kama kawaida. Na Kamati yoyote ile inaweza ku-*lay on the Table* ili kusudi ziwepo kwa *reference* ya Wabunge na Kamati hizo nyingine mpya. Kamati pekee ambayo taarifa yake itabidi tuijadili kwa mujibu wa sheria ni Kamati ya Hesabu za Serikali *(Public Accounts Committee)* na Hesabu za Serikali za Mitaa. Hizo zitakuja kipindi hiki kabla hatujaondoka. Hizo zitawasilishwa kwenye Meza na kujadiliwa, kwa sababu ni matakwa ya kisheria kwamba taarifa hizo lazima ziwasilishwe Bungeni na kujadiliwa. Kwa hiyo, ni taarifa mbili tu tutakazozijadili kwa maana hiyo. Baada ya kusema hivyo mchana Mheshimiwa Jenista Mhagama, atakuja kukaa Mezani. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 jioni.

*(Sasa 6.48 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*
*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na *Order Paper* yetu jioni hii ya leo kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza toka mmeniidhinisha tena kuwa Mwenyekiti wa Bunge, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuruni sana kwa kunirudisha tena kwenye Kiti hiki, nasema asanteni sana. Baada ya maneno hayo ya shukrani, Katibu endelea na shughuli zilizopangwa.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu wa umeme *Electricity Bill*, 2007. Mimi nimeusoma Muswada huu vizuri na nikauona unaleta matumaini makubwa sana hasa kwenye maeneo mawili, kwanza, utasaidia watumiaji wa umeme kupata bei nafuu na pili wenye maeneo ambayo hatujapata umeme mpaka sasa hivi tuna matumaini makubwa sana ya kupata umeme ambayo tunategemea kutokana na Muswada huu. Muswada huu tunaoupitisha leo, sisi ndiyo wenye maslahi nao, hatuna umeme, nina imani tunaupenda sana. Kabla sijaendelea na mchango wangu naunga mkono kwa asilimia 100.

Umeme ni kiungo kikubwa sana katika maendeleo ya nchi. Kwa bahati mbaya sana kwa muda mrefu hata Mheshimiwa Waziri alisema vijijini ni asilimia moja tu ambao wameweza kupata umeme. Kama umeme utaweza kwenda vijijini utachangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa. Nilipata nafasi ya kutembelea nchi mbalimbali kama China na Thailand.China utakuta umeme umeenea mpaka kwenye mashamba ya wakulima. Waliweza kupeleka umeme mpaka vijijini kwa wakulima ndiyo maana utakuta China wanalima mara tatu kwa mwaka kutokana na ama na mvua. Baada ya mvua kwisha wanatumia kilimo cha umwagiliaji kutokana na umeme ilio-*invest* Serikali kupeleka kwa wakulima. Katika hii ibara ya 37, 38, 39 kuhusu *REA* hapa tunaona tu kwamba tunapitisha Muswada, *REA* itafanya kazi vizuri lakini kwa jinsi gani *?* Leo itafanyaje kazi, itawezaje kupeleka umeme vijijini kama hela hazitoshi? Tulikuwa na mpango wa *ERT* umetoka, sasa hivi inakuja REA, *REA* hii isije baadaye ikageuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana walipewa shilingi bilioni 10, gharama ambazo *REA* wamesema kwamba ili waweze kupeleka umeme vijijini ni shilingi trioni 1.2. Angalia tofauti iliyopo hapo, sasa tunawezaje, kwa sababu kupitisha Muswada ni kupitisha tu!

Tumemaliza Muswada kinachofuatia sasa ni umeme uende vijijini haraka iwezekanavyo ukasidie siyo tu wanakijiji maana yake unapo-*invest it will be repaid, in the future* unarudi katika pato la Taifa. Je, tunawawezesha *REA* wapate fedha za kutosha? Shilingi bilioni 10 kwa 1.2 ina maana zaidi ya miaka tisa, kumi, kumi na mbili ndiyo hata iweze ku-*cover* nchi nzima waweze kupeleka umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono napendekeza kuwa badala ya asilimia 5 iwe asilimia 10 lakini tutazame pato lingine kwa *REA*. Kuna *other sources of income* ambazo tunaweza tukazitengeneza na kupata *revenue* ya kutosha kwenye *airtime*, kwenye simu.

Tukiweka asilimia tano tu kwenye simu maana yake mtu anayeweza kuongea na simu hawezi kushindwa kulipa asilimia 5 au 10. Hiyo moja kwa moja itakwenda *REA i*kasaidiana na hii asilimia 10 ambayo wanapata kwenye pato lingine. Na Serikali yenyewe itafute fedha ili angalau ipate shilingi bilioni 30 mpaka 40 kwa mwaka. Leo ikipata ndani ya miaka mitatu minne Tanzania nzima itakuwa imepata umeme kutosheleza vijiji vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea bado zinakimbia kwa maendeleo sisi we *are developing country* lakini naona kama bado tunatembea ni muhimu sana kufikiria, Muswada tunapitisha lakini tunapeleka umeme vipi ni fedha, fedha tunazipataje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa maoni yangu hayo kwamba ili REA waweze kupeleka umeme vijijini vizuri ni muhimu sana wapate fedha za kutosha angalau bilioni 30 au 40 kwa mwaka ili waweze kufanikisha zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa *ERT* ambao sasa hivi *REA* ukienda jimbo la Solwa, wananchi hasa wa maeneo ya Pandakichiza, Ndisera, Magazi, Solwa na Sarawe, ukiwaambia mimi kila siku nasema nitajitahidi kadri ninavyoweza kushirikiana na uongozi husika kuona kwamba umeme unakuja jimbo la Solwa, wengine hawaamini wanaona kama ni kitu cha ajabu kutoka tu mbinguni.

Lakini wakati tunapitisha Muswada huu sasa niiombe Serikali ifikirikie kwa kiasi kikubwa jimbo la Solwa tuupate umeme. Na nimewahi kwenda kwa Mheshimiwa Waziri Ngeleja mara nyingi tu na naomba kweli kweli kwamba Serikali imeweza ku-*invest* kuweka bomba la maji kutoka Mwanza imepita jimbo la Solwa kwenye kata saba mpaka Shinyanga kwa nini isifanikishe katika umeme.

Gharama ya lile bomba ni *almost* shilingi bilioni 100 na 80 na kitu. Sasa hivi tukiongeza shilingi bilioni 1.5 tukachangia pamoja na ile miundombinu ya maji tutakuwa tumekamilisha, itaweza kuvutia hasa wafanyabiashara wadogo wadogo, mashirika madogo madogo na hata viwanda. Kwa hiyo, utaona umeme una umuhimu kiasi gani.

Mheshimiwa Waziri Ngeleja niliongea naye sana nina imani sasa hivi ananisikiliza na hapa namwomba kwa mara ya pili atambue kuwa umeme ni muhimu sana tena sana katika jimbo la Solwa na kwenye maeneo ambayo hawana umeme katika Jamhuri ya Muungano huu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* nawaomba sana wawe makini. Tunafurahia hii Miswada lakini baadaye kwenye mikataba ile na kadhalika tunapo-*privatise* yanaweza yakijitokeza mambo ambayo hatukuyatarajia. *EWURA* wawe makini sana waweze kusimamia bei na ni matumaini yangu kuwa kwa sababu *private sector* watakaopewa kuzalisha na kusambaza umeme mpaka kwa watumiaji hawatabeba haya madudu *(capacity charge)* ambayo sasa hivi Wizara imesema inaichukua yenyewe, ni kwamba bei ya umeme itashuka kwa asilimia kubwa sana. Mimi nitumaini hivyo kwamba bei ya umeme itashuka kwa asilimia kubwa sana kwa watumiaji na hasa wenye kipato kidogo na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuuliza swali mwaka 2006 kuhusu kupata umeme jimbo la Solwa, nilikuwa nimeahidiwa kwenye Bajeti ya 2009/2010 lakini mimi nimeomba kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Waziri Ngeleja na Mheshimiwa Waziri Mkuu upo hapa, nakuombeni sana kwa mara ya pili mnisaidie Jimbo la Solwa. Kwa muda mrefu sana tumekuwa nyuma kimaendeleo, nadhani Muswada utafungua vizuri njia ili tuweze kupata maendeleo ya uhakika katika jimbo la Solwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu siwezi nikarudia yale ambayo Wabunge wengi wameyaongea, baada ya kusema hayo naomba sasa niunge mkono kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie juu ya Muswada huu mpya wa umeme. Vilevile niwashukuru sana Wabunge wote na wadau wengine walioshiriki kuuweka sawa Muswada huu.

Muswada huu ulipokuja wakati ule haukueleweka. Hata kabla haujaja humu ukakataliwa, lakini kwa sasa tuna imani kubwa tutaupitisha na watafaidika wote. Sisi wengine tunaotoka kwenye mikoa inayoitwa mikoa maskini huu Muswada utatusaidia sana.

Nina imani kabisa wawekezaji binafsi kufika Singida itachukua muda, kwani wao wanafuata mahali kwenye viwanda vingi, watakwenda mahali wenye mazao ya kudumu, watakwenda kwenye migodi lakini kwetu Singida, Tabora na maeneo mengi ya Shinyanga tulie tu! Nafikiri hata Longindo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tunapitisha hii sheria mpya na tunalijenga shirika letu la umeme ambalo tunalo kwa miaka mingi, shirika ambalo limepita kwenye misuko suko mingi. Tukipitisha sheria hii na shirika tuliunde upya kuanzia bodi, kuna wafanyakazi, sio wote wa shirika hili ambao wamekulia humo wamezeekea humo.

Hawa hata mkiteua *General Manager* mpya anaambiwa walikwishapita wangapi wakatukuta humu na wakatuacha. Sasa ni juu yetu sisi tuhakikishe kuwa Bwana Idris Rashid anapata wataalamu wapya wazuri maana tunakwenda kwenye dunia ya kileo hao wengine walikuwa mle na utaalamu uliopitwa.

Sasa hivi tutaleta vitu vipya, sisemi kwamba wote ni wabovu lakini tuangalie wale ambao wamekuwa kikwazo makao makuu ya shirika, mikoani, wilayani, wapewe haki yao wakapumzike. Tupate watu wanaokwenda na wakati, la sivyo tutarudia matatizo hayo hayo. *(Makofi)*

Kwa sababu yanakuja mashirika binafsi, mashirika kutoka nje na pesa zao tuwapongeze sana hawa tuliokuwa nao lakini sasa ni lazima tubadilike tulijenge upya na nina imani hata wananchi wetu kule vijijini wataridhika.

Wananchi wetu wanahitaji sana umeme, wananchi wetu sasa hivi wanajenga nyumba za kisasa, wananchi kama kule Iramba ya Mashariki tunalima alizeti kwa wingi tunataka tuvune alizeti tutengeneze mafuta tuuze mafuta na mashudu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa urais wa Mheshimiwa Mwinyi alikuja Iramba ya Mashariki na kweli wakati ule tulikuwa bado. Akasema lakini nyinyi watu wa Iramba ya Mashariki mnaniomba umeme, umeme unaogopa kuingia kwenye nyumba za nyasi na nyumba za tembe lakini leo njoo Iramba Mashariki yote watu wamejenga nyumba za kisasa na tunahitaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa kulipa tunao, sisi ni wafanyabishara na wakulima wakubwa kwa wale wenzetu waliojaliwa Arusha, Moshi, Mbeya, Bukoba na kwingine na wale wenye machimbo tunajua wale hawana tatizo lakini sisi watu wa chini tutalihitaji shirika hili la umeme. Kwa hiyo, lipewe nguvu na liongezewe pesa na tuombe *development partners* wetu waendelee kutusaidia, mimi nina imani tutafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasema wanaokuja kuleta umeme wanaweza wakatengeneza vifaa vinavyotumika kwenye hizo shughuli za umeme. Hapo ni lazima tuwe waangalifu. Sasa hivi tumekwishasoma, mali inatoka China inakuja inasagwa, sasa na hawa wasije wakaifanya Tanzania kichwa cha mwendawazimu kuja kutengeneza vifaa vibovu.

Hapa *EWURA* na Serikali ndio zisimame na wenzetu wa viwango wasimame, ni lazima tuanze kwa kasi mpya na twende ili tufaidike. *EWURA* wakizubaa tumeliwa, kwa hiyo, ni lazima tuwe wakali na nasema hivi hata hii *EWURA* ikibidi kama kuna watu wanaichezea chezea nayo iundwe upya isafishwe. Tunaingia kwenye hatua ambayo tunataka maendeleo yaende vijijini. Kwa hiyo, ni lazima tuanze upya, Msindai analeta leta mchezo weka pembeni, mpe haki weka mwingine anayeweza. (*Makofi*)

Tuna mengi tutakuja kusema wakati wa Mkutano ujao wa Bajeti ila kwa sasa naomba Muswada huu tuuchukulie kwamba Tanzania sasa tunajiweka kwenye sehemu nzuri na tuzipe vibali kampuni nyingi.

Kuna maeneo mengi ya gesi, ukienda bonde la ziwa Elias, bonde la Wembele, dalili zote zipo lakini wanaogopa wanaokwenda huko sijui kwa nini? Njooni! Huko ndiko

kuna maeneo mengi yana mali, tukishavumbua gesi maeneo hayo ya Bara maana yake tunapunguza hii shida ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana sasa hivi tusilete mchezo kabisa. Tuna imani kubwa na Waziri wa Nishati na Naibu wake na watendaji wote.

Mheshimiwa Waziri Ngeleja na timu yako huu ndiyo mzigo wako, ndiyo utakupeleka au utakurudisha nyuma na sisi bado tuna imani kubwa kwa miaka mingi inayokuja kwani umekuwa tukipewa ahadi miaka na miaka bila mafanikio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iramba ya Mashariki umeme upo pale njiani Iguguno na mwingine upo sehemu ya Nkungi hospitali ambao nao niliupata kwa mbinde baada ya kumtumia Rais Mstaafu, Mheshimiwa Mkapa ndiyo akanisaidia ukafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ule mradi ulikuwa ufike mpaka Nduguti lakini mpaka leo haujafika. Tunasikitika sana na wananchi wa Iramba Mashariki wanasikitika, uwezo wa kulipa sisi tunao, tuleteeni umeme.

Niliahidiwa kupata umeme kutoka Kinampanda kwenye Chuo cha Maendeleo kiasi cha kilomita nne, lakini huu ni mwaka wa saba mpaka leo hakuna. (*Makofi*)

Sasa kazi kwenu, Mheshimiwa Ngeleja pale Tunuli njiani waliokuwa wanatengeneza barabara ya kwenda Sherui wameweka transfoma kijijini na wananchi wamekwishasuka nyaya kwenye nyumba.

Kwanza walitaka kung’oa hiyo transfoma, nashukuru ukasema haing’olewi, sasa waunganishe wananchi wapate umeme.

Kutoka Iguguno kwenda Kinyangili kilomita 17 tunalia umeme mpaka leo 2001. Tuliambiwa kila mbunge aandike maeneo ambayo anataka umeme uende. Tukaorodhesha tena, Waziri aliyekuwa wakati ule akasema umeme utafika Nkalala, Mwaga, Kidarafa, Matongo, Lumanga na Ibaku lakini mpaka leo hakuna.

Sasa sisi tunaomba sheria hii iwape nguvu mpya ili muweze kutimiza zile ahadi kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi wa Tanzania.

Utaboreshaje kama wanakaa kwenye giza, utaboreshaje kama hawawezi kusaga mahindi uwe unga mwananchi auze kwa bei kubwa zaidi. Utaboreshaje kama hawezi

kuweka kiwanda kidogo atengeneze baiskeli apate pesa, atengeneze mkokoteni, mafuta nimekwishasema na hicho ndicho cha kwanza na ndicho muhimu Iramba Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakuomba sana nirudie kusema kwamba tuna Wabunge wazuri wameuchonga huu Muswada mpaka ukarudi ukaendana na sera ya nchi.

Shirika la umeme lina sera nzuri sana. Wizara ina sera nzuri sana, tatizo ni utekelezaji. Kuna watu ambao wao nia yao ni kuharibu, sasa yanakuja mashirika ya nje, mashirika binafsi na huku tutakuwa na shirika letu, kuna watu ndani humo humo watakuwa wanahujumu hili shirika letu na mimi nashukuru kuna kipengele kimesema Waziri uwe unatuletea taarifa tuone maendeleo.

Kwa hiyo, tuepukane jamani na adha hii, tumekwishachomwa mno na miba, mikataba mibovu iko mingi, sasa hebu hii sheria ndiyo iwe mkombozi kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kuunga mkono hoja na niwatakie kazi njema Mheshimiwa Ngeleja na msaidizi wake na watendaji wote. Wale ambao wanaona wanapwaya waachie ngazi mapema. Naunga mkono hoja hii mia kwa mia. (*Makofi*)

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuongea kwa sababu asubuhi wakati jina langu limeitwa nilikuwa kwenye shughuli za Kamati ya Huduma za Jamii na hivyo nikawa nimekosa hiyo fursa na kwa utaratibu uliokuwa umepangwa ni kwamba basi jina langu lilikuwa ndiyo hivyo limekwishapita.

Baada ya hapo naomba nianze kwanza kabisa kwa kusema kuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja kwa sababu zifuatazo:-

Samahani! Kwanza naomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Watendaji wote wa Wizara ya Nishati na Madini na wale wa Shirika la Umeme la *TANESCO* na Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Maji, Nishati na Umeme *(EWURA)* na wakala wa umeme na nishati vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwasahau Waheshimiwa Wabunge ambao kwa hakika kwa muda wote huu toka ulivyoanza mchakato wa kuujadili Muswada huu

wameweza kuuboresha hadi kufikia hatua hii ambayo imetuwezesha hata sisi wengine kukubali kwamba ni muhimu tukaupitisha bila kuupinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme moja kwa moja kama nilivyosema naunga mkono Muswada huu kwa sababu ndiyo pekee utakuwa mkombozi kama ukitungwa ukawa sheria hasa hasa kwa jimbo langu la Mbozi Magharibi kwani ni wazi bila huu Muswada kupitishwa hakuna uwezekano wa jimbo hili kwa ujumla na hata wilaya ya Mbozi yenyewe kupata umeme.

Kwa uchache kabisa ni kwamba Wilaya ya Mbozi yenyewe hadi hivi sasa pamoja na kuwa na vijiji zaidi ya 250 ina umeme kwenye vijiji visivyozidi 10 ambavyo kati hivyo ni viwili tu viko upande wa jimbo la Mbozi Magharibi.

Sasa katika hali kama hii itaichukua Wilaya ya Mbozi miaka 960 kuweza kupata umeme kwa vijiji vyake na italichukua jimbo la Mbozi Mashariki miaka 720 kuweza kupata umeme wake na kwa upande wa Jimbo la Mbozi Magharibi itachukua miaka 2400 ndipo vijiji hivi bila hata kuongeza viweze kupata huo umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hiyo kama *source* ya umeme itakuwa ni hii inayotegemea chanzo kimoja kwa kweli hakutakuwa na uwezekano wa kuwa na maendeleo.

Napenda tu niseme kwa uchache kabisa ile miaka ya 60 ama baada ya uhuru kwa vile vijiji vyetu vyote vipatavyo 200 katika wilaya ya Mbozi vilikuwa havina umeme. Vijiji vingi vilikuwa na wakazi wapato 3000 hivi.

Baada ya hapo kutokana na mabadiliko ya maendeleo na kusambazwa umeme sehemu mbalimbali tumejikuta watu wetu wakijazana katika vijiji visivyozidi vinne.

Kwa mfano, Tunduma ambayo hivi sasa kwa sensa ya mwaka 2002 inadaiwa ilikuwa na wakazi 34,000 lakini nataka kuwahakikishieni ukapita hapa mchana utakuta watu wasiopungua 300,000 japo kwa uchache na labda kwa kuwa watu wanarudi sehemu mbalimbali, usiku wanakuwa 100,000.

Sasa katika uongezekaji huo wa watu ni kwamba, ifikapo miaka 10 au 15 ijayo, jimbo langu la Mbozi Magharibi ambalo lina watu wapatao 250,000 litakuwa kule vijijini hakuna watu; watu wote watakuwa wamesongamana Tunduma kwa sababu ya kutafuta maendeleo. Hii ni kwa sababu huko kwingine ambako kwa wakati huo kulikuwa na

wafanyabiashara wakubwa, waliokuwa wakitumia majenereta, kwa hivi sasa kutokana na matatizo ya Nishati kwamba, mafuta yamepanda, wote wamekimbilia kwenye hiyo miji ya Mbeya, Tunduma ama Vwawa, Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo ni tegemeo letu kwamba, vijiji hivyo vitabaki havina watu, kwa sababu kule vijijini hakuna maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo ninaamini kabisa kwamba, Muswada huu umeletwa kwa wakati na maboresho ambayo umefanyiwa, yamefanywa moja kwa moja. Niungane na wenzangu kwamba, huu ni wakati muafaka wa kupitia huu Muswada kwa sababu ni kutokana na hilo, tutawawezesha wale wawekezaji binafsi kuweza ama kusambaza au kuanzisha vituo vya umeme kwenye vijiji vyetu, ambavyo mpaka hivi sasa viko gizani. Madhara ya giza kama tulivyosema ni ukosefu wa maendeleo na wale wanavijiji hivi sasa wanajitayarisha kulala na kama ni watu wazima *definitely,* kesho lazima wameongeza watu wengine na sisi tunaongea juu ya *population control* ambayo kwa wanavijiji itakuwa ni ndoto.

Kama hatuwezi kuwapelekea kitu cha kuwafanya washughulike zaidi ya ule muda ambao wamezoea wanalala kama kuku saa 12 ni lazima wazaane, hatuwezi kuwalaumu. Hivyo basi, ili tuwe na maendeleo ya uwiano, tunaomba Muswada huu kwa hakika upitishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuendelea zaidi, kwa sababu nina hakika yale yote waliyoongea wenzangu, ndiyo hayo ambayo hata kwa Mbozi na Mbozi Magharibi yana ukweli. Kwa hiyo, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja moja kwa moja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr. Luca J. Siyame na hasa kwa kuweka msisitizo wa ziada kuonyesha ni namna gani umeguswa na Muswada wa leo.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba nimuite Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu. Kwanza, ninaomba nitoe pongezi za jumla kwa walioandaa Muswada huu, nikianzia na Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Watendaji wote na Wabunge wa Kamati, ambao kwa kweli wamejitahidi kutuwekea mambo haya sawasawa tukaelewa; pamoja na kwamba, nilikuwa sielewi kabisa, nilifikiri *TANESCO* itabinafsishwa lakini kumbe mambo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nitoe shukrani za dhati na pongezi kwa Mheshimiwa Rais, kwanza, kwa kumteua Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir na kuongeza uwakilishi wa Wabunge wa watu wenye ulemavu ndani ya Bunge la Jamhuri. *(Makofi)*

Kwangu mimi nimefarijika, kwa sababu ameniongeza nguvu na uwezo ambapo nitashirikiana naye moja kwa moja, kwa masuala ya undani kabisa ya walemavu. Kwa hiyo, kwa kweli ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Rais tena, kwa jinsi alivyoonyesha dhamira ya dhati katika kutokomeza mambo yanayotokea hivi sasa ya mauaji ya *albino* kutokana na ushirikina; sijui umezuka dakika ngapi kwamba ndiyo mtindo wa kupatia fedha! Tanzania inaharibika, sijui tunakoelekea lakini Mheshimiwa Rais, amelivalia njuga akisaidiwa na Watendaji wake *(RPCs),* katika Mikoa husika. Ninadhani jambo hili taratibu na kwa pamoja tutaweza kulimaliza.

Ila hapa nitoe rai kwa sisi wenye ulemavu kwamba, tuungane na wananchi wengine, kujaribu kutoa taarifa kwa yale yote ambayo yanaweza yakatokea katika vyombo vinavyohusika, wala tusiwe na woga kwa sababu Serikali ipo pamoja nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyaeleza hayo, niende kwenye hoja yenyewe; ninaomba ieleweke kwamba, udhibiti wa mashirika ya umma yote yanayotoa huduma katika nchi yoyote ile ni muhimu sana. Hii ni kwa sababu, kutokana na udhibiti huo, ndipo wawekezaji au watendaji ambao mahali ambapo walifikiria hawawezi kutenda kazi kwa sababu ya kutokuwa na faida kutokana na udhibiti, wanaweza wakaelekezwa kufanya hivyo.

Mimi ninaona ndiyo Muswada huu unakotupeleka kwamba, umeme utasambazwa kwa maelekezo ambayo mengi yamekwishasemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo basi, mimi niseme moja kwa moja ninaunga mkono kabisa Muswada huu kwa sababu umetoa ruhusa ya kwamba, wawekezaji binafsi wanaweza wakawekeza katika sekta hii. Wenzangu wengine wameshafafanua, wawekezaji wataweza kutengeneza vifaa vya kuweza kuwarahisishia kazi ili wananchi waweze kupata umeme. Ruhusa hii imetolewa kwa sababu *EWURA* ndiyo itakayokuwa mdhibiti mkuu wa kuangalia masuala haya yanavyokwenda. Hayo yamesemwa sehemu ya nne na mabano yake (1)(c) huko na vifungu viko hapa.

Kwa hiyo, ninaamini kutokana na *EWURA,* ambayo tuliipa meno baada ya kubadilisha kidogo vipengele vya Sheria hii kwamba, *EWURA* ikishirikiana na Serikali au na Waziri, wataweka mipangilio mizuri ili umeme kweli uweze kuwafikia wananchi hasa vijijini na ndivyo Sheria hii ilivyosema kuanzia kifungu cha 37 – 39, mambo hayo yanajieleza. Kingine ambacho kimenifanya niunge mkono hoja hii ni kwamba, *EWURA* inapaswa kuendelea kulinda maslahi ya wote watakaonunua umeme; na kwa sababu sheria imeruhusu kuwa na wawekezaji wengi. Umeme huu hatimaye utaweza kupatikana kwa bei nafuu, kwa sababu hapa *economies of scale* ndizo zitakazofanya kazi kwamba, kwenye ushindani mkiwa wengi, yule atakayepandisha bei watu hatutakwenda kununua kwake tutakwenda kwa yule aliyeshusha. Kwa hiyo, hata yule anayepandisha bei hatimaye itabidi ashushe kwa sababu ya maendeleo ambayo yanaweza yakawepo.

Kwa hiyo, kwa sababu mmegusia vijijini, ninashukuru sana kwa sababu ninasema wakati wa ukombozi wa matatizo ya umeme ndani ya Tanzania ni sasa hivi. Akina mama waliokuwa wanahangaika kupika na kuni mbichi na macho yakawa mekundu,

huenda sasa ukombozi utawafikia, kwa sababu kama umeme utafika vijijini wataweza kuutumia kwa urahisi.

Hapo tu labda niiombe Serikali, vifaa vile vya kupikia vya umeme hapo baadaye hakikisheni vinashuka bei ili umeme huu vijijini uweze kuwasaidia akina mama wengi katika mapishi na shughuli zao ndogondogo; achilia mbali ukuzi wa viwanda na mambo mengine kadha wa kadha, ambayo yanaweza yakaletwa kutokana na maendeleo hayo ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi katika ibara ya 41 na ibara mpya ya 7; Muswada hauruhusu wawekezaji wa sasa kuja kuchukua leseni au kuja kuomba leseni kwa sheria hii mpaka miaka mitano ijayo. Mimi hapo ningependa kufahamu; hivi ni kwa nini; je, miaka mitano si muda mrefu sana wa kumpa mtu adhabu kwa sababu sielewi kama ni adhabu au watakaa miaka mitano ili waendelee kuangaliwa hawa wa sasa, ambao wengi wametuweka katika matatizo mengi au ni kitu gani hicho? Ningeomba nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimependelea tena kuunga mkono hoja hii, kwa sababu Muswada unaruhusu au umeeleza wazi kwamba, wawekezaji wajao hao hawatakuwa na mambo ya *capacity charges*. *Capacity charges* ndiyo ilikuwa njia mojawapo ya ulaji, sasa kwa sababu ulaji huu umekatika, ninashukuru sana kwa sababu pia ilikuwa ndiyo moja ya chanzo kilichokuwa kinaleta mzigo wa umeme kuongezeka bei. Kwa hiyo, kwa walaji kushindwa kumudu kutumia umeme kwa raha. Kwa hiyo, mradi hiki kipengele hakipo na wala hakitakuwepo, hii ni shukrani kwa Serikali kwa sababu hapo ndiyo ule ukombozi unapoendelea kuwepo; umeme huu unatarajiwa kutumika vijijini hata kwa wale wananchi wenye vipato vya chini na ndiyo maana ya maendeleo.

Angalieni wa chini anavyoinuka; akiinuka yeye ndipo utakapoweza kupima maendeleo siyo wa juu. Wenzetu walioko vijijini ni wengi zaidi kuliko walioko mijini. Kwa hiyo, nimeshukuru sana na hilo ndilo ambalo limenivuta niweze kushawishika kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu umeme sasa unaweza ukatolewa na wawekezaji wengi tu kutokana na huu Muswada, ninaomba wawekezaji hao wawe watundu kidogo wa kubuni. Nimepata taarifa ya juu juu kwamba, wenzetu kwa mfano Nigeria, umeme umewekwa hata kwenye nyumba zao za nyasi. Watu wana umeme kwenye nyumba za nyasi; kuna teknolojia mpya inayotumia *ready boards,* sasa mimi siifahamu, lakini nimeipatapata hiyo. Wawe na utundu kusudi wananchi wetu wa vijijini watakaoshindwa kumudu kuweka mabati na kadhalika, hizo sheria *complicated* hizo kuna uwezekano wa kuweza kusaidiwa hata kwa teknolojia hiyo, pamoja na kwamba, lazima tuwahimize kujenga nyumba bora.

Ninaamini wataweza, kwa sababu kutokana na umeme huo watajiendeleza, fedha watakazozitumia basi kidogokidogo unabandua nyasi unaweka bati, *eventually* unakuta nyumba yako tayari ina bati na inakidhi yale mahitaji ya kisasa ya kuhusu umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wenzangu wamezungumza, mimi kwa kweli ni kuunga mkono, kwa sababu kuna wawekezaji ambao tumetajiwa hapa wanatoa umeme katika maeneo yao na mengi nimeona kama ni vijijini. Sheria hii ikipita na wale wakapata *go ahead* ya kutanua *production*, nina hakika Serikali itasaidiwa kabla hata hatujapata hao wakubwa. Hao wadogo waliopo, kwa Sheria hii wakiruhusiwa, umeme utafika katika maeneo yale ambayo yanatarajiwa kufika na ni vijiji vyote, vitongoji vyote na mitaa yote, nchi itakuwa na mwanga. Wenzangu wamesema tatizo la giza ni kuongezeka kwa hatari ya kushambuliwa na mambo mengi tu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja tena na tena. Muswada upite na kazi ianze. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi jioni hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Kwanza, niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kuwasilisha Muswada huu Bungeni. Kabla sijasahau, niseme ninaunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kama Serikali inakumbuka, imechukua muda kidogo mpaka kufika hapa Bungeni, pamoja na semina mara mbili tulizozipata. Hoja kubwa ilikuwa tunahakikisha *TANESCO* inabaki mikononi mwa Serikali kwa asilimia kubwa, hilo ndilo la msingi. Hatutakuwa tayari kuona *TANESCO* inapewa watu wengine, Serikali inakuwa haina asilimia kubwa katika kudhibiti suala la umeme nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema kwamba, hakuna nchi yoyote duniani hata huko Amerika, ambayo wameweza kuachia Shirika la Umeme likawa huru kabisa au holela; ni lazima mkono wa Serikali uwepo katika Shirika la *TANESCO.* Sasa fanyeni mtakavyofanya, lakini hakikisheni kwamba, Serikali ndiyo ina kauli kubwa katika masuala ya umeme nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* pamoja na *assets* zake zote, haiwezi ikalinganishwa na wawekezaji wengine watakaokuja na kupewa uwekezaji katika mambo mengine ya kuzalisha umeme au kufanya shughuli za *transmission* au *distribution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa sababu tukitaka tufaidi vizuri suala la umeme, ili kuwapa nafuu wananchi ni lazima tuwe na miradi mikubwa. Tunafahamu sasa hivi kuna matatizo ya mafuta, tujitahidi kadri inavyowezekana tupunguze matumizi ya mafuta katika kuzalisha umeme ili kuleta unafuu kwa mlaji wa mwisho. Ni vyema wawekezaji watakaokuja nchini, wapewe miradi mikubwa ya *hydro*. Mfano, tuna Mradi wa *Stiggler's Gorge,* leo ni zaidi ya miaka 30, mradi ule umefanyiwa uchunguzi na michoro na kila kitu, lakini umeshindwa kutekelezwa kwa sababu ya gharama. Tena kwa wakati ule mradi ule ulikuwa unagharimu *500 million dollars* na leo ni mabilioni ya dola. Sasa ni vyema mkatafuta mwekezaji aweze kuwekeza katika *hydro*

kama ile, kwa sababu hata akisema anaondoka hawezi akaiondoa *hydro* pale, itabaki Tanzania milele na milele. Hiyo ndiyo miradi ambayo sisi tunaona kwamba, Serikali iingie na wawekezaji katika kutekeleza miradi mikubwa kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka pale Msumbiji kuna Cabora Bassa imejengwa na Serikali ya Ureno, mpaka leo mkataba ule wanaikabidhi Msumbiji, lakini imebaki Msumbiji inapeleka Umeme Afrika Kusini karibu *megawatt* 2000 zinakwenda Afrika Kusini, Serikali inapata kodi ya kutosha kwa hiyo ni kitu cha kudumu.

Sasa *Stiggler's Gorge* ni moja ya miradi ambayo ninaiomba Serikali iwatafute wawekezaji kama hao waje wawekeze. Tuingie mikataba muhimu sana ya kuwekeza katika mambo hayo, tuondokane na masuala ya mafuta. Sasa tunayo gesi, makaa ya mawe tunayo na miradi hiyo tayari imekwishaanza.

Mimi nitoe mfano mzuri ambao Serikali sasa hivi na *TANESCO* mmefanya mkataba na ile kampuni inayozalisha umeme kule Mtwara, hakuna *capacity charge.* Walikuwa wanatumia lita za mafuta 30,000 au sijui 30,000,000 kila siku. Leo kwa kutumia gesi, gharama zake zimeshuka mpaka milioni 13. Sasa na yule mwenye mashine zile kama hakuzalisha halipwi, hiyo ndiyo mikataba mizuri, lakini umezalisha au hukuzalisha ni lazima utulipe, hatuendi. Hii mikataba mingine ambayo imeiingia Serikali au *TANESCO* ambayo sasa hivi inawaumiza wananchi, kwa kweli ninasema kwa mara ya pili; Serikali ifanye juu chini, itafute hata mchawi, lakini ifute hii mikataba kwani itawaumiza wananchi milele na milele. Hata mkisema kwamba, Serikali ndiyo itachukua madeni ya *TANESO,* bado pesa za Serikali ni pesa za wananchi, ndiyo zile zile. Kwa hiyo, hakuna jinsi, mikataba hii nimeiona jana *TANESCO* kwamba, Serikali imekataa ile kesi iliyoko Mahakamani kule kati ya Serikali ya Tanzania na *IPTL.* Tuweke misimamo kama hiyo, tuchunguze mikataba yote na tuondokane na suala zima la mashine ambazo zinatumia mafuta; sasa hivi tuna gesi tuitumie. Mikataba ya kuchimba gesi kama *Songas,* tuitazame vizuri ili tuweze kuitumia gesi yetu kwa manufaa ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa hapa ninataka kusema kwamba, kinachorudisha nyuma nchi hii ni tariff ya umeme. Maendeleo yetu hayaendi kwa sababu *tariff* ya umeme ni kubwa mno katika Bara la Afrika; ninafikiri sisi ni wa pili kwa *tariff* iliyokuwa kubwa kati ya senti 9 -10. Utawezaje ku-*compete* katika viwanda; utatengeneza bidhaa nzuri za aina gani na utauza kwa bei gani na utamuuzia nani wakati Afrika Kusini *tariff* ni senti 2 – 3? Hatuwezi tukafika pahala tukasema kwamba, tuna maendeleo sasa Tanzania kwa kigezo kimoja tu cha *tariff* ya umeme. Sasa kila mkipandisha, anayeumia ni yule mlaji wa mwisho au ni mwananchi, iwe ni kiwanda au iwe ni kitu chochote kitakachowahudumia wananchi. *TANESCO* tengenezeni *formula* mhakikishe kwamba, *tariff* ya umeme inashuka kwa kuzingatia kwamba, sasa hivi tuna gesi na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie hii *REA* (Wakala wa Nishati Vijijini); leo *TANESCO* imefika pahala inashindwa kununua *transformer*, inashindwa kupeleka umeme vijijini! Kumbukeni kuna miradi ya maendeleo ambayo Serikali imeipitisha katika bajeti, nichukue mfano, Mradi wa Maji au Miradi ya Maji inayofadhiliwa na

*World Bank* na miradi mingine ya *Quick Wins,* inashindwa kufanya kazi kwa sababu hakuna *transformer*. Sasa hivi *TANESCO* ikitaka kununua *transformer* ni lazima ipate kibali kutoka *EWURA.* Jana nimepigiwa simu, nina miradi minne ya maji tunataka *transformer,* tunaambiwa *EWURA* mpaka itoe kibali, lakini nimeshauriwa nizungumze na Serikali, tuingize katika Mpango wa *REA* ndiyo nitapata hizi *transformer.*

Hivi *TANESCO* tumeifikisha pahala mpaka inakuwa na hali kama hii? Yote hii imesababishwa na kuipa madeni makubwa, kutokana na mikataba ambayo tumeingia, ambayo haikuisaidia *TANESCO* na Serikali haikuchukua mzigo huo imewaachia *TANESCO;* sasa mimi niseme bado iko *ICU.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *PPRA;* kuna tabia ya mikataba mikubwa na kuna watu ambao hawaipendi nchi hii, mradi ule hauwezi ukatekelezwa kama hakupata mgao wake kwa sababu yeye ndiyo *desk officer* na ndiye mshauri mkuu na ndiye anayasikilizwa, akikataa yeye basi ule mradi utakwama, kwa sababu amekosa mgawo wake wa asilimia kumi. Mradi unakufa kifo cha kawaida kabisa.

Sasa ninasema hizi Sheria za *PPRA* zitazamwe upya, tuweze kudhibiti hali kama hiyo. Tunajua mradi ni mzuri na ni *viable,* utaleta manufaa kwa wananchi, hatimaye unakufa kimya kimya; tutashangaa kuja kuambiwa bwana kuna asilimia kumi haikutoka; nani sasa hatutajani! Huo ndiyo ukweli, haiwezekani miradi hii mizuri ambayo inakuja kwa manufaa ya nchi yetu halafu inakufa kimyakimya, siyo miradi ya umeme peke yake; utakuta kuna miradi ya kujenga madaraja, barabara. Tuipe meno Serikali iingilie kati kuona uwazi unawekwa kuhusu miradi. Endapo kuna mradi mzuri halafu unakataliwa; ni sababu zipi? Sasa hivi wamefungwa na Sheria hawawezi kuingia huko, lakini ninafikiri itafika mahali itabidi turekebishe kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wengine wanasema hili suala la *Richmond* limefanyika haraka haraka, inawezekana kuna mtu *TANESCO* hakupata asilimia kumi yake ndiyo maana limeibuka haraka sana, lakini ingekuwa na yeye kapata mgawo, pengine wala tusingejua kuna matatizo gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninataka kusema kwamba, hawa wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika suala la umeme, ninakubali tu kwamba, wawekezaji wadogowadogo wasipate nafasi miradi yao kuingia katika *Grid* ya Taifa mpaka iwe imefika kiwango kikubwa cha uwekezaji. Niseme mfano, labda mtu anawekeza kwa ajili ya kuzalisha *megawatt* 100, hapo anaweza akaruhusiwa akaingia katika *Grid* ya Taifa, lakini mtu anayazalisha *megawatt* 50, 20 au hata *megawatt* moja, halafu huyo mumruhusu aingize umeme wake huo katika *Grid* ya Taifa, ninafikiri kitaalam siyo sahihi. Tutafute wawekezaji ambao miradi yao tunaweza tukaiingiza katika *Grid* ya Taifa, lakini kuwe na kiwango maalum kuanzia labda *megawatt* 100 ili tumwingize katika *Grid* ya Taifa la sivyo tunaweza tukaleta matatizo ya kukatika kwa umeme mara kwa mara, kwa sababu ya mitambo midogomidogo ambayo imepata hitilafu, ikasababisha ku-*trip grid* nzima ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na hayo ya kusema, ninasisitiza tu kwa mara ya mwisho, Serikali tafadhalini tutakuja kuhukumiwa na vizazi vyetu kama mtaiachia *TANESCO* iende kiholela na kila mmoja akija hapa, basi Serikali isiwe na mkono wa kudhibiti umeme katika nchi hii tutaumia vibaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitangulie tu kusema kwamba, Muswada huu ninauchangia nikiwa na hasira na uchungu sana. Ninasema hivyo kwa sababu nimeshiriki kupitisha Miswada mingi, ambayo haina msaada kabisa kwa wananchi. Kwa hiyo, ninaona kwamba nina mzigo mkubwa, kwa sababu nimepitisha Miswada ambayo haikuwasaidia wananchi, bali imekuwa ni mzigo kwa Taifa hili.

Ninapenda pia kutaja machache; hapa tuna Wabunge ambao bado wana matumaini na wengine ambao hawana matumaini kabisa kama mimi. Tulipitisha hapa Muswada wa *Net Group Solution* na Serikali hii hii imeleta Muswada, ikapiga kampeni kama inavyofanya leo hapa. *Net Group Solution* imegeuka ikawa *Net Group Problem* kwa nchi hii. Niambieni kama *Net Group Solution* imepeleka umeme katika kijiji chochote na mniambie ni vijiji vipi?

**MBUNGE FULANI:** Hakuna!

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Ilichofanya ni kuchota fedha za wananchi, ikawa ni kilio; hatukupata umeme kwa *Net Group Solution.* Kwa hiyo, hilo ni jambo moja ambalo ninaliona ni mzigo mkubwa kwangu, nimeshiriki kupitisha Muswada ambao haukuwasadia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada mwingine ni wa Umeme Vijijini. Mwaka 2005, tulipitisha Muswada wa Umeme Vijijini, Serikali ikaweka Sh. 10bn/=. Ninasema ni Muswada wa Msabaha, yeye ndiye ameleta Muswada huo, tukaupitisha, mpaka leo sikusikia kama umeme umekwenda vijiji vipi kutokana na hizo Sh. 10bn/=. Kwa hiyo, ninaona nina mzigo ambao Muswada tulioupitisha tukidhani kwamba utawasaidia wananchi kumbe haukuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopitisha Miswada hapa, Serikali inakwenda kukaa na kuunda mikataba pamoja na wawekezaji; mikataba inayotengenezwa inalinda upande mmoja na kuumiza upande mwingine wa wananchi. Mara nyingi sana inasaidia upande wa wawekezaji. Serikali ikitaka kuvunja mkataba wanasema ohoo, tutaingia kwenye hasara kubwa, mtu anayeingia hasara ni mwananchi. Kwa mfano, Mkataba wa *IPTL,* ambayo tunalipa mabilioni ya fedha, Serikali imeshindwa kuuvunja. Mikataba mingine sisi tunashiriki kupitisha Muswada tu, lakini mikataba inafanywa siri kubwa sana tusiione. Kuna hii kampuni inayoitwa *DOWANS,* tumekuja kuisikia baada ya

matatizo; hivi jamani nani alishiriki kuipitisha *DOWANS*, wanalipwa Sh. 152m/= kwa siku; mmeshiriki?

**WABUNGE FULANI:** Hatujashiriki.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Kesho yakiletwa tena makampuni mengine yaandikiwe mikataba kama hiyo, itakuwa tumefanya nini. Kuna mikataba ambayo inanipa uchungu sana nikifikiria kwanza MEREMETA, ilikuwa inaletwa na Waziri wa Ulinzi tu ndiye alikuwa anatupa taarifa ya kusema kwamba ni Mradi wa Jeshi; Jeshi ni la nani? Kwa hiyo ni mambo makubwa tunayofanya na kupitisha hapa na mengine hayapitishwi, yanaletwa kinyemela kama MEREMETA, hatujawahi kuijadili hapa. Mimi sijui Mikataba wa Benki ya *NBC* na *NMB* tuliyoipitisha kama ina manufaa, lakini ninategemea kwamba, benki hizo nazo zina mikataba; sasa sijui ni mikataba inayolinda wananchi au wawekezaji? Ninaomba tuunde Timu au Tume ya Bunge, Waziri wa Nishati na Madini akienda kukaa na kupanga mikataba inayotokana na Muswada huu, basi hiyo Tume iangalie kama ina manufaa kwa wananchi na hiyo Tume itokane na Bunge au tuseme Kamati Ndogo ambayo itaangalia masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia *TANESCO*; jamani *TANESCO* wamefanya kazi kubwa sana, wasingeweza kusambaza umeme vijiji vyote vya Tanzania huku wamebebeshwa mizigo mikubwa ya kulipa madeni. Kwanza, Serikali yenyewe inatumia umeme na hailipi bili na ndiyo watumiaji wakubwa halafu huku wamewekewa mikataba ya ajabu ya kuwalipa watu kwa mitambo yote inayoletwa, tena inayoletwa kwa mikopo. *TANESCO* ndiyo inalipa mikopo, ninashangaa na ninawahurumia sana. Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema *TANESCO* ipewe nguvu ili iweze kuhudumia, hakuna chombo chochote kinachoweza kuwahudumia wananchi isipokuwa *TANESCO*. Baadaye nitazungumzia Jimbo langu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona *REA* ndiyo imekuja kuingia sasa badala ya ule Mfuko wa Umeme Vijijini, wanasema Mfuko wa Msabaha. Walipokuwa wakinadi hapa Bungeni, waliorodhesha vijiji vyote vilivyoko Tanzania kwa awamu tatu *(phase one, phase two and phase three)* na *phase three* ilikuwa wapate umeme mwaka 2010, lakini sasa imegeuka tunaanza upya, ndiyo imekuja kuundwa *REA,* kipindi chote cha miaka mitatu iliyopita hakuna kilichofanyika. Kwa hiyo, ninaomba huo Mfuko ukipita usikae miaka mitatu halafu mje kutuletea kitu kingine tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ukipita njiani ukimwona nyoka mkubwa, siku nyingine ukifika pale utaanza kutazama kama utamwona kwa sababu umeogopa eneo lile na sisi sasa tumeanza kuogopa Miswada mnayoleta hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani Peramiho umeanza kuipigia debe au kuipigia kelele mwaka juzi, mimi nimepiga kelele hapa Bungeni kwa miaka kumi na tatu. Kila Waziri aliyepita katika Wizara hii aliahidi kwamba, Longido nitapata umeme; alianza Mheshimiwa Dr. William Shija, akaja Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, akaja

Mheshimiwa Daniel Yona, akaja Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, akaja Mheshimiwa Mustafa Karamagi na sasa ni Mheshimiwa William Ngeleja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Mkapa amekwenda Namanga akasema, lazima umeme utafika, haiwezekani Namanga Kenya wakawa na umeme sisi tukawa giza. JK amekwenda juzi akasema, lazima umeme ufike Longido kwanza, hatuhitaji fedha za wafadhili, umeme kutoka Namanga hadi hapa Longido ni fedha chache sana ni Sh. 700m/= na mimi ndiyo nitakuja kuuzindua umeme hapa, amemwambia Mheshimiwa Karamagi na Mheshimiwa Ngeleja na wewe unasikia. Nimelia kwa miaka kumi na tatu sijapata umeme, ndiyo maana ninasema sina matumaini tena ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewaambia wananchi wangu ikifika mwaka 2010 kama umeme hauji Longido sigombei, hicho ni kitu ambacho nimekwisha watangazia. Kwa hiyo, ningeomba kusema kwamba, tuna tatizo kubwa sana kwa sababu kila mkataba unaopitishwa na Serikali, ufisadi umo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ufisadi ndiyo umeiua nchi, kwa sababu kila mkataba ni ufisadi mtupu. Mheshimiwa William Ngeleja wewe bado ni msafi, lakini tunategemea mikataba ijayo inayotokana na Muswada huu, ndiyo itakuletea shida. Kwa hiyo, ndugu zangu, wananchi wamepoteza imani kabisa kutokana na ufisadi huu, hawana imani tena; kwa sababu mikataba yote inayopitishwa inawalinda wawekezaji kuliko wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninapenda kusema kwamba, ninaunga mkono Muswada huu, lakini ninaomba mikataba yote iangaliwe upya. Ninaomba Timu au Kamati ya Bunge hili ishirikishwe kuangalia mikataba inayopitishwa, tusije kuletewa tena mikataba kama hii ya *DOWANS*, *IPTL* au MEREMETA ambayo haijulikani ni ya nani mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu ulio mbele yetu. Pamoja na kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na kwa hiyo maoni ya Kamati yaliyosomwa asubuhi ni mdau wa maoni hayo, lakini kwa sababu Waziri mwenye Wizara hii na Naibu wake ni wadogo zangu na marafiki zangu, nimeamua nichangie ili kuwapa nguvu kwa sababu ninaamini kwamba, huu Muswada umekuwa mtihani mkubwa sana kwao na wameshinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niongelee huu Wakala wa Umeme Vijijini. Wakala wa Umeme Vijijini umekuwepo kwa Sheria ya Bunge ya Mwaka 2005, kama walivyosema wenzangu wengi na mapato yake yanatoka kwenye mgawo wa bajeti na pia kwenye tozo. Sasa kwenye mgawo wa bajeti, katika bajeti ya mwaka huu wa sasa wamepangia Sh. 10bn/=, hizi fedha ni kidogo sana, ninaomba Waziri mwenye dhamana aongeze mgawo huu ili angalau wakipata Sh. 20bn au Sh. 30bn/= wanaweza kupeleka umeme kwenye vijiji vya kutosha. Vilevile kwa Sheria ya *REA,* wanatakiwa wapate

mapato kwa tozo, yaani wale ambao wana umeme mijini, waweze kuchangia mpaka asilimia tano ili umeme uende vijijini. Sasa hilo lipo kwenye sheria lakini mpaka sasa halijatendeka. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, hilo tozo mambo yakiwa shwari au kasheshe za akina *Richmond* zikishapoa, tozo ianze ili ambao tuna bahati tuko mijini, tuchangie umeme kwenda vijijini. Vijiji ni vingi sana nchi hii na vyote vinahitaji umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo njia nyingine ya kupata tozo ya kuweza kupeleka umeme vijijini; ninataka niongelee makampuni ambayo hayalipi kodi, ninayachagua makampuni mawili, matatu ambayo hayalipi kodi. Yapo makampuni ambayo ni makubwa lakini yanalipa kodi kidogo sana, kwa ujanja wao mwingi sana ambao nitauelezea. Makampuni haya ni makampuni ya simu za mkononi, yanalipa kodi kidogo sana, ukilinganisha mapato wanayopata na kodi wanayolipa inachefua. Kwa hiyo, makampuni yote ya simu za mkononi hayalipi kodi ya kutosha, kwa ujanja ambao nitauelezea lakini yapo ambayo hayalipi kodi kabisa kwa mfano, Kampuni ya *Coca Cola* hailipi kodi kabisa kwa kutumia ujanja huu huu ambao nitauelezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, wanatumia *weaknesses* za sheria zetu. Sheria yetu ya Kodi imeruhusu *depreciation rate* imekuwa kubwa mno; kwa makampuni ya madini asilimia mia, kwa makampuni mengine *fifty percent.* Imeruhusu sheria yetu ya Kodi na huyo mtu akileta *capital equipment* yake, anapunguza kwenye *income statement* yake ile *fifty percent* anaipunguza kwenye *profit and loss* yake. Kwa hiyo, mwisho wa mwaka anasema mimi nina hasara bwana sikupata faida na kama hakupata faida ina maana hakuna kodi au anasema mwaka huu nimepata hasara na akiwa na hasara ana-*carry forward* mwaka unaokuja! Kwa hiyo, wanatumia ujanja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujanja wa pili, wanatumia *Sister Companies*; Kampuni ya Afrika Kusini au ambayo ipo Marekani inakuwa na kampuni ndogo hapa, anaagiza malighafi yote kutoka kwa *Sister Company* na akiagiza malighafi kule; wa kule wanai-*over invoice*, kwa hiyo huku ananunua kwa gharama kubwa na kwa hiyo anapata hasara lakini kule wanapata faida na kulipa kodi, huku hawalipi kodi. *(Makofi)*

Njia nyingine wanatumia *management fees*; *Sister Company* iko hapa, kwa hiyo,inabidi mlipe hiyo *fees* ya *management* na zinakuwa kubwa sana, kule wanapata faida wanalipa kodi, huku hawalipi kodi. Ninachoshangaa, kampuni hii iko hapa hailipi kodi miaka minne, mitano au sita; kuna wakaguzi siyo Mkaguzi wa Serikali, Makampuni ya Ukaguzi, anakaguliwa kila mwaka na apewa cheti safi wakati huyu halipi kodi, anapata hasara kila mwaka lakini anampa cheti safi!

Ninadhani ipo haja Wizara ya Fedha waangalie ili hawa wakaguzi waweze ku-*qualify*. Akifika pale, anaona mwaka huu wamepata hasara, mwaka kesho wamepata hasara, mwaka kesho kutwa wanapata hasara, a-*qualify statement,* anasema huyu *is not a going concern*, akim-*qualify* namna hiyo, mwaka kesho atapata faida ili na sisi tupate kodi. Kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali, iangalie haya makampuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema pamoja na ujanja wao wote wanaofanya kwa sasa, Serikali wapeni tozo angalau walipie umeme vijijini, wapeni angalau asilimia mbili haya makampuni ya simu kama walivyosema wenzangu au *Coca Cola* ili kusaidia angalau kupeleka umeme vijijini. Hii inawezekana, nimesoma kwenye mtandao nchi za Amerika Kusini kama mbili, tatu, zinafanya hivyo hasa kwa haya makampuni ya simu, wanawapa tozo za asilimia mbili, wanalipa na inasaidia kupeleka barabara na umeme vijijini. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, awasiliane na Mawaziri wenzake wa Fedha na wengine ili waweke tozo kwa makampuni haya ambayo aidha hayalipi kodi au yanalipa kodi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza itakuwa faida kwao, wakitoa tozo hiyo ya asilimia mbili umeme ukaenda vijijini, maana yake simu zao zinatumia umeme na tunataka kupeleka umeme vijijini, kwa hiyo, wao watafanya biashara zaidi. Umeme ukienda vijijini kwa sababu kutakuwa na mafriji mengi, wanavijiji watakunywa soda nyingi, watapata faida wao. Kwa hiyo, ninaomba sana tuweke tozo kwa makampuni haya ambayo hayalipi kodi ili yaweze kuchangia umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Wakala wa Umeme Vijijini, Jimboni kwangu kuna miradi ya umeme kwenda vijijini ambayo ina miaka minne au mitano, Wilayani kwangu siyo Jimboni kwangu. Kwenye Jimbo langu mimi kuna Mradi wa Umeme kutoka Makongorosi kwenda Lupa una mwaka wa tano sasa hivi nguzo zipo barabarani.

Kwa hiyo, ninaomba *REA* wauangalie sana mradi huo. Kuna Mradi wa Umeme kutoka Isenyela kwenda Sangambi, kuna Mradi wa Umeme wa kutoka Kiwanja kwenda Mlima Njiwa ni vijijini huko tena kuna wachimbaji, kuna Mradi wa Umeme kwenye Jimbo la kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Sigonda hapa, umeme kutoka Mkwajuni kwenda Galula, kuna Mradi wa Umeme kutoka Mkwajuni kwenda Kanga, kuna Mradi wa Umeme kutoka Mkwajuni kwenda Mbuyuni, yote hiyo ina miaka karibu mitano. *REA* ninaomba uiangalie kwa macho mawili na tunaomba uongezewe hela ili uweze kufikisha umeme vijijini kama ilivyosema Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo machache, hasa kuyaangalia makampuni ambayo hayalipi kodi yachangie umeme vijijini na Serikali kwenye bajeti tuiangalie *REA* badala ya kuipa vijisenti tuipe fedha ya kutosha ili ipeleke umeme Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi ya kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nipate kuchangia katika Muswada huu. Pia ninampongeza mtoa hoja (Mheshimiwa Waziri mhusika), kwa kweli ameufanyia kazi ya kutosha Muswada huu kwa kipindi kirefu, kwa uvumilivu wake mkubwa tu na hatimaye leo ameweza kutuwasilishia hoja hii. Nami kwa pamoja, ninaungana na wenzangu waliotangulia kwamba, nimesimama kwa lengo la kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu sasa utatupeleka katika sheria ambayo itakapokuwa imepita; itaifungua mipaka, itaondoa vipingamizi na vikwazo vingi

vilivyokuwa vinachelewesha ongezeko la watumiaji wa umeme katika nchi yetu. Kwa hali hiyo, ninayo kila sababu ya kusema Muswada huu ni mzuri, umekuja kwa wakati ambapo Watanzania katika utandawazi huu, wamekwishaelewa umuhimu mkubwa wa kuwa na umeme. Kwa hiyo, Muswada huu unakusudia kutoa nafasi kwa sekta binafsi, kuivutia ili iweze kuzalisha umeme, iusafirishe na iusambaze nchini. Vilevile Muswada huu utawezesha huduma hii kubwa iweze kuwa biashara nzuri tunayonunua sisi kama Watanzania, lakini vilevile nchi iweze kuuza umeme katika nchi jirani, ikiwa ni katika hatua za kisheria badala ya kutumia maelewano zaidi na kusainiana mikataba ambayo pengine ni maelewano ya urafiki zaidi. Hii mimi ninaipongeza, ninasema ni hatua nzuri ambayo kimsingi itaweza kuinua uchumi wetu na itaweza kutusaidia kuboresha hali ya maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiunga mkono hoja hii kwanza, kwa kuwatambua wale wazalishaji wa umeme wadogo wadogo, ambao walikwishaanza kuzalisha umeme kwa kipindi kirefu sana katika nchi yetu, wakiwemo wale wa Jimboni kwangu na wale wa Ndolage Hospitali. Wameanza kuzalisha umeme zamani, mimi ndiyo watu wa kwanza kuona umeme kwao kwa sababu ni eneo maarufu, kuna hospitali maarufu, watu wengi wa eneo lile la kwetu, ninadhani ndiyo tulipoanzia kuona umeme ukiondoa ambao labda walikuwa wanasafiri kwenda mbali zaidi. Kwa hali hiyo, kwa kuwatambua hawa na nimesikia wametajwa wengi Lindi, Tanga, Mtwara, basi ninaamini kabisa kwamba hii ni hatua nzuri na itawatia moyo kuweza kuzalisha umeme zaidi na kwa mujibu wa Muswada ni kwamba, hata hawa wawekezaji watakaokuja watambue kushusha umeme katika maeneo ambayo umeme unapita. Katika vile vijiji ambavyo umeme unapita, badala ya *TANESCO* ilivyokuwa inafanya, inarusha umeme watu wanaumia, wanaona nyaya zinapita lakini hawawezi kufaidika na umeme huo wa karibu yao. Pia kipengele cha kwamba watatoa huduma za kijamii katika maeneo yao ni vipengele ambavyo ninasema Muswada huu ni wa kipekee katika Miswada mingi ambayo tumewahi kuipitisha; umekuwa wa kuangalia watumiaji mno kuliko mingine ambayo mara nyingi inaangalia wawekezaji, kwa hiyo ni Muswada mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda niipe changamoto *TANESCO*, Ibara ya 41(6) na (7), zimeongezwa makusudi baada ya mjadala mkubwa sana kati ya Wabunge na Serikali kwamba ni lazima *TANESCO* ilindwe. Ninachotaka kusema ni kwamba, *TANESCO* isibweteke, kwa sababu tayari Muswada huu itakapokuwa sheria, inaingia ndani ya ushindani. Sasa ushindani huu utakuwa ni kati yake na makampuni mengine binafsi, ambayo nayo yatakuja kuonyesha uwezo wake japokuwa *TANESCO* itakuwa ya kwanza kupewa nafasi, lakini makampuni mengine yananyemelea kuona kama imeweza.

Sisi wapokea huduma tunaiangalia kama *TANESCO* imeweza. Hatutakaa kimya kuona *TANESCO* imeshindwa, kwa sababu tu tunailinda kisheria, hapana. Tutaomba sheria hiyo irudi tuifumue ili tuweze kutoa nafasi kwa wengine, kwa sababu tunachohitaji ni huduma nzuri ya umeme kwa Watanzania wote, mmoja mmoja, vikundi na viwanda. Tunataka kuona uchumi unakwenda mbele. Kwa hiyo, hii nafasi ambayo *TANESCO* imepewa sasa, iitumie kwa faida kubwa sana, wenzangu wamesema ifumuliwe, wenyewe watajiangalia na Serikali wataangalia kwamba; je, tumeipa *TANESCO* nafasi lakini pia

tumekaribisha wengine, tutaendelea kuibeba kwa muda gani, kwa sababu haitaendelea kubebwa kama haibebeki. Hicho ni kitu ambacho ninaamini kwamba, hakitawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uamuzi mzuri ambao umepewa *TANESCO* kwa Ibara hii ambayo nimeitaja iwasaidie kuwapa nguvu kujiunda upya, kuangalia miundombinu yao inakaa kaaje, kuangalia bei zao kuona kwamba huduma zao zinakuwa nzuri. Haitawezekana kumwambia mwananchi kwa nguzo moja ya umeme atoe shilingi milioni moja, huyo ni Mtanzania gani; unataka aibe? Sisi sote hatuna fedha za *Richmond* wala hatujui mambo ya ufisadi, mwananchi atapata wapi hizo fedha? Umeme utabaki kuwa ni wa watu wenye uwezo, hiki ni kitu ambacho hakiwezekani kumwambia mtu aweke umeme ndani ya nyumba yake hawezi kuvuta umeme. Kwa hali hiyo ni lazima *TANESCO* ijue kwamba, hapa imelindwa kinamna namna ikiwa inapewa tahadhari kubwa sana nayo ikafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu tunahitaji sasa uwafikie Watanzania wote. Sote tunakaa maeneo ya mijini tunapita tunafanya kazi zetu, si kweli kwamba kila aliyepo mjini ana umeme ni kwa sababu ukiritimba sasa ndani ya *TANESCO* ulikuwa umefikia mahali pabaya na mengine ambayo wenzangu wameshayasema sina haja ya kuyarudia, lakini yalisababisha hata wale wanaoishi mijini, *TANESCO* ishindwe kuwapa umeme kwa sababu ya gharama kubwa. Kwa vijijini hali ni mbaya zaidi, wenzangu wametamka kwamba ni asilimia moja. Asilimia moja kwa Watanzania wanaoishi vijijini ambao tunasema ni asilimia sitini na tano ni kiasi kidogo sana. Kwa maana kwamba, asilimia 34 ya Watanzania wanaoishi vijijini, hawana umeme. Hii ni hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa ninachangia katika Muswada uliopita, nilisema kwamba, hii sheria itakapokuja ni vizuri na leo ninashukuru imekuja, hiki kitu kinachoitwa umeme wa vijijini, sasa ni wakati ambapo lazima kipewe umuhimu mkubwa sana. Sasa hivi Sera ya Chama cha Mapinduzi na ndiyo Sera ya Maendeleo kuhakikisha kwamba, kila Kata angalau kwa upungufu ina Shule moja ya Sekondari. Maana yake ni kwamba, tumejiandaa kusomesha wataalam katika Shule zetu za Sekondari, lakini unasomeshaje mtu ambaye huwezi kumpa majaribio halisi, kwa sababu kwa upande wa *physics* na *chemistry* mara nyingi inategema maabara, *biology* unaweza kwenda nje, lakini hayo mengine lazima utumie maabara. Mheshimiwa Rais anasema “Nataka kuona kwamba, mnaongeza ufundishaji wa masomo ya sayansi …” Kwa vipi?

Kwa hiyo, ni lazima kwanza *priority* ipelekwe katika shule zetu za vijijini, shule za Kata ziwe na umeme kupitia hii inayoitwa *Energy Rural Agency*, lazima ihakikishe kwamba, hilo linalifanya. Vilevile huduma za afya; hizo zahanati tunazotaka kujenga moja kwa kila kijiji na kwenye Kata; tuhakikishe tunaweka kituo cha afya bila umeme, *operation* hazifanyiki bila umeme, huduma nyingine ni saa ishirini na nne, haiwezekani kabisa ukategemea kwamba watu watashika kandili na mishumaa kuweza kufanya huduma zilizoko katika hospitali zetu ni lazima tuhakikishe kwamba umeme unafika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi ambao tunatoka vijijini, tunafahamu umuhimu wa vituo vya mazao. Kuna wizi mkubwa sana unaofanyika katika vituo vya mazao

nyakati za usiku kwa sababu ya giza. Kwa hiyo, umeme huu ni lazima pia ukaangalie vituo vya mazao kuhakikisha kwamba, kwa kila penye kituo cha mazao umeme lazima ufike. Kwa hiyo, tunaposema habari ya umeme wa vijijini, ninadhani Wakala huyu sasa ajue kwamba kazi kubwa anayo, lakini ana kikwazo kimoja kikubwa, ambacho sisi Waheshimiwa Wabunge hapa ndiyo tunao uwezo wa kusema tumsaidie na Serikali yetu ikiwa inatusikia. Lazima Mfuko wa kupeleka Umeme Vijijini uongezwe maradufu. Lazima kila ambaye ameshatangulia kupata umeme achangie, ambaye hana umeme apate umeme, anayepata sana anapunguza mwingine anapewa. Kwa hiyo, hata katika suala la umeme aliyekwishatangulia kupata ni lazima atozwe zaidi ili kuweza kuchangia wale ambao hawana umeme waweze kupata, hii ndiyo sera yetu ya kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, ninasema Mfuko huu waongezwe fedha lakini lazima wachangiaji waongezeke. Ninawaunga mkono wenzangu wanaosema, makampuni yote ya simu yachangie. Wanaochaji simu vijijini ni kati ya Sh. 200 na Sh. 500 kwa kuchaji simu mara moja tu. Kwa hiyo, kama anachaji simu kwa wiki mara nne ni sawa sawa na Sh. 4,000 kwa mwezi, kama mwananchi anaweza kuchaji simu yake mwenyewe kwa Sh. 4,000 kwa mwezi, haiwezekani kampuni ambayo inamwuzia na ananunua mtandao wake ishindwe kuchangia umeme huu.

Kwa hiyo, ni lazima kampuni hizi zichangie na umeme huu ni mtambuka katika kila Wizara, lazima kila Wizara ambayo inaguswa hapa ichangie; hospitali watachangia, ulinzi na usalama watachangia na maeneo mengine wachangie changie kuonyesha kwamba, umeme vijijini sasa si suala tena la kuona kwamba tuendelee kusuasua na malengo ya miaka mingi yasiyofikika, hiki ni kitu ambacho kwa kweli sasa hakifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile, wale wawekezaji wetu sasa ambao watakuja wachangie *ten percent.* Mimi ndivyo nilikuwa ninapendekeza kwamba, *five percent* pengine ni kidogo, pengine waongeze mpaka *ten percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Ibara ya 41, Sehemu ya Saba inasema hayo makampuni ambayo katika Mikataba kuna maeneo pale yameandikwa kwamba yasubiriwe kwa miaka mitano; nilikuwa ninapendekeza iwe miaka kumi, itakuwa imewapa muda pengine wengine kuwa wanakua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 26(5) mpaka (6) pale, ninaishauri sana *EWURA* ijijenge upya. Ijipe nguvu mpya baada ya Muswada huu ukishakuwa Sheria,. ihakikishe kwamba, inasimamia ipasavyo masuala ya leseni, utapeli ni mwingi tu katika masuala mazima ya leseni. Bei ya umeme lazima ikae vizuri, haki na kinga ya wateja lazima ikae vizuri, kwa sababu kuna watu wengi ambao wanapata hasara sana ya umeme ama wanakufa; juzi nimesikia mtoto maskini ameamka asubuhi amekuta nguzo imeanguka kuigusa akafariki, sijui wazazi wake wamelipwa nini? Kwa hiyo, basi kuna watu wengi ambao wanaunguziwa vifaa vyao ndani ya majumba yao na umeme na nyumba nzima inapata matatizo, *TANESCO* inasema wao hawahusiki na mengine mengi ambayo yanafanana namna hiyo. Yapo mengine makubwa sana yanatokana na uzembe; *TANESCO* wanapopewa taarifa hawataki kujali; wakisikia kifo gari na mafuta vipo, wakisikia kwamba kuna tahadhari hawataki kwenda. Hayo ni mambo ambayo ninadhani

sasa *EWURA* katika utaratibu huu, kwa upana zaidi, wasimamie vizuri ili mambo hayo yasiendelee kutokea tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa ninataka kusema kwamba, katika Ibara ya 11 Sehemu ya Nne, nilikuwa ninaomba kwamba, huyo mwekezaji ambaye kama nia yake ni kutaka kuhamisha huduma yake kuitoa eneo moja kwenda eneo lingine katika Tanzania aruhusiwe, lakini kama kusudi lake ni ku-*sub-let* ile leseni yake kwa mwekezaji mwingine, ninashauri hili angeliacha akarudisha leseni yake kwa waliompa, wao wakatafuta nani anaweza zaidi badala ya kumwachia mtu huyo huyo akatafuta mwenzake. Maana yake itakuwa sawasawa na hadithi ya wakoloni tuliojifunza kwamba, mkoloni hata siku moja hawezi kumng’oa mkoloni mwenzake na wala shetani hata siku moja hataki kuua shetani mwenzake, ila atakachojaribu kutafuta ni shetani mkubwa zaidi ili awadhibiti wenzake. Ikiwa kama huyo kashindwa amwachie mwingine, itakuja kuwa ni mchezo wa *Richmond* na *Dowans*, ambao tunauzungumza mpaka leo na umekuwa ni mchezo mbaya na mfano huo utufundishe kwamba haifai. Haifai kwa mwekezaji wao kwa wao hata kubadilishana kama *EWURA* inaambiwa kwamba ipewe taarifa. Mimi ningependekeza hiyo leseni irudishwe, halafu na mwenye kushindwa basi ameshindwa aondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 19(1) kama mwekezaji anakuwa hataki kuendelea kuwa mwekezaji wetu, nisingeshauri akaondoa miundombinu yake, kwa sababu atakapoiondoa inawezekana hatari yake ikawa ni kubwa sana. Nafuu akapata muda wa kuzungumza *then* ushauri ukawepo, lakini yeye aondoke aache miundombinu ichukuliwe na mtu mwingine. Tunaona hawa watu wa simu, tulianza na *TRITEL* waliposhindwa wakauza kwa watu wengine, lakini wao waliondoka hawakuondoa miundombinu. Mimi ningeshauri iwe hivyo hivyo. Afadhali auze kwa mtu mwingine mitambo siyo leseni, kuliko kuing’oa kwa sababu watumiaji pale watakuwa wameshazoea, kuiondoa watakuwa hawajawasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninapenda kurudia kwamba, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami angalau nichangie kidogo kutokana na Muswada ambao upo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa ninapata matatizo sana hasa ikiwa kama wenzangu wamekwishazungumza, kwa sababu matatizo ambayo yamezungumzwa na wenzangu, ndiyo hayo hayo yanafanana na sehemu ambako nimetokea. Kwa hiyo, huwa inanipa shida kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri wake na Watendaji wake, kwa kusikia na kuzingatia hoja za Waheshimiwa Wabunge walizozitoa, kukubali kwenda kufanya mabadiliko kwa ajili ya kuboresha Muswada huu. Ninawapongeza sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kuona kwamba karibu maneno mengi yamezungumzwa, nilikuwa na angalizo tu; sasa hivi Muswada huu unatilia mkazo wa kujaribu kuliimarisha Shirika letu la *TANESCO*. Ninakumbuka kabisa kwamba, kilichopelekea mpaka Muswada huu umechelewe ilikuwa ni kutokana na matatizo ambayo yaliifanya *TANESCO* iyumbe.

Sasa nilikuwa ninategemea hata Wajumbe wenzangu wa Kamati, angalau waonyeshe masikitiko katika upande huo ni kitu gani kilichoifanya *TANESCO* iyumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi wa Bunge uliopita, tulifikia hatua ya kuteua Kamati kusudi iangalie ni tatizo gani? Sasa hapa angalizo langu ni kwamba, nilikuwa ninategemea kwamba, hao waliohusika kuifanya hii *TANESCO* ikatetereka, basi wawajibike. Nina uhakika kabisa kwamba, Serikali inalifuatilia, lakini inalifuatilia vipi? Kwa sababu mimi katika Mkutano wa Kumi wa Bunge nilisema hiyo ni hujuma ambayo imefanywa dhidi ya Serikali na hujuma ni makosa ya jinai. Hivi hao waliohusika Serikali inakuwa na kigugumizi gani kuwawajibisha na watu wakajua kwamba kweli wanawajibishwa? Ikiwa kama makosa mengine tunasema kwamba basi hili ni kosa linajulikana, huyo mhusika angalau aende akapumzike mahali wakati uchunguzi unafanyika. Sasa hivi Serikali inasema tutalishughulikia. Mimi ninasema ni sawa walishughulikie, lakini ilikuwa ni angalizo tu kwamba, chelewa chelewa ndiyo hayo mengine ambayo tayari wameshaanza. Wangekuwa mahali wamepumzika, ninafikiri haya madogo yasingekuwa yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sasa hivi *TANESCO* tunataka kuipa nguvu ili iingie katika ushindani. Nilikuwa na mawazo tu kwamba, hao wawekezaji wanaokuja nao tuwaangalie vizuri sana, tusije tukafikia hatua ambayo tumeifikisha *TANESCO* hivi sasa. Zipo njia mtu anapokuja kuomba nafasi ni lazima achunguzwe, tusiende tu kwa sababu eti Sigonda ameamua kwamba yeye anaweza kuwekeza, basi ndiyo tukamchukua moja kwa moja. Lazima tufuate yale maadili ya utendaji ya kujaribu kumchunguza mtu na kumjua na vyombo tunavyo. Hata kama anatoka huko Ulaya bado atajulikana na ndiyo hiyo hatua tu ambayo inaweza kutusaidia kumjua huyo mtu kweli ana uwezo ama hana. Kwa hiyo, hilo lilikuwa ni angalizo langu tu kwamba, tuwafahamu hao wawekezaji na kuwafahamu lazima walete maombi kama kawaida, lakini tuwe na njia zetu za namna ya kuweza kuwathibitisha hao watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *EWURA* ni katika maadili yale yale kwamba, Mfuko huu au kikundi hiki ni muhimu sana. Ninategemea kwamba, viongozi ambao watakuwepo huko, lazima nao watakuwa ni viongozi makini na ambao ni waaminifu kwa kiwango kinachotakiwa. Sasa uaminifu wao utajulikana namna gani? Ndiyo hilo hilo kwamba nao tusianze kuchagua tu Sigonda leo unakuwa Mkurugenzi, fulani unakuwa Mkurugenzi bila kumjua huyo yuko namna gani? Hiyo itatusaidia sana kuondoa yale matatizo ambayo yamekuwa yakitupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili tatizo, sasa hivi tumetoa kazi na Muswada unaelekeza kuipa *EWURA* uwezo wa kuweza kudhibiti hali ya gharama ya

umeme. Ninasema sasa hivi gharama ya umeme ni kubwa mno. Ifike mahali tuanze kufikiria wakati tunapoagiza *EWURA* kujaribu kudhibiti bei hii ya umeme iliyopo sasa hivi ambayo mwananchi mpaka hivi sasa, inampa tabu itaendelea hiyo hiyo; kwa nini tusitamke tu kwamba waangalie bei ya umeme iliyopo sasa hivi kwa nia ya kuirekebisha iwe ndogo ya kumwezesha mwananchi aweze kuwa na uwezo huo? Nilikuwa ninafikiri kwamba, hiyo iwe ni moja ya hatua ambayo *EWURA* itaifanya kupunguza hizo gharama za umeme, hatuwezi kama tunakwenda nazo hizo gharama za umeme hivi hivi. Nilikuwa ninashauri hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri hili litakuwa la mwisho ambalo ninataka kulizungumza kuhusu *REA*; ni kazi nzuri, matarajio yetu ni kwamba, hata vijiji kama wenzangu walivyozungumza vitafaidika, lakini ni katika nafasi ya kuiwezesha tu hii *REA*. Sasa ninaunganisha moja kwa moja na kazi ambayo pengine nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuifikiria; kuna Mheshimiwa Naibu Waziri mmoja alikuja Jimboni kwangu na Wilayani kwetu. Baada ya kutembelea kwa muda mfupi akatoa sifa ama *qualification* za Wilaya ya Chunya na hasa Jimbo langu la Songwe. Alitumia Kiingereza akasema: "*That area is* a *disadvantaged, hard to reach and difficult to manage*." Haya maneno mimi yalinifikisha mahali kuanza kufikiria kwa undani zaidi. Wilaya yetu ina matatizo na huyo Mheshimiwa Naibu Waziri siyo aibu wala siyo vibaya kumtaja, alikuwa ni Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, ninamshukuru sana. Kwa sababu aliiona hali halisi ya Wilaya ya Chunya na Jimbo la Chunya na siku zote mimi nitaendelea hata nikizungumza namna gani, nitapenda Waheshimiwa Mawaziri waelewa kwamba, sisi tunahitaji msaada zaidi kwa upande wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu miaka minne iliyopita, kama mwenzangu alivyozungumza, sehemu zote alizozitaja tayari kuna nguzo za umeme. Tumejitolea sisi pamoja na wananchi, tumeweka nguzo za umeme kwa matarajio kwamba, watakuja kuweka nyaya tu, lakini mpaka hivi sasa hakuna kinachoendelea. Nilisema katika Mkutano wa Bunge uliopita, nimegundua kumbe zile fedha ambazo zilikuwa zinakwenda huko zilikuwa zinaishia kwa akina *Richmond*, ndizo zilizosababisha mpaka sisi tuendelee kuteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba tu kwamba, wakati tukitekeleza Muswada huu, kuwe na mwelekeo wa kutambua maeneo ambayo yana matatizo makubwa zaidi kama eneo la Wilaya ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema kwamba, siwezi nikarudia rudia yale ambayo wenzangu wameyazungumza, ninaunga mkono yote na kwa kweli ninaweza nikasema kwamba, mwishoni kabisa ninauunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kuhusu Muswada huu wa Umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wake, pamoja na timu yake, kwa kweli wamefanya kazi nzuri sana. Tulipokutana mara ya kwanza kwenye Kamati mwezi Februari, 2008, kulikuwa na kasheshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba, Muswada huu ni moja kati ya Miswada bora ambayo imeingia katika Bunge hili kwa hivi sasa. Kwa sababu wameshirikishwa wadau mbalimbali na pengine kwa kiasi kikubwa sana, umeshirikisha nia na haja kubwa za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufikie mahali tukubali mabadiliko, lakini mabadiliko yaje kwa msingi wa ustaarabu. Ni vyema kila kitu kiweze kupata *guidance,* inapobidi kuwa na *guidance* siyo kuachia tu hivi hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kuzalisha nishati kwenye nchi yoyote ni tata kweli na ni tete vilevile. Huwezi ukaachia *utility facility* kwa *Private Investors* pekee yake haiwezekani, lazima kuwe na mkono wa Serikali kwa kiwango kikubwa zaidi na hii itasaidia sana kuweza kuhamasisha hata shughuli mbalimbali za uzalishaji na maendeleo kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwamba, Watanzania ni wazuri sana wa kusema, lakini utekelezaji wetu kidogo una mushkeli. Ninaamini kabisa kwamba, leo hii tungeamua fedha iliyoibiwa kwa njia za ufisadi ingerejeshwa tukawekeza kwenye umeme, ninadhani shida ya umeme kwa kiasi kikubwa ingeweza kwisha katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kusema kwamba, hatuna jinsi sasa hivi lazima tuwekeze kwenye umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* hapa walipofikia ni sisi wenyewe tumewafikisha. Kwa sababu akikaa pale Mswahili akisema umeme usiende mahali fulani, anaambiwa hapana huna kazi, lakini Mzungu akikaa mahali fulani watu tunalipa *bill* mpaka Serikali inalipa *bill*. Kwa hiyo ni tatizo kwanza, ndani ya Serikali; lazima Serikali iweze kutoa mwongozo sahihi na isiweze kuingilia Mashirika yetu haya. Vinginevyo, tunayoyazungumza hayawezi kutusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tu niseme kwamba, *TANESCO* wanahitaji msaada lazima tuwakarabati na kuwakarabati lazima tuwapatie fedha za kutosha kuweza kujiendesha na kujikarabati. *TANESCO* ilikuwa imeelemewa na mzigo mkubwa sana wa madeni, itawezaje ku-*produce* umeme *more efficiently and effective* haiwezekani, lakini nani amesababisha hayo ni sisi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tuna Makampuni saba na katika ya hayo, Makampuni yote sita ulikuwa ni mzigo mkubwa sana kwa *TANESCO. ALSTOM* peke yake *capacity charge* yao ni *dollar* milioni 1.75; *IPTL* ni *dollar* milioni 2.84; *AGGREKO*

ni *dollar* milioni 1.4; *DOWANS* wa juzi hawa wao *capacity charge* peke yake ni *dollar* milioni 3.7; Songas ni *dollar* milioni 6; ukizijumlisha ni zaidi ya *dollar* milioni 15, ambayo ni sawa sawa na shilingi bilioni 18, hiyo ni *capacity charge*, bado umeme haujafuliwa kwenda kwa mlaji. Hivi kweli unategemea *TANESCO* watafanya namna gani kazi na bila kuzalisha katika nchi hatuwezi kupiga hatua za maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba chonde chonde walioiba fedha za Serikali, basi wekezeni katika miradi ya kuzalisha umeme, badala ya kuficha fedha huko nje, kwa sababu hiyo haimsaidii Mtanzania hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukiangalia katika takwimu zilizopo ni zaidi ya *dollar* milioni 900 zimeibiwa. Sasa hizo fedha ni msingi mkubwa sana kufanya Mtanzania azidi kupata matatizo na maisha ambayo ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni kwamba, sasa ni muda wa kubadilika na Watanzania tubadilike hakuna jinsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme ni la kiuwiano, hakuna asiyependa umeme hapa na ni siasa kwenye Majimbo. Ukienda Mtwara watasema kuhusu umeme, Mchuchuma wapi umeme, ukienda Songea watasema kuhusu umeme, ukienda Korogwe watasema kuhusu umeme, ukienda Sumbawanga hata kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda naye atasema analia hana umeme Jimboni kwake. Sasa ukija Shinyanga, Mwanza, Mara na Kagera, ndiyo balaa hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata watu wa Pemba wanalia umeme hakuna. Sasa kila mtu analia, hivi tutalia mpaka lini? Kama tulianzisha mpango mahususi wa kukopa fedha kutoka Benki ya Dunia tukatekeleza Miradi ya MMEM na MMES; kwa nini tusikope fedha kuwekeza katika kufufua nishati na kusambaza umeme vijijini, kwa sababu hatuna jinsi ni heri mkopo wa namna hiyo ambao utakuwa na tija kwa kila Mtanzania? Leo tunaruhusu Makampuni hayo yanachukua fedha nyingi eti *capacity charge;* jamani tutafika wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningesema kwamba, hata katika Muswada huu ni vyema wawekezaji binafsi kuingia katika *market*, kwa sababu ukiwa na *players* wako kwenye *market* inamsaidia mlaji safi kabisa. Lazima Serikali iweze kuzalisha umeme kwa kiwango ambacho hatuwezi kuwa na wasiwasi. Tuna vyanzo vingi sana hapa nchini kila mmoja ametaja; kuna Malagarasi na kuna sehemu mbalimbali, lakini vyote hivyo vikiweza kuzalisha vizuri na Serikali kuweza kuwekeza mtaji unatosha, umeme utaweza kufika vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilio cha wananchi ni umeme; tunasema maendeleo hata mtoto anapozaliwa kwa kutumia kile kibatari anakuwa na akili ya kuwa na kibatari, lakini akizaliwa akaona umeme atakuwa na akili ya kuwa na umeme. Watanzania lazima twende na Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni tatizo la umeme; Jimboni kwangu, ndio lazima niseme kwa sababu sitarudi hapa. Jimboni kwangu nina miaka minne ninaomba umeme, kuna *portion* ya kilomita 18 kutoka Lamadi, Kalemela, Kabita mpaka Nyashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo majibu hapa ya Serikali kwenye *Hansard*, kwa miaka minne ninaambiwa fedha zimetengwa utapata umeme, sijapata umeme. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, safari hii nitapata umeme na amesema ni ahadi hai. Sasa ninasema hivi; Mheshimiwa Waziri aitekeleze, kwa sababu vinginevyo itakuwa kashehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe ukienda maeneo ya Sengerema kule nako wanalia kuhusu umeme; Kamanga, Sengerema wanalia kuhusu umeme; Katunguru kule Kijiweni kwa wavuvi wanalia kuhusu umeme; Sengerema - Ngoma wanalia kuhusu umeme; Buyagu - Busisi wanalia kuhusu umeme; sasa jamani, kila mmoja analia kuhusu umeme hapa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba suala hili lazima tuliwekee mkakati mahususi, tusilie sana bali tutafute njia mbadala ambayo itatupatia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu Wakala *(Rural Energy Agency),* fedha hii bilioni kumi ni kidogo sana. Kama tunataka ifanye kazi huu ni utani kabisa. Ningeomba tutafute vyanzo vingine mahususi kama ni kwenye bajeti, basi tuchukue bajeti ya Serikali asilimia kadhaa ichangie kwenye suala la umeme vijijini vinginevyo itakuwa ni hadithi. Hatuwezi kupeleka umeme vijijini bila kumwezesha *REA* anahitaji trilioni 1.2, atazipata wapi fedha hizo? Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba kwamba, lazima tuwe na mkakati mahususi wa kumpatia *REA* fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mikataba ni tatizo na bado ni tatizo. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema na Mheshimiwa Michael Laizer akasema na wengine wamesema, sina haja ya kurudia sana hilo. Ninadhani tuwe makini katika mikataba hiyo ambayo inatuingiza mahali ambapo siyo pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *EWURA;* yeye ni *regulator*, lakini ataweza ku-*regulate* tu kama *system* zitakuwa zina-*function* na ninachoomba ni kwamba, yeye atusaidie kuhakikisha kwamba, wanaopewa leseni wote kweli wawe ni wawekezaji ambao wana sifa kamilifu.

Tusipate matapeli hapa, kuna watu wanakuja na *briefcase* ni mwekezaji anakuja anatafuta mradi hapa, anachukua mradi anautafutia fedha na anatajirika hapo hapo, lakini tufike mahali lazima tuache. Wawekezaji wote wanaokuja ni lazima tuwa-*scan*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, ninakushukuru sana, ninaona una uzoefu sana hata na Jimbo la Mheshimiwa Waziri umelizungumzia kweli

hapa. Baada ya kumsikiliza Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, ninaomba nimwite sasa Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe mchango wangu katika Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianzie katika kuielezea *TANESCO* kwa sababu niliwahi kufanya kazi *TANESCO* kwa takriban miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wamezungumzia juu ya hali na mustakabali wa *TANESCO* na matatizo yanayojiri kwa *TANESCO* hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ina matatizo makubwa ambayo sasa hivi Waheshimiwa Wabunge walio wengi wamesema iko hoi. Kwa kuwa mengi yamezungumzwa na wenzangu walionitangulia, nitajikita zaidi katika kuzungumzia yale ambayo wenzangu hawakuyagusia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* ilianzishwa mwaka 1964, sasa hivi ina umri wa miaka 44. Makubwa ambayo yameitafuna *TANESCO* ni pamoja na muundo wa Shirika hili ambalo kwa kipindi kirefu imekuwa nao, ukiondoa miaka hii ya karibuni. Kwa kipindi kirefu, *TANESCO* ilikuwa na muundo ambao ulikuwa unaitafuna yenyewe. Nikitoa mfano, miaka ya 80 mpaka 90, *TANESCO* ilikuwa inazalisha takriban kama megawati 600 hivi. Kipindi hicho Shirika hilo lilikuwa na Wakurugenzi wanaofikia 21, ukilinganisha na wenzetu wa Zambia ambako Kampuni yao ya *ZESCO* wao walikuwa wanazalisha megawati takriban 1600, lakini ilikuwa na Wakurugenzi kwa kipindi hicho waliofikia saba. Sasa ukitafuta *ratio* hapo, utakuta *overhead cost* ya *TANESCO* ilikuwa ni kubwa sana, kwa sababu ya kuendesha Shirika hili, kulipa watu mishahara minono na kuweza kuwaenzi hao Wakurugenzi na Mameneja wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo limekuwa likiitafuna *TANESCO* ni juu ya mipango yake ya uwekezaji. Nitatoa mifano hai juu ya namna *TANESCO* ilivyokuwa inawekeza; Jengo la Ubungo ambalo kwa kipindi kile bajeti ya kujenga jengo lile ilikuwa ni shilingi bilioni mbili, sioni kwa nini kulikuwa na haja ya kujenga jengo lile, kwa sababu Ofisi inayokidhi mahitaji kwa *TANESCO* Makao Makuu ilikuwepo na hasa ukizingatia kwamba, jukumu la msingi la *TANESCO* ni kuzalisha umeme, kuusafirisha, kuusambaza na kuuza kwa wateja! Sasa ikachukua jukumu la Shirika la Nyumba likaibeba *TANESCO.* Kwa hiyo, hiyo ni sehemu mojawapo ambayo *TANESCO* imeweza kutafunwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, sasa hivi ninasikia vuguvugu tena inataka kuanzisha Chuo. *TANESCO* ilikuwa na Chuo; kimeitafuna sana *TANESCO,* ninashukuru kwamba, waliweka maamuzi ya kukivunja, lakini sasa hivi ninasikia kuna vuguvugu tena la kutaka kuanzisha Chuo. Ninaishauri sana *TANESCO* isirudie tena

kwenye mtego huo; *is better to hire than to own*, hasa wakizingatia kwamba kile wanachokihitaji siyo cha mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu sasa badala ya ku-*own* Taasisi ambayo wanahitaji mara kwa mara, *TANESCO* ndiyo ikaamua kuiuza. *TANESCO* ilikuwa inamiliki shamba la nguzo lililopo Mbeya, likauzwa shamba hilo kwa mmiliki mmoja, ninalihifadhi jina lake. Mimi ninalinganisha suala hili kama la wakwe zangu Waluguru wa Morogoro; maana yake tumeoa sisi kule; Mluguru anaweza akavuna mihogo huko Mgeta au Matombo akaipeleka sokoni na kuiuza yote; baadaye atakwenda sokoni hapo hapo kununua mihogo ambayo imewekwa bizari na kadhalika. Ataisifia sana mihogo ile kwamba ni mitamu na inanukia kisokosoko. Ndiyo sawasawa na hawa ndugu zangu wa *TANESCO. (Kicheko/Makofi)*

Sasa hivi wanazisifia zile nguzo; nzuri, ndefu lakini zilikuwa za kwao! Kwa hiyo, katika kipengele hiki kwa kweli ndicho kilichoongeza bei ya nguzo. Zamani ilikuwa nguzo moja tunanunua shilingi 20,000, sasa hivi baada ya kuuza shamba lile la nguzo, nguzo moja imepanda mpaka shillingi 60,000 na sehemu nyingine shilingi 90,000. Hii ni kwa sababu shamba lile na mtambo ule umeuzwa kwa mtu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu kuna kitu kimoja *TANESCO* kinaitwa *Staff Tariff*; sisi tunalia hapa *unit* moja tunanunua shilingi 195, lakini mfanyakazi wa *TANESCO* analipa senti 20 kwa *unit* moja. Kwa mujibu wa tovuti ya *TANESCO* sasa hivi ina wafanyakazi wanaofikia 4,670. Sasa chukulia kila mfanyakazi atatumia *unit* 200 kwa mwezi, maana yake Shirika litatumia *unit* 934,000. Ukizidisha mara 195 maana yake Shirika lingeweza kupata shilingi 183,130,000, lakini matokeo yake Shirika lina-*realize* 186,800. Kwa hiyo, utakuta 181,900,000 hizi zinaliwa na wafanyakazi wa *TANESCO.* Leo hapa Wabunge tunasema kwamba, tuiinue *TANESCO,* lakini wafanyakazi wenyewe hawana *spirit* hiyo ya kuiinua *TANESCO*. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili na alitolee tamko, kwa sababu sisi sote ni Watanzania na Shirika la *TANESCO* ni la kwetu, isionekane kwamba mtu ambaye anayepewa dhamana kuendesha Shirika lile ananufaika zaidi kuliko yule ambaye yuko nje ya Shirika. *(Makofi)*

Tatizo la nne, ambalo Wabunge wenzangu wamelizungumzia ni juu ya wawekezaji ambao ninaamini kwamba ni sawa sawa na mgonjwa ambaye siku zake za kufa zimetimia, lakini unapokwenda wewe kumwangalia basi ndiyo siku hiyo hiyo anakufa. Hawa ndio akina *DOWANS* na *RICHMOND,* wamekuja kuongeza kifo cha mgonjwa ambaye tayari yuko mahututi. Ninaomba Wabunge wenzangu wasiwe na hofu, kwa sababu Muswada huu uko ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Ukisoma ibara ya 43(g), utaona imeelezwa kwa ufasaha kabisa na vilevile iko ndani ya Sera ya Taifa ya Nishati, utaikuta katika ibara ya 58 ukurasa wa 46 mpaka 47. Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi, tuko ndani ya sera pamoja na ndani ya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna fikra za wenzangu ambazo zinasema kwamba, wawekezaji binafsi hawataweza kufika vijijini, ninadhani tusiogope mawingu mpaka mvua itunyeshee. Ninayo mifano halisi, *ARTUMUS* ambayo sasa hivi iko pale Mtwara,

wameonyesha na wamethibitisha kwamba wanaweza. Katika makala hii ambayo imetolewa na *ARTUMUS* wanasema kwamba, dira yao itakuwa ni kupeleka umeme vijijini na *connection fee* itakuwa ni kati ya shilingi 60,000 mpaka shilingi 80,000, ambapo *TANESCO* sasa hivi tunalipa shilingi 500,000. Kwa hiyo, huu ni mfano halisi ambao wenzetu wanasema kwamba, wako tayari hata kuingiza umeme kwenye nyumba za nyasi; teknolojia hiyo wanayo. *(Makofi)*

Vilevile Tunduru ninadhani sio mjini ni vijijini; hivi majuzi kuna mwekezaji ambaye ameonyesha nia, anaitwa Kanyan Capital. Makao Makuu yake sasa hivi kwa hapa nchini yapo Zanzibar, wameshakwenda ku-*survey* na wako tayari kuwekeza umeme vijijini sio Dar es Salaam. Kwa hiyo, ninasema hii ni fikra ambayo tunatakiwa tuiondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niliwahi kuuliza swali hili kwa Mbunge mwandamizi mmoja, ambaye kwa bahati nzuri na yeye ni mfugaji; nilimwuliza hivi kama zizi limejaa vidume tupu kuna uwezekano wa kupata ndama, akasema hakuna. Nikamwuliza kama imejaa mitamba tupu bila dume, akasema hapana lazima lipatikane dume. Sasa kwa kuwa *TANESCO* lina umri wa miaka 44 hatujapata ndama ni dhahiri kwamba, zizi letu aidha lina madume tupu au lina ndama watupu. Kwa hiyo ni lazima twende kwenye zizi la jirani yetu, tukachukue madume ili tugawane ndama watakaopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia, kwa sababu inakaribisha madume kutoka zizi la jirani ili tupate ndama ambao tutagawana. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mtutura, mchango wako leo umekuwa kiboko hasa. Wale wakwe kule Morogoro kama wamekusikia, wanaweza kukunyang'anya mke. *(Kicheko)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa Umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii, kuipongeza sana Kamati ya Nishati na Madini, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuuboresha Muswada huu. Tulikuwa tunashirikiana nao na sisi wengine sio Wajumbe wa Kamati ile, lakini tunajua wenzetu wakati mwingine walitoka usiku hata saa 3.00 kwa ajili ya kuufanya Muswada huu uweze kuwafaa Watanzania. Pia ninampongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kuwa wavumilivu katika kupokea maoni ya Wabunge mmoja mmoja, maoni ya Kamati na maoni ya wadau mbalimbali katika kuuboresha Muswada huu. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muda wote ambao tulikuwa tunashiriki au nilikuwa ninashiriki katika mchakato mzima wa kutengeneza Muswada huu, liko jambo moja lilijitokeza sana ambalo pengine sayansi yake ni vizuri sana tukajiuliza kila aliyekuwa anasimama ama anaunga mkono au anaupinga, alikuwa anazungumzia habari

ya maslahi ya Taifa. Sasa neno hili maslahi ya Taifa, linaweza wakati mwingine likatuchanganya tukashindwa kwenda kwenye kitu ambacho tunakihitaji. Mimi ningesema tu, hakuna maslahi ya Taifa mazuri kama hayatupeleki kwenye matokeo tunayoyataka. Hofu kwamba Muswada huu unaoruhusu wawekezaji binafsi kuzalisha, kusambaza na kuuza umeme ni hofu ambayo haiendani na wakati wa sasa; haina msingi wowote, kwa sababu kunapotokea ushindani katika sekta yoyote, ndipo utakapopata tija na hasa kupata unafuu kwa yule mlaji. Kwa hiyo, *consumer* anapata nafuu kwa ushindani unaotokana na wale wanaofanya shughuli ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya Muswada huu, ambao sasa unaalika wawekezaji binafsi wa kuzalisha umeme, nina matumaini makubwa kwamba, ule umeme ambao ulikuwa ni ndoto na ambao wengi tunauzungumzia hapa, tutaweza kuupata kule vijijini. Msingi wa Muswada huu, unatokana na sera yetu ya umeme ambayo sasa inatambua uwepo wa wawekezaji binafsi *(Private Power Companies),* ambazo ujio wao unakuja kuleta *challenge* kwa mfumo uliokuwepo wa Shirika letu tunalolitegemea, tunaliheshimu na tunalipenda sana la *TANESCO.* Pamoja na mapenzi ya *TANESCO, everyone* ata-*declare* kwamba, *I love you TANESCO.* Mapenzi haya ya kuwapenda *TANESCO*, yatakuwa hayana manufaa kama kile tunachokitegemea Watanzania wakipate hawatakipata. Watanzania wanachokitaka ni umeme; wanapataje? Ni kwa njia yoyote ile itakayoonekana ina matarajio na matumaini makubwa kuwapelekea umeme. Kwa hiyo, ninasema sheria hii iko safi. Miongoni mwa sheria ambazo nimeshiriki kuzitengeneza nikiwa kama Mbunge, ninadhani sheria hii imepitia katika viwango vyote vinavyostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilitaka niseme nini Watanzania wanachokihitaji baada ya mijadala yote hii, baada ya misukosuko yote iliyotokea lakini mwisho wa siku ni nini wanachokihitaji? Watanzania wana kilio cha mzigo wa *capacity charges.* Kwa hiyo, tutazungumza hapa mengi tutaweka blablaa nyingi na mikwara mingi, lakini mwisho wa siku tukirudi kule kwa wale wanaopata umeme sasa wanatuuliza; je, umeme umeshuka bei; kama haujashuka maana yake tumecheza ngoma bado mbichi, tunatokaje hapo? Tutazungumza hapa, tutapiga blablaa, tutasema sheria nzuri lakini kama umeme haufiki kule kijijini bado ngoma ni mbichi. Unafikaje kijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimboni kwangu ndipo ambapo kuna kinu kinachofua umeme wa Mtera. Watu wengine wanachanganya jiografia wanasema, Mtera iko Iringa, wengine wanasema ipo sijui Dodoma Vijijini; Mtera iko Wilaya ya Mpwapwa jimbo la Kibakwe. Kijiji kinachofuatia cha Kisima, Chipogolo na vingine vya karibu kama Rudi, pamoja na Shule ya Sekondari tunazojenga na zahanati tulizonazo, hawajawahi kutumia toka wazaliwe, wanajisikiaje watu? Tukipiga hapa maneno ni bure tu. Kwa hiyo, kimsingi ni kusaidia Serikali kwa kuipa sheria nzuri kama hii ili waweze kutuletea umeme vijijini na ninaamini kabisa kwa maana ya Muswada huu, Tanzania wawe na matumaini na kwa niaba ya wapiga kura wangu, ninataka niwaambie hata ile mipango ya kupeleka umeme mpaka Rudi, Kinusi na Pwaga sasa inawezekana kwa kupitia sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu baadhi ya mambo ambayo ninadhani yanaweza yakawa na changamoto katika sheria hii pia; *compulsory acquisition of land.*

Suala la ardhi limesemwa vizuri katika sheria hii, lakini pamoja na kusemwa kwake, sina hakika kwa sababu hii *compulsory acquisition of land* ilitumika vizuri wakati huo tulipokuwa tunazungumzia habari ya *public interest*. Sheria hii ya *Land Acquistion Act* ya Mwaka 1967, ilifaa sana kwa wakati ule kwa sababu mara nyingi tulikuwa tunafanya hivyo kwa ajili ya ku-*preserve* maslahi ya Taifa. Sasa kuna *a mixed interest* hapa; tunaye *private and public interests.* Ni muhimu Serikali ikaona haja ya kuifanyia ukarabati hiyo *Land Acquisition Act,* ambayo sasa inatumika sambamba na *Land Act* ya 2000 katika kufanya mambo yote yanayohusu ardhi na hasa masuala ya *compensation* na masuala ya kutwaa ardhi kutoka kwa wananchi wetu. Kama tutaiacha katika upungufu iliyonayo sheria ile na makali yale yaliyokuwa yanatambua tu kwamba kwa kuwa ardhi iko chini ya Rais, basi maslahi ya Taifa yalikuwa yanakuwa *declared* kirahisi. Kwa sasa hivi si hivyo, kwa sababu sasa kuna *a private sector* inaingia. Kwa hiyo, ningependa sana Mheshimiwa Waziri ulitambue hili na Serikali ni vizuri ikalitambua lile katika mtazamo wa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vijijini; pamoja na yote tunayoyasema hapa ukiangalia *section* 37 ya Muswada huu, haizungumzii tu wazalishaji wale wa umeme lakini pia bado inaipa *task TANESCO.* Wanapoipa *task TANESCO* ni katika maana ya *TANESCO* kujipambanua kuchemka sawa sawa ili iweze kukutana na ushindani wa *Private Sector.* Tumesikia wenzetu hapa wa Kusini, wanalia na *ARTUMUS,* hawana njia lazima walie na *ARTUMUS* kwa sababu ndilo wanaloliona suluhisho. Kama unatoka Kigoma lazima ulie na Malagarasi ndiyo suluhisho, ama unatoka Kibakwe lazima ukawaone wale Mapadri wanaozalisha umeme pale Parokia ya Rumuma na wao bila sheria hii, hawawezi wakasambaza umeme ule hata kijiji kimoja. Kwa hiyo, ninasema sheria hii kwa ujumla wake na kwa maana ya malengo yetu ya umeme vijijini ambapo katika takribani asilimia ya Watanzania karibu 40,000,000 ni asilimia 11 tu ya Watanzania ndio wanaopata umeme na wa vijijini ni asilimia moja. Kama *TANESCO* haijajiweka sawa, ikashiriki katika mchakato wa sasa, haitaweza kabisa ku-*exist* katika ushindani na waache visingizio kwa sababu sasa tumetengeneza mpango wa kuwaongezea mapato, lakini usiwafanye wabweteke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii nzima pamoja na yote ambayo yamesemwa; Muswada huu ni kama Muswada wa *EWURA;* ni *as if EWURA* sasa wanapata sheria ya pili ya kuwafanya wafanye kazi katika mazingira ya kisasa ya ushindani. *EWURA* sasa ndio ma-*referee,* maana yake wana sheria ya kwao lakini pia katika Muswada huu imewazungujmzia *EWURA;* wakitusaliti tumekwisha. Maana wao ndio wanao-*dominate a major role* ya *operation* ya mchezo unaokuja kati ya sekta binafsi kuingia katika uzalishaji na usambazaji wa umeme, kama *EWURA* wakitusaliti tumekwisha. Kwa hiyo, ninasema ninawaheshimu sana ndugu zangu wa *EWURA*, ninajua kuna watu waadilifu na makini wapo pale, waiangalie *EWURA* isije ikaingiliwa na kidudu mtu. Ninataka niwaambie ndugu zangu kwamba, kama *EWURA* haitasimama kidete kutetea yote yaliyosemwa hapa, hakuna kitakachokwenda kwa mtazamo tunaouona. *EWURA* msije mkatusaliti, ninawaomba sana mjitahidi kutimiza wajibu wenu kwa sheria zilizowekwa. Vilevile mhakikishe kwamba, ushindani unakuwa wenye maslahi na tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa wananchi katika uchumi huu mpya unaokuja kuamshwa na ujio wa umeme kwa madhumuni hayo sasa; ninasema kama sekta hizi hawa *foreign investors* wataingia, lazima tujue *the position of local contractors*. Isije ikawa wakiingia hapa, basi hata balbu ikafungwa na mtu kutoka South Africa. Watakuja na mikwara hapa unajua teknolojia hii ya umeme wetu sisi lazima anayekuja kuweka *installation* atoke Shirika la kutoka sijui Uingereza. Ninasema *local contractors* wetu lazima walindwe. Wanao uwezo; tunao wasomi wa kutosha ni lazima tuwalinde na wao wapate kazi katika Makampuni hayo, kama kazi wameiweza basi wapewe *local contractors*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ndugu zangu sekta binafsi ikiingia katika ushindani huu *TANESCO* watachangamka. Tuangalie Shirika la Posta na Simu leo linafanya nini; ni matokeo mazuri ya ushindani. Tuangalie leo huu ushindani uliopo katika mawasiliano ni mkubwa na unaleta tija na sisi tunapata nafuu. Kama walivyosema wenzangu kwamba ni vizuri sekta hii sasa ikasimamiwa vizuri na Serikali na pengine tuseme tu kwamba hizi *capacity charges,* ambazo ni mzigo kwa Watanzania leo; ukiangalia kwa mfano mimi nimenunua umeme wa shilingi 50,000 mzigo wa umeme nilionunua ni wa shilingi 24,000 lakini *the difference* ya ile 50,000 yote imelipa kitu kinachoitwa *service charges* na kodi. Kwa hiyo, karibu shilingi 16,000 nimebeba mzigo wa *service charges* ambayo kwa lugha nyingine ni *capacity charges.* Kwa hiyo, maana yake hapa mzigo mzito sana tunawabebesha Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii nami niungane na wenzangu wote katika kuchangia huu Muswada muhimu sana kwa ajili ya Taifa letu. Awali ya yote, nianze kwa kusema ninaunga mkono Muswada huu, kwa viwango vyote vinavyostahili kwa kuutambua umuhimu wa umeme ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza vijana wenzetu ambao wamekabidhiwa hii Wizara; walikutana vitani lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na uelewa wao na kwa kutafakari yale tuliyokuwa tunayazungumzia au kuyalilia kwa maana ya kuwatetea wananchi wetu, wameweza kuyaweka kama *amendments* na ndiyo maana leo tunaujadili huu Muswada kwa furaha na amani kubwa kabisa. Tunawapongeza wote mlioshirikiana nao, ikiwa ni pamoja na Kamati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Muswada ni muhimu, hakuna asiyefahamu umuhimu wa umeme ndani ya nchi yetu. Tunazungumzia mambo ya kufundisha masomo ya sayansi katika shule zetu, kama hatuna umeme tutafundishaje. Ili Taifa letu liweze kuendelea tunahitaji umeme wa viwango vyote katika nyanja zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwanza kusema kwamba, Wabunge wenzangu ile dhana ya kusema labda kuna eneo fulani la nchi hii ambalo lina umeme zaidi si kweli, ule umeme umepita tu katika baadhi ya maeneo na hapa ninazungumzia

sana kule Kaskazini ambako wanasema umeme upo mwingi sana. Si hivyo, bado tuna vijiji vingi sana ambavyo havina umeme na tuna maeneo mengi ambao umeme haujafika. Kwa hiyo, niseme kwamba ni nchi nzima ya Tanzania tunahitaji umeme. Tunapokuja kuzungumzia masuala muhimu, tusianze na masuala ya majimbo na maeneo; tuzungumzia kwa maana ya Taifa letu la Tanzania. Watanzania wote tunahitaji tuendelee, hilo ningeomba lieleweke wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba katika kutekeleza huu Muswada, elimu kwa wananchi wetu ni muhimu sana. Tuwaelimishe nini manufaa na ubora wa huu Muswada tunaouzungumzia hivi leo. Matunda yake yatakuwaje, kwa sababu wananchi wetu wameshaanza kuwa na wasi wasi, ukishang'atwa na nyoka hakuna asiyejua kinachotokea. Tuondoke hapa tukawaelimishe ili nao waweze kuwa na imani kutokana na hiki tunachokizungumzia na kukiamua hivi leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuainishwa katika huu Muswada mpya kuhusu mambo ya *capacity charges* kwamba, hazitakuwepo tena kwenye mikataba mipya, ninawapongeza sana. Ningeomba basi zile *capacity charges* tunazozizungumzia hapa za Makampuni tuliyonayo sasa hivi, hebu *TANESCO* waondolewe ule mzigo ubebwe na Serikali kwani halikuwa kosa la *TANESCO.* Kwa njia moja au nyingine, halikuwa kosa la *TANESCO*; ni kile kitu kinachoitwa mikataba mibovu. Mimi ningeomba kabisa *capacity charges* zote zibebwe na Serikali Kuu ili viwango vya umeme viweze kushuka, *affordability* iwepo ili wananchi wetu waweze kupata umeme na kuweza kuutumia. Kwa sababu tukiendelea namna hiyo, umeme utakuwa ni anasa. Hata tukipitisha Miswada mingine mizuri namna gani, bado mzigo utakuwa ni mikubwa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ibara ya 41(6), *TANESCO* itapewa kipaumbele katika miradi mikubwa ya uzalishaji na usambazaji. Niungane na wenzangu kuwaomba ndugu zetu wa *TANESCO*; ukibebwa ujishike, ukibweteka utaanguka. Wenzangu wameshazungumzia vizuri sana, sasa niwaombe ndugu zangu nao wajishike, tunajaribu kuwabeba wajishike wasije wakaanguka. Kwa sababu wakishaanguka, aibu itarudi kwetu sisi wenyewe ambao tumeitetea sana. Tuiimarishe kabla ya kuiingiza kwenye mchakato kama huu. Kwa hiyo, ninawaomba wenzetu wa *TANESCO*, yale mengine ambayo yameshazungumziwa hapa ya matumizi ya ajabu ajabu, uagizaji wa vifaa kwa maana ya kuzidisha bei na mambo mengine yote ambayo yataweza kuleta dalili mbaya, waachane nayo na Mungu awasaidie sana wasije wakaingiliwa na shetani anayeweza kuharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatana na Muswada, tukitumia vizuri rasilimali tulizojaliwa na Mwenyezi Mungu, ikiwa nii pamoja na gesi, maji, upepo na kwa sababu *capacity charges* hazitakuwepo katika mikataba mipya.; nina uhakika kwamba, umeme wetu utakuwa ni mzuri, bei itakuwa chini vizuri kabisa tutakwenda hata viwango kulinganisha na nchi za jirani, nikiwa na maana kwamba, tutaweza kuuza umeme wetu nchi zinazotuzunguka. Hakuna asiyefahamu kwamba, nchi zinazotuzunguka na wao wana uhaba mkubwa sana wa umeme. Kwa hiyo, ningeomba sana ile mikataba itengenezwe vizuri ili manufaa yaweze kuwepo kwa ajili ya wananchi wetu na kwa ajili

ya kuweza kuuza nchi za nje. Hili litatusaidia wananchi wakishaendelea tutaachana na ile dhana iliyopo hivi sasa. Maana yake ndani ya nchi yetu sasa kuna dhana potofu; wapo wenye nchi na wananchi. Hii dhana ya wananchi na wenye nchi, iweze kuondoka. Wananchi wanahitaji waendelee na umeme uwe *affordable.* Kwa sababu wale wenye nacho na bahati mbaya wengi wao hawana asili yetu, wanasema wao ni wenye nchi kwa sababu wana uwezo na mamlaka zaidi, sasa sisi wananchi ndio tunaoumia. Wananchi wetu tukishaweza kuwaeleza hiyo dhana ya wenye nchi na wananchi itaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)*; hiki tunachopendekeza cha asilimia tano ni kidogo. Ningeomba tuongeze angalau asilimia kumi ili kasi ya umeme kwenda vijijini iwe kubwa zaidi na hiki cha kukaa hapa kuzungumzia mambo ya umeme tukifanya vizuri na kuwaimarisha hawa *REA* miaka mitano, kumi ijayo, tutasahau mambo ya umeme nchini mwetu; umeme utakuwa umesambaa maeneo yote yanayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie vyanzo; hata kama ni vidogo tunaweza tukapata umeme. Kwa mfano, kule ninakotoka Wilaya ya Hai, kipo chanzo cha zamani kidogo cha Kikuletwa. Nimeshakizungumzia sana, kwa bahati mbaya mitambo iliyoletwa pale ilikuwa imezeeka, lakini ikapuliziwa rangi ikaonekana kama mipya, ikafa baada muda sio mrefu. Kuna wataalamu walikuja pale na Wajapan wakaangalia na kufanya utafiti, ninadhani sio chini ya *megawatts* 20 ambazo zingeweza kuzalishwa pale, ambazo tungeweza kupata mahitaji ya Kilimanjaro na Arusha na umeme mwingine ukaweza kwenda mikoa mingine, pamoja na ku-*export.* Kwa hiyo, ningependekeza kupitia kwa wataalamu wetu Wizarani, vyanzo hata kama uzalishaji wake ni mdogo na sasa kwa sababu tumeruhusu sekta binafsi, viachiwe viweze kuzalisha umeme ili tuwe na umeme mwingi kushinda hata matumizi yetu na tuweze kuuza nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitishwa Muswada huu, niwapongeze sana Wabunge wenzangu, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Niungane na wenzangu kukiri kabisa kwamba, huu ndio Muswada ninadhani tangu tumeanza hili Bunge kwangu mimi ambaye ni kipindi cha kwanza, ninaona ni Muswada kamili, ila mambo mengine ya kuja na kutelezateleza, wanasema ikiwa rahisi sana nayo ni hatari sana. Niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge wote, mlionyesha uzalendo wa hali ya juu kabisa hatimaye marekebisho yakafanyika hadi leo kila mmoja ana raha moyoni mwake na sio sisi tu, hata wale tunaowawakilisha, ninatumaini nao wamefurahia. Nizidi kumwomba Mungu, aendelee kutujalia ujasiri, tusiweze kubabaishwa babaishwa; yale ya Kitaifa tuyazungumzie kwa lengo zuri na udhabiti mzuri pasipo kumwogopa yeyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, nimalizie tu kwa sababu na wengine wameshazungumzia, niwape *credit* wenzangu Waheshimiwa Wabunge; hili Bunge limekuwa *e-Parliament*. Bunge la kisasa, Bunge la Ki-*digital,* limeweza kuonyesha mambo mazito kabisa na kufanya wananchi wetu waanze kutuheshimu, kutupenda na kuwa na uhakika kwamba tunawawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana waliotangulia kuzungumza, nami ninazidi kusema kwamba, ninaunga mkono hoja na ninazidi kuwapa moyo vijana

wenzetu waendelee kufanya kazi. Tuko pamoja, msiwe na wasi wasi. Ninaunga hoja mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niwe msemaji wa mwisho kwa leo.

Kabla ya kuanza kuchangia, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii muhimu sana. Bila shaka, Mheshimiwa Rais anajua uwezo wako na wananchi wa Jimbo langu la Nyang'hwale, ambao ni jirani zako, wanakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni kati ya Muswada ambao umechambuliwa kwa kina kwa sababu umeshirikisha wadau wengi na tumekaa nao kwa muda mrefu sana, kwa kweli hatuna mashaka nao. Watanzania walikuwa wanafuatilia sana na mpaka sasa wanafuatilia kinachoendelea kuhusu Muswada huu kwa sababu juzi tumetoka kwenye matatizo ambayo yamesababishwa na mikataba mibovu ambao Wizara hii iliingia. Leo tunaendelea kuchambua Muswada huu ambapo tukishamaliza utakuwa Sheria na Sheria inaonekana ni nzuri sana lakini tukimaliza tu matatizo yanaanza na yanaanzia kule Serikalini ambapo wataingia mikataba ambayo inapelekea sasa kazi ianze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Bungeni tumekuwa tukilalamika kuhusu mikataba mibovu na wengi wamesema kuhusu mikataba hiyo, sina haja ya kurudia, lakini ni mingi kwa mfano mkataba wa *IPTL, Net Group Solution, Richmond, ATC* na mikataba ya madini, yote hii ni mikataba mibovu ambayo inapelekea Serikali inaonekana kwamba ni Serikali ya wezi na Serikali ya wezi wananchi hawaipendi na hata Mungu haipendi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika kitabu cha Isaya 1:23, Mungu anasema: "Yerusalemu, umezungukwa na wezi wapenda rushwa." Hata Mungu anachukia suala hilo, inabidi Serikali ikubali, ijisafishe kuanzia sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanakuja kwenye mikataba wakati Serikali inaposema mikataba ni siri na ni mali ya Serikali. Sisi Wabunge mara nyingi tumetaka kuiona mikataba hiyo lakini Serikali inasema tutakuwa tunaingia jikoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ile Ibara 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inasema: "Bunge ndilo litakuwa na mamlaka ya kuisimamia Serikali na kuishauri katika kutekeleza mambo yake". Kwa hiyo, Wabunge wanapohitaji mkataba wauone, wanafanya hivyo kwa mujibu wa Katiba. Sasa Serikali inapokataa au kutoa sababu hizi na zile, kwa tafsiri yangu ni kwamba Serikali moja kwa moja inavunja Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana, kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia hapa kwamba mikataba hii sasa, ni vizuri kama Wabunge watahitaji kuiona, tuione ili tusifikie mahali ambapo tupo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa kwenye Muswada huu. Ukiangalia katika *Order Paper* ya kila siku, maswali mengi sana yanahusu umeme kwa maana ya Wizara ya Nishati na Madini. Muswada huu umelenga kupeleka umeme vijijini; hapa ninaomba kutoa angalizo.

Katika nchi yetu kuna maeneo ambayo tayari yana miundombinu ya umeme na yana umeme na kwa bahati nzuri na miundombinu mingine kama vile barabara na maji lakini yapo maeneo ambayo hayana vitu vyote hivyo, hakuna umeme, hakuna barabara wala maji.

Maana yake ni kwamba kuna sehemu ya nchi ambayo iko kwenye mwanga na sehemu nyingine ya nchi iko gizani. Kwa hiyo, ninaomba baada ya kuanza kutekeleza Sheria hii, ni vizuri wakaangalia kipaumbele. Tupeleke kwanza sehemu ambapo kuna giza kabisa halafu baadaye tupeleke na huko ambako kuna umeme ili kuziba mapengo. Ninasema hivi kwa sababu inawezekana kabisa Mfuko huu wa *REA* hautatosheleza kuanza kufanya kazi nchi nzima, haiwezekani, tutaanzia na maeneo fulani na nitaomba sasa tuanzie na maeneo yale ambayo yana matatizo.

Huu ni karibu mwaka wangu wa kumi ndani ya Bunge hili lakini katika miaka yote nimekuwa nikitoa ombi la kupelekewa umeme katika maeneo ya Jimbo langu. Nyaya za umeme wa *grid* zinapita pale Karumwa kutoka Shinyanga kwenda kwenye Mgodi wa *Barrick* Bulyankhulu lakini kwa miaka tisa nimekuwa nikiomba umeme, siku moja wananchi wamenisaidia kwa maandamano, mpaka leo sijapata wakati umeme unapita pale. Sasa leo hii kwa maana ya Muswada huu, ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, anihakikishie kwamba sasa vijiji vyangu ambavyo nimekuwa nikivisemea kila siku vikiwemo vya Karumwa, Nyang'hwale, Bukwimbwa, Kafita, Kakora, Shabaka, Nyugwa na sehemu nyingine kama Nyarubere vinapata umeme kwa utaratibu huu. Maeneo haya Mheshimiwa Waziri anayajua na hili suala la Karumwa analijua na kwa bahati nzuri yeye ndiye Waziri na yeye kwake kuna matatizo, hakuna umeme vijiji vya Ngoma, Nyanchenche, Buyagu, Kasungamile na Katunguru. Vijiji hivyo Mheshimiwa Waziri, ukienda kule kama hutaviweka kwenye mpango huu, watakuuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku moja kwenye Kamati tulimuuliza Waziri mmoja kwamba Mheshimiwa mbona sasa wewe miradi hii unaipeleka kwako tu? Waziri akasema kwamba, jamani mpishi naye huonja. Sasa kwa utaratibu huo Mheshimiwa Ngeleja, mimi nitakuomba uonje lakini na mimi kwa kuwa nipo jirani pale Busolwa na vijiji vyote nilivyovitaja tuonje wote. Wakati wa kujibu, napenda kupata ahadi yako kwamba vijiji hivyo nilivyovitaja ni lini vitapata umeme? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sasa kuhusu *EWURA*. *EWURA* kwa maana ya Muswada huu kwenye kifungu cha 6(1) (a) – (h), watakuwa na mamlaka ya kusimamia masuala ya leseni, bei za umeme, haki na wajibu wa wamiliki wa leseni, kodi

na ushuru, haki na kinga kwa wateja, ufuatiliaji, ukaguzi, uchunguzi na utekelezaji wa masharti mbalimbali yanayohusiana na Sheria hii.

Liko tatizo kubwa sana, Watanzania wanalalamika kwamba kwa sababu ya biashara huria, vifaa vingi vya umeme ambavyo vimekuwa vikiingizwa kutoka nchi za mashariki za mbali, ni vifaa feki na matokeo yake nyumba nyingi sasa zimeathirika kwa maana ya kupata *shot* na kuungua. Hivi vitu vinafahamika, Serikali nayo inalifahamu suala hili, nayo imekuwa ikilalamika kwamba ni tatizo la *dumping* lakini wanaopata hasara ni wananchi. Kwa hiyo, ninaomba sasa *EWURA*, kwa Muswada huu, hili lipewe kipaumbele, lisimamiwe vizuri sana ili tatizo hili lisitokee kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa nijielekeze kwenye matatizo ya kukatika umeme. Ukatikaji wa umeme, nalo ni tatizo kubwa sana kati ya matatizo ambayo *TANESCO* wanayo. Mara kwa mara sehemu nyingi za nchi hii, umeme umekuwa ukikatika ila nashangaa hapa Bungeni hata lile Bunge refu la mwezi wa sita mpaka wa nane hatujakatikiwa na umeme.

**MBUNGE FULANI:** Jana ulikatika!

**MHE. DR. JAMES P. MUSALIKA:** Naambiwa jana ulikatika, lakini sehemu nyingi umeme unakatika. Linapotokea tatizo hilo, wakati mwingine *TANESCO* huwa wanatoa taarifa ya kuomba radhi kwamba kutakuwa na katizo la umeme kuanzia saa fulani hadi saa fulani lakini ni hasara kubwa kwa wafanyabiashara na kwa watumiaji kwa sababu inabidi sasa wengine wanunue *generators* ambapo hii ni gharama ambayo haipo kwenye mpangilio wa kwanza wa biashara, mtu analazimika kununua *generator* na *generator* ina gharama zake, anunue mafuta. Sasa hii ni hasara ambayo inasababishwa na katizo la umeme. Kwa bahati mbaya sana *TANESCO* wanaomba radhi tu kwamba bahati mbaya, kutakuwa na katizo la umeme.

*(Hapa umeme ulikatika)*

**MHE. DR. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika Muswada huu, ningependa kuona kipengele kinachomlinda mtumiaji kwamba, *TANESCO* au *Supplier* hiyo hasara wachangie *percent* fulani. Pia kwa sasa hivi kabla Sheria haijaanza, namwomba Mheshimiwa Waziri akubali pendelezo langu kwamba kwa kuwa *TANESCO* ukichelewa kulipa *bill* wanakukatia umeme lakini wao wasipo-*supply* umeme au wakikata, wanaomba radhi basi *na* watumiaji sasa hivi *tuw*e tunaandika hati kwamba tunaomba rad*hi, ha*tutaweza kulipa *bill* miezi miwili, mtuvumilie kwa sababu wao wanafanya hivyo, hatuwalalamikii na hatuwashtaki. *(Kicheko)*

Umeme huu utasaidia katika maeneo ya kwetu kwa sababu kuna wachimbaj*i wadogo wadogo k*wenye migodi ya dhahabu. Utasaidia kupunguza matumizi mabaya ya miti kwa sababu ndiyo chanzo cha energy peke yake huko. Pia utafufua viwanda vidogo vidogo huko, kwa mfano mashine za kukoboa mpunga, kusaga u*nga pa*moja na miradi mingine. Kwa hiyo, utaongeza ajira kule vijijini. Kama nilivyosema mara ya kwanza, kwa sababu hiyo ni vizuri, sasa Mheshimiwa Waziri akubaliane na mimi kwamba mfuko

huu wa REA uanzie katika maeneo ambayo yana historia hiyo ya kutokuwa na umeme, maeneo ambayo yako gizani ili sasa n*a s*isi tuwe na mwanga ili twende pamoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musalika, nakushukuru sana na hasa kwa staili yako leo ya kuomba umeme kwa Mheshimiwa Waziri, haijapata kutokea kabisa. Nafikiri Mheshimiwa Musalika, itabidi utuombe radhi, leo umetuchulia, umeme umekatika.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe tangazo moja. Katika orodha yangu niliyobakiwa nayo, wachangiaji watakaoanza kuchangia tena mada yetu wiki ijayo, siku ya Jumatatu, tutaanza na Mheshimiwa John Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi na wengine watafuata. Kabla sijaahirisha Bunge, ninaomba nitoe tangazo la semina. Ofisi ya Spika, imeomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho Jumamosi, tarehe 19 Aprili, 2008 na Jumapili tarehe 20 Aprili, 2008 hakutakuwepo na semina kama ilivyotegemewa. Waliokuwa wanaandaa Semina hizo, wameahirisha kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wao hadi hapo watakapotujulisha tena. Kwa hiyo, Jumamosi na Jumapili, hakutakuwa na semina. Tangazo lingine, wachezaji wa timu za Bunge wataendelea na mazoezi kama kawaida kutokana na taratibu zetu kama tulivyojipangia.

Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana. Nawatakia *weekend* njema na niwatakie maandalizi ya kuanza kazi itakayoanza Jumatatu.

Baada ya kusema hayo, naomba sasa niahirishe Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi, ahsante sana.

*(Saa 01.46 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu, Tarehe 21 Aprili, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*